# Nipashe

Jumatano Julai 31, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579984

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mawakili 15 watoana jasho saa 5 ma-DED kusimamia uchaguzi

UKURASA 3



Ukurasa 18

Washirika wa Marekani wa mtaka Jenerali Haftar, waipuuza UN

TUJIKUMBUSHE: YAKUBU GOWON

Ukurasa 19

Kimataifa

siasa

JUMATANO JULAI 31, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

EAC isipuuzie mgogorohuu wa Rwanda, Uganda

Ukurasa 14

BAADA YA MIAKA 55

Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-7

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa Serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua.

Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya saba ya kitabu hicho inayoanzia na Changamoto ya Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

5.3 Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano

Hii nayo imekuwa ni kero kubwa kwa upande wa Zanzibar. Tarehe 2 Desemba, 1994, Bunge la Jamhuri ya Muungano ilipitisha mabadiliko kumi

Endelea 16

Mbunge aliyeng'ong'wa na Trump aipania Israel, haigusi Somalia

Ukurasa 20

Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. PICHA: MTANDAO

Ripoti ya mauaji yazusha maandamano mapya Sudan

Ukurasa 17

UKURASA 13

# Magufuli, Mbowe wakutana msibani

• **Wakaa** pamoja na kuteta mambo... *Endelea ukurasa wa 2*





Rais John Magufuli, akizungumza na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), na Mbunge wa Hai, Freeman Mbowe, wakati alipokwenda kuhani msiba wa Meja Jenerali mstaafu marehemu Albert Lameck Mbowe, nyumbani Salasala, jijini Dar es Salaam jana. Meja Jenerali Mbowe ambaye ni kaka wa Freeman, alifariki Julai 28, 2019, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alikokuwa akipatiwa matibabu. Kulia ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo. **PICHA: IKULU**

## PSSSF yatumia vikokotoo viwili

UKURASA 3



## Polisi waanika sababu mwandishi kukamatwa

UK. 2

**MICHEZO** **AZAM, POLISI TANZANIA KUTOANA JASHO** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# JPM, Mbowe wakutana msibani

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, jana alikwenda nyumbani kwa marehemu Meja Jenerali Mstaafu, Albert Mbowe, kutoa salamu zake za pole na kupokewa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe.

Meja Jenerali mstaafu Mbowe alifariki dunia Jumapili katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Baada ya kuwasili nyumbani kwa marehemu Salasala jijini Dar es Salaam jana asubuhi, Rais Magufuli alikutana na familia hiyo iliyoongozwa na Mbowe ambaye ni mdogo wa marehemu.

Akiwa kwenye familia hiyo, Rais Magufuli alitoa pole kwa kupeana mikono na Mbowe ambaye pia ni Mbunge wa Hai mkoani Kilimanjaro.

Rais Magufuli pia alisalimiana na ndugu, jamaa na marafiki waliofika kutoa pole na baadaye aliingia ndani kukutana na familia ambayo alizungumza nayo na kutoa neno la faraja kwao.

Kabla ya kuondoka, Rais Magufuli aliungana na familia hiyo kufanya sala ya pamoja huku wakiwa wameshikana mikono, wa pembeni yake akiwa ni Mbowe.

Baada ya sala hiyo, Rais Magufuli alitaka familia hiyo iendelee kuwa na umoja kama ilivyokuwa wakati wa uhai wa Meja Jenerali mstaafu Mbowe na wamtangulize Mungu.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alisema pamoja na kustaafu Meja Jenerali Mbowe alikuwa mshauri wa karibu wa jeshi.

Alisema katika utumishi wake wa miaka 36 na siku 27 jeshini, alitoa mchango mkubwa katika masuala ya fedha.

Meja Jenerali mstaafu, Mbowe, alizaliwa Januari mwaka 1953 na alijiunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ) mwaka 1973 na alistaafu utumishi jeshini mwaka 2009.



Mshtakiwa Khamisi Saidi akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, na kusomewa shtaka la kumuua mke wake aitwaye Naomi Marijani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Nape asema hana kinyongo na serikali

**Na Mary Geofrey**

MBUNGE wa Mtama, Nape Nnauye, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni chama cha wakulima na wafanyakazi ndiyo maana amekuwa akiwatetea wakulima wa korosho, zao ambalo kwa asilimia kubwa linazalishwa mikoa ya kusini.

Nape aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa jimbo hilo katika mkutano wa hadhara kuhusu zao la korosho na kusema hana ubaya na mtu wala kinyongo na serikali zaidi ya kuwatetea wananchi wake.

"CCM ni chama cha wakulima na wafanyakazi, sina jambo baya na mtu, sina kinyongo na serikali yangu, lakini tuliwaahidi tutasimamia haki yenu," alisema Nape.

Alisema ana matumaini na serikali kuwa itarekebisha kasoro zilizojitokeza hasa kuondoa korosho zilizoko kwenye maghala kabla ya msimu mpya wa zao hilo haujafika.

"Kazi yangu kuhakikisha watu wangu wanalipwa na mimi matumaini yangu baada ya muda huu wa milima na mabonde, serikali imejifunza watarekebisha mambo. Ninayo matumaini kwamba korosho zilizoko kama bado nzima itapata soko. Ni matumaini yangu juhudi zinazofanywa na serikali kuondoa hizo korosho zifanyike mapema maana zisipotoka korosho mpya hazina pa kukaa," alisema.

"Nilipokuwa bungeni ndiyo maana mbunge wenu nikawa mkali. Wako watu wanasema Nape mkali na wakati mwingine wakubwa wanachukia, lakini nasema bora nichukiwe lakini watu wangu waone nimesimamia haki yao."


IN LOVING MEMORY



115351902

PATRICK LUCIAN MATERU
21st MARCH 1986 - 31st JULY 2011

BELOVED PATRICK, TODAY IT IS EXACTLY EIGHT YEARS SINCE YOU DEPARTED FROM US. WE LOVED YOU DEARLY, BUT IT PLEASED THE LORD TO CALL YOU BACK HOME. WE THANK THE LORD FOR PRECIOUS GIFT OF ALLOWING US TO SHARE YOUR LIFE, BEING BLESSED IN MANY DIFFERENT WAYS TILL THE DAY HE TOOK YOU FROM US. THE TIME SEEMS TO BE SHORT LIVED, YOUR MEMORY UNFORGETABLE, EXPERIENCES LEARNED AND LIVES TO BE TREASURED IN OUR HEARTS FOREVER.

YOU ARE FONDLY REMEMBERED AND MISSED BY YOUR BELOVED FATHER, MOTHER, BROTHER, SISTER, RELATIVES ,FRIENDS AND YOUR CO WORKERS IN THE MINISTRY OF HEALTH. WE CAN NOT FORGET THE TIME WE SPENT AS FAMILY.

The Lord gave and has taken away, may God rest your soul in eternal peace AMEN.


# Polisi wataja sababu mwandishi kukamatwa

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linamshikilia Mwandishi wa Habari za Kiuchumi, Erick Kabendera (39), kutokana na kitendo chake cha kukaidi wito baada ya kumwandikia barua.

Juzi, kulisambaa kwenye mitandao ya kijamii taarifa zilizomhusu mwandishi wa habari huyo na vitendo vya utekaji baada ya kudaiwa kuchukuliwa nyumbani kwake Mbweni jijini na watu wasiojulikana.

Hata hivyo, akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema Kabendera hajatekwa bali alikamatwa kutokana na kitendo chake cha kukaidi wito wa jeshi hilo.

Alisema awali mwandishi huyo aliandikiwa barua ya wito wa kufika Jeshi la Polisi kwa ajili ya mahojiano lakini alikaidi.

"Mtuhumiwa huyu kuna mashaka makubwa kuhusiana na uraia wake, tutakapobaini mara moja tutamkabidhi kwenye Idara ya Uhamiaji ili kushughulika naye na ndiyo maana alikuwa akikaidi wito wa polisi na kujihami kuwa ametekwa," alisema.

"Niseme kuwa mwandishi huyu hajatekwa ila tumemkamata kwa mahojiano. Utii wa sheria bila shuruti ni muhimu sana kuzingatiwa kwani ukishindwa kutii sheria inakuwa shuruti."

### AJIFANYA POLISI

Katika tukio lingine, jeshi hilo linamshikilia Ramadhan Iddy (23), mkazi wa Tabata Segerea, kwa tuhuma za kujifanya ofisa wa polisi.

Kamanda Mambosasa alisema Iddy alikamatwa Julai 19 baada ya kupata taarifa kutoka kwa askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makao Makuu Mlalakuwa kuwa kuna kijana amevaa sare za Jeshi la Polisi na wanamtilia shaka.

"Makachero walifika Makao Makuu ya JKT na kumkamata na alipohojiwa, mtuhumiwa huyo alikiri kujifanya ni ofisa wa polisi na kufanya utapeli," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema kijana huyo alikiri alipitia mafunzo ya JKT huko Mafinga mwaka 2006 na kujitolea kwa mujibu wa sheria katika kambi hiyo.

"Upekuzi ulipofanyika, alikutwa na sare moja ya polisi aina ya kaki, vyeo vya Koplo, Sajenti na mkaguzi msaidizi, pea moja ya kombati Jungle Green, pingu moja, kofia moja ya askari wa usalama barabarani, redio ya upepo aina ya Motorola, mikanda miwili ya JKT, mkanda mmoja wa bendera ya Jeshi la Polisi na buti na viatu vya kawaida," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema upekuzi wa kina unaendelea kufanyika na kwamba mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

## HABARI KIMATAIFA

# PSSSF yalipa mafao kwa vikokotoo viwili

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umesema unalipa mafao kwa kutumia vikokotoo viwili kutokana na kuunganishwa kwa mifuko minne kuunda.

Akiwasilisha mada ya mwamko na mafao ya mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma kwenye semina ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja Matekelezo wa PSSSF, Victor Kikoti, alisema hali hiyo itaendelea hadi yatakapofanyika marekebisho ya sheria mwaka 2023.

Alisema waliokuwa wanachama wa PSPF na LAPF, kikokotoo chao ni cha mkupuo wa asilimia 50 na wanalipwa kwa kiwango hicho kutokana na maelekezo ya serikali ya kurudi kwenye kikokotoo cha zamani kwa kila mfuko.

Alisema kwa wanachama wa mifuko ya PPF na GEPF, wanalipwa kwa kikokotoo cha asilimia 25 kwa mkupuo, kwa kuwa ndicho kilichokuwa kinatumika kabla ya kuunganishwa.

"Kabla ya sheria mpya, kila mfuko ulikuwa na kikokotoo chache, taratibu zake na mifumo yake, baada ya kuunganisha ilipaswa kuwe na kikokotoo kimoja, lakini kwa agizo la Rais John Magufuli ni kwamba kila mfuko utarudi kwenye kikokotoo chake hadi mwaka 2023 kutakapokuwa na mwafaka wa fomula," alisema.

Katika hatua nyingine, PSSSF imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.7 kwa miezi nane kutoka kwa waajiri 106 ambao hawakupeleka michango ya wanachama kwa mujibu wa sheria.

Meneja wa Sheria wa PSSSF, Mkenda Kileo, alisema jana kuwa Sheria Na. 2 ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018 inamtaka mwajiri anayechelewesha michango kutoa fedha anazodaiwa kabla ya kupata haki ya kusikilizwa.

Alisema kwa sheria hiyo, waajiri waliofikishwa mahakamani kabla ya kupewa haki ya kujitetea, walilipa michango wanayodaiwa pamoja na faini ya asilimia 1.5 na ndipo walipata haki ya kijitetea na kesi kuendelea.

Alisema wengi wa waajiri wameomba muda wa ziada kwa kuandikisha mbele ya mahakama ili walipe kidogokidogo fedha wanazodaiwa na kwamba sheria mpya imesaidia kuondoa usumbufu na kesi sugu.

Alisema kuna kesi 80 zilizoko mahakamani ambazo zilianza kwa sheria ya zamani na zilitoka kwenye mifuko ya GEPF, PPF, PSPF na LAPF na wanaendelea nazo.

Kwa mujibu wa Kileo, PSSSF imerithi michango, mali na uwekezaji ulikuwa chini ya mifuko iliyounganishwa na kuunda mfuko.

"Wanachama wa PSSSF ni wale walioko kwenye sekta ya umma na mashirika ambayo serikali ina hisa kuanzia asilimia 30 kwenda juu," alisema.

"Kama mwajiri atatimiza wajibu wake, mfuko utatakiwa kulipa mafao ndani ya siku 60, zaidi ya hapo mfuko unatozwa faini ya asilimia tano ya malipo stahiki," alisema.

# Samia awaonya wanaume wanaopapasa mama ntilie

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameonya tabia ya wanaume kuwadhalilisha wafanyabiashara wa kike sokoni kwa kuwashika viungo vyao huku akiwataka wanaofanyiwa vitendo hivyo watoe taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Samia alitoa onyo hilo jana jijini hapa alipozindua mradi wa kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto kwenye maeneo ya masoko ambao utatekelezwa jijini na katika Mkoa wa Shinyanga.

Mradi huo unatekelezwa na Jumuiya ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Alat) kwa ufadhili wa Shirika la UN-Women.

Samia alisema matumizi ya lugha chafu, kuwashika maungo pamoja na vitendo vya kiudhalilishaji dhidi ya wanawake havikubaliki kwa kuwa wanawake na wanaume nchini wanalindwa na katiba na wana fursa sawa kushiriki shughuli za kiuchumi. Alisema mama ntilie ndiyo wamekuwa waathirika wakubwa wa vitendo vya udhalilishaji huo.

"Vitambulisho vya ujasiriamali ni kwa wote - wanaume na wanawake na wote wana haki ya kukaa kwenye soko na kufanya biashara, sasa anayekuja kukudhalilisha huyo anavunja sheria, ni lazima ashughulikiwe," alisema.

"Bado tunashuhudia wanawake wanakumbana na vitendo visivyoridhisha vinavyowarudisha nyuma kimaendeleo na hivyo kuwanyima fursa za kiuchumi."

Alisema mama ntilie wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo na ubabe na maneno ya kejeli yamekuwa yakielekezwa kwao na baadhi ya wateja baada ya kula na kukataa kulipa.

"Masuala hayo yanavunja heshima ya wanawake kwenye masoko, yanamfanya ajisikie vibaya hata pale mwanawe anapokuja kumpokea anapotoka kazini kwa kuwa wanashuhudia wakitolewa lugha chafu, kushikwa matiti. "Hivi ni kwanini msishikane wanaume kwa wanaume? Wanawake wanaumia kisaikolojia. Unakaa sokoni unavurumsha matusi kwa viungo vya mwanamke, wewe ulitoka wapi au mwanamke unayemtukana ana tofauti gani na mama aliyekuzaa?

# Mawakili 15 wanyukana saa 5

**Na Enock Charles**

KESI ya kupinga wakurugenzi wa majiji, miji na manispaa kusimamia uchaguzi imechukua sura mpya baada ya serikali kutoa hoja 11 katika rufani dhidi ya uamuzi uliotolewa na Mahakamu Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Katika uamuzi huo, Mahakama Kuu ilifuta kifungu cha 7(1) na 7(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kinachoipa mamlaka Tume ya Uchaguzi (NEC) kuteua wakurugenzi hao kusimamia uchaguzi.

Jopo la mawakili 10 wa serikali likiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Clement Mashamba, jana lilitoa hoja hizo katika Mahakama ya Rufani kuiomba kutupilia mbali uamuzi huo pamoja na kuamuru wafungua mashtaka kulipa gharama za kesi hiyo.

Wakitoa hoja zao, mawakili wa serikali walidai kuwa wakurugenzi hao si wahusika pekee katika uchaguzi na kwamba kuna wahusika wengine ambao kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi katika mchakato wa uchaguzi. Pia walidai kuwa mahakama imepora mamlaka ya bunge ya kutunga sheria ya kuweka taratibu za kusimamia uchaguzi.

Pia mawakili hao wa serikali walidai Mahakama Kuu ilishindwa kutambua kazi nzuri zinazofanywa na wakurugenzi wa majiji, miji na manispaa katika kuwaletea maendeleo wananchi na kwamba imeshindwa kutambua nguvu ya kiapo wanachokiapa wakurugenzi hao kabla ya kusimamia uchaguzi nchini.

Walidai kuwa iko sheria inayowawajibisha wakurugenzi hao wanapokwenda kinyume cha sheria na taratibu zinazosimamia uchaguzi huo na kuwa hapakuwa na haja ya kuwaondoa katika mchakato mzima wa kusimamia uchaguzi.

Katika kesi ya msingi, iliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Bob Wangwe, aliitaka Mahakama kubatilisha kifungu cha 7(1) na 7(3) cha Sheria ya Uchaguzi kinachoipa mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuteua wakurugenzi wa majiji, miji na manispaa kuwa wasimamizi wa uchaguzi jambo alilodai linakiuka Katiba ya nchi inayotaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa huru na wasimamizi wa uchaguzi kutojiunga na vyama vya siasa.

Katika kesi hiyo iliyosikilizwa kwa saa tano mfululizo na jopo la majaji watano wa Mahakama ya Rufani wakiongozwa na Jaji Augustine Mwarija, upande wa wajibu rufani ukiwa na mawakili watano wakiongozwa na Wakili Fatma Karume uliibuka majibizano makali ya hoja za kisheria baina yao mawakili wa serikali.

Wakijibu baadhi ya hoja hizo, mawakili wa wajibu rufani walidai kazi nzuri zinazofanywa na wakurugenzi haziwezi kuhalalisha kuvunjwa kwa Katiba ya nchi inayotaka uchaguzi kuwa huru na haki.

Kuhusu kiapo wanachoapa wasimamizi hao kabla ya kusimamia uchaguzi, mawakili hao walidai ni kinyume cha Katiba kwa kuwa hairuhusu wasimamizi hao kuwa na vyama na kwamba hakuna haja ya kuwa na msimamizi anayetiliwa shaka badala yake, tume iweke watu wasiokuwa na rekodi ya kuwa na uanachama wa chama chochote cha siasa.

Kuhusu hoja ya kuwapo sheria inayoweza kuwawajibisha wasimamizi wa uchaguzi pindi wanapobainika kuvunja sheria za uchaguzi, wajibu rufani walidai kuwa ni muhimu kudhibiti uwezekano wa kuvunjwa kwa sheria kuliko kutegemea kujibu matokeo ya kuvunjwa kwa sheria.

EBRAHIM HAJI CHARITABLE HEALTH CENTRE KWA KUSHIRIKIANA NA SHALBY MULTI-SPECIALITY HOSPITALS IMEANDAA KAMBI YA UCHUNGUZI WA MATATIZO YA MIFUPA NDANI YA TANZANIA



DR PRANAY GUJJAR

Daktari Bingwa wa mifupa atatoa ushauri nasaha kwa watu wanaosumbuliwa na maumivu yafuatayo:

- Maumivu ya Magoti
- Maumivu ya Bega
- Maumivu ya Nyonga
- Na mengineyote yanayo husiana na viungo

TAREHE: 31 JULAI 2019

SEHEMU

Ebrahim Haji Charitable Health Centre, Asia Street, P.O. Box 14861, Dar Es Salaam, Tanzania

KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NASI KWA NAMBA ZILIOPO CHINI

+255 2114996 / +255 713873830

SHALBY HOSPITALS, AHMEDABAD (INDIA)
+91 95740 77720
E: international@shalby.org | W: www.shalby.org

SHALBY MULTI-SPECIALTY HOSPITALS

Tafadhali njoo na x-ray zako za nyuma na ripoti yako wakati waushauri

215353402

## HABARI KIMATAIFA

# Diwani aeleza alivyoacha nyumba, mali kukataa kurithiwa na shemeji

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

DIWANI wa Kata ya Mahenge, Kilolo mkoani Iringa, Shella Ngailo, amesema alikimbia nyumba na kuacha mali zote walizochuma na mumewe kwa kukwepa kurithiwa na shemeji yake ambaye ni mdogo wa marehemu.

Ngailo alitoa ushuhuda huo hivi karibuni wakati wa Kikao Kazi cha Shirika la lisilo la kiserikali la Iringa Civil Society Organization (ICISO-Umbrella) kilichofanyika katika mji mdogo wa Ilula, wilayani Kilolo.

Alisema baada ya mume wake kufariki dunia mwaka 1997 na baada ya kumalizika msiba, alipewa kikombe cha pombe ya kienyeji na upande wa mume wake na kumtaka akabidhi kikombe hicho kwa mtu yeyote wa kiume isipokuwa mtoto.

Kutokana na maelekezo hayo, alisema alimpa kikombe mdogo wa marehemu mumewe (shemeji) ndipo walipomweleza kuwa huyo ndiye mume wake mbadala.

Shirika la ICISO linatekeleza mradi wa umiliki sawa wa ardhi na mali zinginezo kwa wanawake na watoto wa kike tangu mwaka 2017 wilayani humo.

Alifafanua kuwa yeye ni miongoni mwa watu walionufaika na mradi wa umiliki wa ardhi na mali zinginezo unaotekelezwa na ICISO kwa Wilaya ya Kilolo.

Ngailo alisema tangu mradi huo umeanza kutekelezwa katika wilaya hiyo, wanawake wengi wameanza kudai haki ya kumiliki ardhi na uelewa umeongezeka tofauti na hapo mwanzo wanawake walikuwa gizani.

Pia alisema serikali za vijiji zimeanza kugawa ardhi na kuwatazama wanawake wakati wa ugawaji wa ardhi ya kijiji na hata familia mbalimbali nazo zimeondokana na mfumo dume wa kupendelea wanaume tu na kuwanyima haki ya kumiliki ardhi wanawake na watoto wa kike.

"Kabla ya mradi wa usawa wa kumiliki ardhi na mali zinginezo katika Kata ya Mahenge, wanawake na watoto wa kike wengi walikuwa gizani. Hawakupata haki ya kumiliki ardhi isipokuwa wanaume na watoto wa kiume," alisema.

Alisema mwaka 1997 ni mwaka aliyefariki dunia mumewe na mali zote kuchukuliwa na baba mkwe baada ya kukataa kurithiwa na shemeji yake.

"Niliondoka nyumbani na watoto wangu na kwenda kuishi kwa wazazi wangu na kuanza maisha mapya na kujihusisha na masuala ya kisiasa ndipo nilichaguliwa kuwa diwani viti maalum na baada nikagombea nafasi tena pamoja na wanaume na kuchaguliwa kuwa diwani wa Mahenge-Kilolo, mwanamke ni kujiamini kila ulifanyalo utafanyikiwa," alijigamba.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata ya Image, Ahmad Abdallah, ameishukuru ICISO kwa kutoa elimu ya usawa wa umiliki wa ardhi na mali zinginezo katika kata hiyo ambako kumekuwa na mabadiliko chanya. Alisema kumekuwapo na mabadiliko kwa kiasi kikubwa wanawake pamoja na wanaume wamepata elimu ya usawa hivyo kupunguza migogoro katika maeneo mengi ya vijiji.

Abdallah alitoa mfano kwa Kijiji cha Iyai, ambapo kulikuwa na matatizo ya migogoro ya ardhi na kufanya Baraza la Ardhi kuzidiwa na mzigo wa kutatua migogoro pamoja na mfumo dume wa kuwapendelea wanaume kuliko wanawake.

Alisema kuwa Baraza la Ardhi la vijiji vingi vilizidiwa na migogoro ya ardhi lakini baada ya ICISO kufika katika maeneo yao kutoa elimu ya umiliki wa ardhi kwa kuzingatia jinsia mambo yamebadilika.

Katibu Mtendaji wa ICISO-Umbrella, Raphael Mtitu, alisema shirika lake limekuwa likifanya kazi mkoani Iringa tangu 2017 na linatekeleza mradi umiliki sawa wa ardhi na mali zinginezo kwenye vijiji vya wilaya za Kilolo na Iringa.

Alisema kuwa kipindi chote wamekuwa wakifanya mikutano, midahalo, mafunzo mbalimbali kwa vikundi na mikutano ya viongozi wa vijiji.

## Wanafunzi 190 kuonyesha ubunifu wa kisayansi

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI 190 kutoka katika shule mbalimbali za sekondari nchini wanatarajiwa kuonyesha kazi zao za kisayansi katika maonyesho ya tisa ya wanasayansi chipukizi yanayotarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia leo na kesho jijini Dar es Salaam.

Kazi hizo ni walizoziandaa kwa kipindi cha mwaka mmoja kupitia mpango wa mafunzo ya kisayansi shuleni unaoendeshwa na taasisi ya Young Scientists Tanzania (YST).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, alisema wanafunzi watakaoshiriki maonyesho hayo watapata fursa ya kuboresha ujuzi wao wa kisayansi.

"Tulipoanza tulipokea miradi 327, na washindi walichujwa mara mbili, mchujo wa kwanza 120 na wa pili ulikuwa wa miradi 95 kutoka shule 79 ambao ndiyo ulikuwa na wanafunzi 190 walioshinda na wataambatana na walimu 85 kutoka shule mbalimbali nchini," alisema.

Alisema wanasayansi chipukizi watakaokuwa na ugunduzi mzuri

INAENDELEA UK. 8






Baadhi ya waombolezaji wakitoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Agnes Kabigi nyumbani kwake Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika katika makaburi ya Kwa Kondo Bahari Beach. Marehemu Kabigi alikuwa Meneja Mawasiliano wa Shirika la AGPAHI. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mil. 500/- kujenga hosteli

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeahidi kukipatia Sh. milioni 500 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Karume Zanzibar ili kujenga hosteli za wanafunzi ambazo ni moja ya changamoto zinazokikabili.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, aliyasema hayo jana muda mfupi baada ya kutembelea kampasi hiyo na kukagua maeneo yake na kuzungumza na wafanyakazi.

"Wizara inatambua umuhimu wa elimu na ndiyo maana inajitahidi kwenda na kasi na kauli ya Rais John Magufuli ya hapa kazi tu," alisema.

Aliongeza kuwa fedha hizo zitatolewa mapema ili kuunga mkono jitihada za chuo za kutumia mapato yake ya ndani kwa kujenga miundombinu ya kutolea elimu bora.

Alisema Wizara ya Elimu inafanya kazi katika kuendeleza falsafa ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ya kufuta ujinga, umaskini na maradhi.

Alisema wizara itasaidia ujenzi wa hosteli hizo ili uanze mapema na kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi.

Pia, aliwapongeza wafanyakazi wa kampasi hiyo ya Zanzibar kwa jitihada zao kuhakikisha chuo kinajulikana hadi kuaminika na wananchi visiwani huko.

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema katika kampasi hiyo, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa imeongezeka kutoka 22 hadi ya 1,000.

Alisema changamoto zinazoikabili kampasi hiyo ni kukosekana kwa hosteli za wanafunzi, uvamizi wa maeneo ya chuo na upungufu wa wafanyakazi.

Mkuu wa Kampasi ya Karume Zanzibar, Rose Mbwete, aliahidi kuwa chuo hicho kitashirikiana na mamlaka zote husika katika kuhakikisha kinatekeleza majukumu yake vyema kwenye jamii ili kuinua viwango vya elimu nchini.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yasema ombaomba wamevuka mipaka

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema wapo baadhi ya watu wanaofanya biashara haramu ya usafirishaji binadamu kwa kuchukua watoto na walemavu kuwapeleka nje ya nchi kuwa ombaomba.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya kupinga biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Katika maadhimisho hayo, waziri huyo alisema wanaofanya biashara hiyo haramu, mwisho wao umefika na kuwataka watafute shughuli nyingine.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2016, wadau wameokoa jumla ya waathirika 390. Kati yao, wanawake ni 373 na 320 walikuwa chini ya umri wa miaka 18.

"Biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu inafanyika dhidi ya watoto au walemavu wa miguu kwa ajili ya kuwatumikisha kama ombaomba kwenye mitaa yenye mkusanyiko wa watu au barabara zenye foleni.

"Serikali inafanya mawasiliano na mamlaka za Kenya ili kuwarejesha watoto watatu wa Kitanzania waliookolewa huko wakiwa wanatumikishwa kuomba fedha ambapo kati yao wawili ni walemavu.

"Ninatoa onyo na ole wao, yeyote ambaye anamchukua mtoto au mtu yeyote kwa kumdanganya na kumfanya mtumwa ama wa kumbebea dawa za kulevya au kuuza pombe haramu ya gongo au kufanya uhalifu mwingine wowote pamoja na danguro, waache kwa sababu tunakaribia kuwafikia," alisema.

Alisema baadhi wamewachukua watu na kwenda kuwatumikisha kwenye mashamba, viwandani na wengine nyumbani.

Waziri Lugola alitaja mikoa inayoongoza kwa utumikishaji wa biashara hiyo kuwa ni Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Geita, Dodoma, Singida, Shinyanga, Tanga na Morogoro.

Pia alisema katika kipindi cha miaka minne kilichoanzia mwaka 2016, Jeshi la Polisi lilifanya upepelezi wa matukio 50 ya aina hiyo dhidi ya watuhumiwa 76.

"Watuhumiwa 60 walipatikana na hatia na kuhukumiwa kulipa faini au kutumikia kifungo. Kati ya hao 60, wanawake ni saba.

"Waathirika wengi wanaosafirishwa nje ya nchi wanatoka Dar es Salaam, Tanga na Dodoma (hususan wilaya ya Kondoa) na wachache mikoa mingine," alisema.

Lugola aliongeza kuwa waathirika wengi wa biashara hiyo ni wanawake wenye umri kati ya miaka 16 hadi 26 ambao hupelekwa nchi za India, Thailand, China, Indonesia na Malaysia kwa ajili ya kutumikishwa biashara ya ukahaba.

Alisema wengine hutumikishwa kazi za ndani katika nchi za Oman na baadhi uarabuni ikiwamo Irak.

"Vyombo vya ulinzi na usalama vitaendelea kuwasaka na kuwachukulia hatua wote wanaohusika na biashara hii, Watanzania wasidhani vita hii ni nguvu ya soda mapambano haya ni endelevu hadi mfanyabiashara haramu wa mwisho atakapotiwa mkononi au yeye mwenyewe kujisalimisha," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Biashara hiyo, Vincent Magere, alisema mwaka 2018/19, wahalifu waliokamatwa ni 36, kesi zilizofikishwa mahakamani ni 33, waathirika waliookolewa ni 147. Kati yao, 141 walikamatwa Tanzania na sita nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mussa Zungu, alisema changamoto hiyo itakwisha kwa asilimia 100 ikiwa wananchi watasaidia kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama.

# Mamia wamzika Agnes Kabigi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMIA ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam wakiongozwa na wanahabari, jana walijitokeza kwa wingi kuaga na kuzika mwili wa mwanahabari mbobezi, Agnes Kabigi, aliyefariki dunia wiki iliyopita akiwa kazini, Kahama mkoani Shinyanga.

Kabigi (52), alizikwa katika makaburi ya Kondo, Kunduchi jijini Dar es Salaam.

Wakati mamia hao wakimsindiza mpendwa wao kwa mara ya mwisho, aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Betty Mkwasa, akitoa siri ya mipango waliyopanga kwa mara ya mwisho na Kabigi.

Akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya kundi la fursa ambalo Kabigi alikuwamo, Mkwasa alisema wiki chache zilizopita, alimshirikisha mipango yake ya kufungua bucha ya kisasa, hivyo wakapanga kwa pamoja kwenda nchini China kwa ajili ya kununua mashine.

"Wiki chache zilizopita, Agnes (kabigi) mbali na kufanya kazi za kuajiriwa pia alinishirikisha kwamba anataka kufungua bucha ya kisasa kwa sababu alikuwa anafanya pia mambo ya ujasiriamali. Tulipanga kwamba Oktoba tungesafiri kwenda China, lakini cha kushangaza aliniambia tena kwamba anaona kwamba ni mbali na leo (jana) nimegundua kwa nini alisema Oktoba ni mbali,"alisema Mkwasa.

Akisoma risala kwa niaba ya familia katika ibada ya kuaga iliyofanyika nyumbani kwa marehemu, Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, mmoja wa

INAENDELEA UK.8

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **BOSTON AUCTION COMPANY & JOSINA AUCTION MART,** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba husika ilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE | MAHALI ILIPO DHAMANA NA KAMPUNI INAYOUZA | MUDA WA MNADA | AUCTION COMPANY. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAHEGERE/MARWA,FRANCIS | MPEMBE/MICHAEL,JEREMIAH | NYUMBA | 16/8/2019 | BUSWELU | SAA5:00 ASUBUHI | BOSTON AUCTION COMPANY |
| 2. | KISUMHO/N,ROZA | KISUMHO/N,ROZA | KIWANJA | 17/8/2019 | KATORO | SAA5:00 ASUBUHI | JOSINA AUCTION MART |
| 3 | MASOTA/ELIKANA,BENJAMIN | DICKSON/J,MARY | NYUMBA | 16/8/2019 | IGOMA | SAA5:00 ASUBUHI | BOSTON AUCTION COMPANY |
| 4 | ISONZO/J,MAYUNGA | MTONI/I,HASSANI | NYUMBA | 19/8/2019 | BUNDA | SAA5:00 ASUBUHI | BOSTON AUCTION COMPANY |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.

ii. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

iii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

**Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na**
**Mratibu wa MIKOPO,**
**AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**S.L.P. 95068,**
**Dar Es Salaam.**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**Simu: JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER 0713203040/ 0768203040**
**BOSTON AUCTION MART 0766547732/ 0717494900/ 0786600606**

215351402

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **ANDAN GROUP COMPANY LIMITED & BOSTON AUCTION MARTS,** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba husika ilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE | MAHALI ILIPO DHAMANA NA KAMPUNI INAYOUZA | MUDA WA MNADA | AUCTION COMPANY |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAKELELE/INGOMBE,KA SHINDYE | MAKELELE/INGOMBE,KA SHINDYE | NYUMBA | 16/08/2019 | ISAKA | KUANZIA SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 2. | BUNDALA/R,ALLY | BUNDALA/R,ALLY | SHAMBA | 19/08/2019 | SUNGE | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 3 | LUTEGE/M,ADAM | LUTEGE/M,ADAM | NYUMBA | 14/08/2019 | BULUNGWA/USHETU | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 4 | DUWA/J,ROSEMARY | DUWA/J,ROSEMARY & MAGENI/D,ALEXANDER | NYUMBA(2) | 15/08/2019 | MAJENGO & MBULU | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 5 | PELEKA/N,ROBERT | PELEKA/N,ROBERT | NYUMBA | 13/08/2019 | SEGESE | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI | ANDAN GROUP LIMITED |
| 6 | WILLY/W,ELIAS | WILLY/W,ELIAS | NYUMBA | 15/08/2019 | MALUNGA | KUANZIA SAA 9:00 MCHANA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 7 | WASILE/Z,LEONARD | WASILE/Z,LEONARD | NYUMBA(2) | 17/08/2019 | RUNZEWE | KUANZIA SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 8 | SHAGEMBE/NGWATA,AS TELIA | SHAGEMBE/NGWATA,AS TELIA | NYUMBA | 17/08/2019 | RUNZEWE | KUANZIA SAA 9:00 MCHANA | ANDAN GROUP LIMITED |
| 9 | DOTTO/CHARLES,RENATUS | DOTTO/CHARLES,RENATUS | NYUMBA | 19/08/2019 | MALUNGA | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI | ANDAN GROUP LIMITED |
| 10 | NYEREMA/MATIKU,MTONDI | NYEREMA/MATIKU,MTONDI | GARI T915CBU TOYOTA | 09/08/2019 | MWANZA | KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI | BOSTON AUCTION MARTS |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.

ii. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

iii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

**Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na**
**Mratibu wa MIKOPO,**
**AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**S.L.P. 95068,**
**Dar Es Salaam.**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**Simu: ANDAN GROUP LIMITED 0684 078 494**
**BOSTON AUCTION MART 0766547732/ 0717494900/ 0786600606**

215351401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ya kudhibiti udukuzi mawasiliano kamwe haikwepeki

**HIVI** karibuni kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo waliowahi kuwa viongozi katika nafasi za juu serikali kuhusu kudukuliwa kwa mawasiliano yao.

Miongoni mwa watu ambao wamekuwa wakidai kudukuliwa kwa mawasiliano yao ni pamoja na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika serikali ya awamu ya nne, Bernard Membe.

Mwanasiasa na mwanadiplomasia huyo alikiri kuwa mawasiliano yake yalidukuliwa na watu wasiojulikana hivyo kusababisha taharuki katika jamii kwa ujumla.

Licha ya Membe, wanaharakati wa haki za binadamu wakiongozwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na Mbunge wa Ubungo (Chadema), walilizungumzia kwa kina suala hilo huku wakilaani na kutaka sheria itungwe kuwabana watu wenye tabia hizo.

Wengine waliodai mawasiliano yao kudukuliwa ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Yussuf Makamba na Katibu Mwenezi wa chama hicho, Nape Nnauye ambaye aliwahi pia kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika serikali ya sasa.

Suala hilo limesababisha baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa kulaani na kuiomba serikali kutunga sheria kwa kuwa vitendo hivyo ni kinyume cha sheria za kimataifa na mikataba mbalimbali juu ya faragha ya mtu.

Membe, akiwa mwathirika wa vitendo hivyo, alisema ni wakati mwafaka kwa serikali kutunga sheria kuwadhibiti watu wanaoendesha vitendo hivyo vinavyokinzana na haki za binadamu.

Mwanasiasa huyo alisisitiza kuwa jambo hilo ni kosa la jinai ndio maana dunia nzima inapiga vita na ni vigumu kusikia watu wanafanya udukuzi waziwazi, lakini akaishangaa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliyopewa dhamana ya kusimamia sekta ya mawasiliano ikikaa kimya.

Alishauri kuwa kuendelea kwa vitendo hivyo kunahatarisha pia maendeleo ya sekta hiyo na kampuni za simu kwa kuwa watu wanaweza kukosa imani na baadhi yao, hivyo kujikuta zikikosa wateja na kufunga biashara.


Kutokana na malalamiko hayo, TCRA kupitia idara yake ya mawasiliano kwa umma, iliruka kimanga na kusema haiwezi kuingilia suala hilo kwa kuwa ni la kijinai, hivyo vyombo vya dola kama polisi ndivyo vinavyopaswa kuchukua hatua. Pia ilisema wanaolalamika wafuate taratibu ikiwamo kwenda mahakamani kufungua kesi.

Kwa ujumla, suala hilo halipaswi kufumbiwa macho kwani kama wahusika wataachiwa wakaendelea kutekeleza uhalifu huo, kuna uwezekano madhara makubwa yakajitokeza ikiwamo siri za serikali pia kudukuliwa.

Kama wahenga wasemavyo ni heri kuzuia kuliko kutibu, ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kusikia kilio cha wadau, wakiwamo walioathirika na vitendo hivyo, kwa kutunga sheria kali itakayowabana watu wanaoendesha mambo hayo.

Ni imani serikali ya awamu ya tano ambayo siku zote imekuwa ikisikiliza vilio vya wananchi na kutetea wanyonge, itapokea mawazo yaliyotolewa na hatimaye kudhibiti uhalifu huo kwa kutunga sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mabadiliko ya sheria yachagize kudhiti ulevi kwa madereva

Na Mashaka Mgeta

**KWA** kipindi cha takribani miezi mitatu, nimeshiriki fursa ya uhamasishaji wenye lengo la kuleta mabadiliko ya fikra, sera, kanuni na sheria ili kukidhi azma ya kuifanya Tanzania iondokane na ajali za barabarani.

Mabadiliko hayo yanalenga kuchagiza kasi ya utekelezaji wa mipango mbalimbali inayofanywa na polisi wa usalama barabarani, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wadau wengine kupunguza kama si kuondoa kabisa uwapo wa ajali hizo zinazogharimu maisha na uharibifu wa mali.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limeainisha vyanzo kadhaa vya ajali za barabarani ambavyo kama vitashughulikiwa na kada tofauti, kila moja kwa nafasi yake, basi ni rahisi kuipata sehemu ya dunia kama Tanzania isiyokuwa na ajali hizo.

Kwa mujibu wa WHO inayofanya kazi na kuwa na mafungamano ya mahusiano na Tanzania, vyanzo hivyo ni pamoja na mwendokasi, kutovaa kofia ngumu upande wa pikipiki, kutofunga mikanda ya kwenye gari, ulevi, miundombinu mibovu, miongoni mwa mengine mengi.

Nikiwa katika ushiriki huo unaoratibiwa na Wakfu wa Vyombo vya Habari (TMF), nimefanikiwa kujikita zaidi katika nafasi ya ulevi kwa jinsi inavyochangia kutokea na ongezeko la ajali za barabarani.

Nimepitia maandiko kadhaa, nimezungumza na vyanzo vya habari kutoka kada tofauti na kubaini kuwa, hatari bado inazidi kulikabili taifa ikiwa suala la ulevi kama sehemu ya vyanzo vya ajali za barabarani, halitapewa kipaumbele na nguvu zaidi za kisheria katika udhibiti wake.

Mathalani, kifungu cha 44 hadi 49 ya Sheria ya Usalama Barabarani vinaeleza kuwa ukomo wa kiwango cha kilevi kinachopaswa kubainika kwa dereva ni kinachofikia 0.008, zaidi ya hapo kunakuwa na mwanya wa kutolewa adhabu kwa mhusika.

Lakini kwa upande wake, WHO imeweka kiwango kwa ajili ya udhibiti wa ulevi kwa madereva kuwa ni 0.005. kiwango hiki kinatumika pia kwenye nchi kadhaa duniani.

Pasipoweka taarifa za kitaalamu kuhusu ujazo wa kiwango hicho, tafsiri rahisi inayoweza kueleweka kwa haraka ni kwamba Tanzania inatumia kiwango kikubwa cha utambuzi wa kilevi kwa madereva kuliko ilivyo kwa WHO.

Nilipozungumza na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilimu, akasema miongoni mwa mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani yanayopendekezwa sasa ni kuhusu kupunguza kiwango hicho angalau kufikia 0.005 kama ilivyo kwa WHO.

Lakini kwa mtazamo wake binafsi, Kamanda Musilimu akasema ingefaa sana kiwango hicho kuwa 0.00, lakini kwa vile kuna sababu za kibaiolojia kuhusu mwili wa binadamu kuwa na ming'emenyo inayotengeneza kilevi mwilini, basi angalau 0.005 itafaa kwa nchi.

Inapofikia hatua ya Kamanda wa kikosi cha usalama barabarani kufikiria hivyo, ni ishara kwamba nafasi ya kilevi katika kusababisha ajali nchini bado ipo kwa kiwango kisichofaa.

Lakini hoja kama hiyo ipo pia kwa mukhtadha wa athari za kiuchumi, ambapo Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa na Magonjwa ya Ajali wa Taasisi ya Mifupa (MOI), Dk. Kennedy Nchimbi, anasema matibabu ya mifupa kwa majeruhi wa ajali zikiwamo zilizosababishwa na ulevi, yanagharimu fedha nyingi zinazoweza kuelekezwa kwa huduma nyingine za kijamii.

Dk. Nchimbi anatoa mfano kuwa, chuma kimoja kinachowekwa kwenye eneo la mfupa unaovunjika hasa kwenye ajali, kinagharimu Sh. milioni mbili wakati matibabu yake yanagharimu Shilingi laki tatu.

Hata hivyo, Dk. Nchimbi anasema gharama za chuma hazifahamiki kwa watu wengi kwamba zinatolewa kwa msaada wa watu wa Marekani, ndio maana kiasi cha Sh. laki tatu pekee kinatozwa kwa majeruhi hao.

Ni kwa mifano hiyo michache inatoa taswira kwamba umefika wakati wa kila mwenye dhamana ya udhibiti wa ajali za barabarani, kusimama, kupaza sauti na kuhakikisha anachangia kwa namna yoyote, kutokemeza ajali na kuifanya Tanzania mahali salama kwa usafiri na usafirishaji.

MJADALA

# Kanda ya ziwa changamkieni elimu toka Brela



Ofisa Habari na Mawasiliano wa BRELA, Robertha Makinda (kushoto), akitoa ufafanuzi kwa baadhi ya wageni waliotembelea banda la Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA) katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa hivi karibuni katika viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

MKOA wa Simiyu ni mwenyeji wa maonyesho ya wakulima, wavuvi na wafugaji (Nanenane) kitaifa kwa mwaka huu wa 2019, ambayo yatahusisha shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu.

Elimu hiyo itatolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) ikilenga kuwawezesha wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kujua jinsi ya kusajili kampuni, kupata leseni na namna ya kupata soko zuri la bidhaa zao.

Wataelimishwa pia jinsi ya kurasimisha shughuli zao ambazo mara nyingi zimekuwa kwa matumizi ya nyumbani, na inawezekana baada ya elimu hiyo watabadilika na kusajili shughuli zao ili ziwaletee manufaa zaidi.

Hivyo ndivyo anavyosema, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Emmanuel Kakwezi na kufafanua kuwa taasisi hiyo ya Serikali imejipanga vizuri kutoa elimu kuhusu shughuli zinazofanywa na wakala.

Maonyesho hayo yalitarajiwa kuzinduliwa jana, hivyo hii ni nafasi ya pekee kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa kupata elimu hiyo kwa ajili ya kuboresha shughuli zao ili ziweze kuwanufaisha.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan atayazindua rasmi Agosti Mosi, huku waonyeshaji zaidi ya 300 wakiwa tayari wamejiandikisha kushiriki katika maonyesho hayo, Brela ikiwa miongoni mwao.

Kakwezi anasema taasisi yake hiyo ya umma imejiandikisha kushiriki ili kutoa elimu hiyo kwa Watanzania na hasa wa mikoa ya kanda ya ziwa wanaojishughulisha na biashara mbalimbali.

Anasema Brela itakuwa na banda la kutoa elimu pia huduma ya usajili majina ya biashara, kutoa leseni, kusajili alama za biashara, kutoa hati na leseni za viwanda.

Mengine yanayotarajiwa kufanyika katika maonyesho hayo ni washiriki kuonyesha teknolojia, huduma na bidhaa zao.

Hivyo ni vyema wadau kuchangamkia fursa hiyo ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Kimsingi wafanyabiashara, wakulima, wavuvi na wafugaji hii ni nafasi muhimu kwao kwa ajili ya kuwezeshwa kwa kuelekezwa taratibu mbalimbali zikiwamo za jinsi ya kusajili kampuni na namna ya kupata masoko.

Ujasiriamali unaweza kuwa suluhisho la ajira nchini, lakini inawezekana baadhi ya Watanzania hawana elimu ya ujasiriamali, hivyo zinapotokea fursa za kuelimishwa bure kama hizo za Brela, ni muhimu kuzichangamkia.

Kwa mujibu wa Kakwezi, Brela ina mfumo wa kuuza bidhaa nje ya nchi na wanatoa elimu hiyo ili kuwafanya Watanzania wajue namna gani wanavyoweza kuuza bidhaa zao nje ya mipaka ya nchi.

Anasema kuwapo kwa Brela katika maonyesho hayo ni habari njema kwa wakazi wa mikoa ya kanda ya ziwa, hivyo wanatakiwa kufika ili wapate elimu itakayowanufaisha katika shughuli zao.

Kwamba banda la Brela litakuwa limesheheni wataalamu, ambao watasaidia kutoa maelezo yote yanayohusu huduma zinazotolewa na Brela na kupata elimu itakayowasaidia kurasimisha shughuli zao. Sasa ni mara ya pili Simiyu kuwa mwenyeji wa maonyesho hayo, kwani mwaka jana ofisi ya mkoa huo ikishirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) iliandaa maonyesho hayo kitaifa.

Kilichosistizwa na mkuu wa mkoa huo, Anthony Mtaka na ambacho pia safari hii amekirudia ni kufanya maonyesho yawezeshe Watanzania kupata fursa ya kuona teknolojia mbalimbali kwenye eneo la kilimo, mifugo na uvuvi.

Brela inasema, wafanyabiashara wanaposajili biashara zao wanatambuliwa kirahisi na kuwa na uwezekano mkubwa wa kufanya biashara kwa ushindani wa kitaifa na kimataifa.

Hatua hiyo pia inaweza kwenda sambamba na kile ambacho Rais John Magufuli amekuwa akisisitiza cha kuwa na Tanzania ya viwanda, hivyo kuchangamkia elimu kutoka Brela ni muhimu.

Ukiangalia kwa umakini utagundua kwamba Brela, inataka kuhakikisha wadau wote kuanzia wakulima, wavuvi, wafanyabiashara na wengine wengi wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali, wanapata elimu.

Ikumbukwe kuwa elimu kwa maana pana ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia au uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi, ingawa kwenye dhana ya kiufundi, elimu ni njia inayotumiwa kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

## TAARIFA KWA UMMA

### 1.0 Utangulizi

Katika siku za hivi karibuni baadhi ya watu wamekuwa wakitoa taarifa zisizo sahihi kupitia njia na vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Na. 14 ya Mwaka 2017 na namna Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) litakavyofanya kazi.

Taarifa hizo zinapotosha umma kuwa utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli utasababisha madhara kama vile urasimu katika utoaji huduma, watumiaji wa bandari kupungua, makampuni ya forodha kufungwa, msongamano wa shehena bandarini na kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa watoa huduma kwa kuwa Mdhibiti anashiriki katika utoaji wa huduma .

### 2.0 Sheria ya Uwakala wa Meli Na. 14 ya Mwaka 2017

Tunapenda umma ufahamu kwamba Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Na. 14 ya Mwaka 2017, ambayo imeanzisha Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), ina lengo la kuhakikisha kuwa nchi inanufaika ipasavyo kutokana na sekta ya usafiri na usafirishaji majini. Sheria imeainisha majukumu na kazi za TASAC ni usimamizi wa usalama wa vyombo majini na ulinzi wa mazingira kutokana na shughuli za usafiri majini, udhibiti wa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji nchini, udhibiti wa nyaraka za usafirishaji shehena kwa njia ya maji, kazi za uwakala wa meli, kazi za uhakiki wa shehena na uwakala wa forodha.

### 3.0 Matokeo ya Utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli

Kinyume na vile inavyopotoshwa, utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli utaleta matokeo yafuatayo:

(i) Kuchochea utoaji wa huduma bora miongoni mwa watoa huduma na kuvutia watumiaji wa bandari zetu kwa kuimarisha udhibiti wa shughuli za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji nchini. Hatua hii itaongeza watumiaji wa bandari zetu kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuwa huduma zitatolewa kwa viwango vinavyostahili. Aidha, watumiaji wa huduma wanayo fursa ya kuwasilisha malalamiko na kupatiwa ufumbuzi iwapo hawakutendewa haki na watoa huduma wanaodhibitiwa na TASAC.

(ii) Kuongezeka kwa biashara ya usafirishaji kwa njia ya maji kutokana na kuwepo kwa uwazi, njia sahihi za mawasiliano na uwazi ili kuondoa urasimu katika shughuli za uwakala wa meli, uhakiki wa shehena zinazosafirishwa kupitia bandari zetu na uwakala wa forodha. Kuongezeka kwa biashara ya usafirishaji kunatoa fursa kwa makampuni mengi zaidi ya forodha kushiriki katika utoaji wa huduma. Ni kwa sababu hiyo, mwaka 2019 idadi ya makampuni ya wakala wa forodha imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 20 ikilinganishwa na mwaka 2018.

(iii) Kuimarisha ulinzi, usalama, mazingira, afya za watanzania na mapato ya taifa kwa kuruhusu TASAC kushiriki katika utoaji huduma zenye maslahi mapana kwa taifa ili kuzuia udanganyifu, uwasilishaji wa nyaraka na taarifa zisizo sahihi kwa mamlaka mbalimbali nchini. Sheria imeainisha bidhaa na maeneo ya huduma ambazo zitafanywa na TASAC pekee (exclusive mandate) kutokana na kuwa na maslahi mapana kwa umma ili kuepuka dhana ya Mdhibiti kuwa mshindani katika soko. Bidhaa kama madini, makinikia, na mitambo yake, silaha, nyara za Serikali n.k. yanahusika. Maeneo mengine ya biashara ambayo hayakuainishwa kuwa ya TASAC pekee yanaendelea kufanywa na sekta binafsi.

(iv) Kuchochea ushindani miongoni mwa watoa huduma katika sekta na kuhakikisha utendaji kazi wenye tija kwa wadau wote, hivyo kuongeza ufanisi katika shughuli za bandari na uondoshaji wa shehena. Hatua hii itaondoa changamoto ya msongamo wa shehena na meli katika Bandari zetu kwa kuwa watumiaji wanayo haki ya kupewa huduma bora kwa saa 24 kwa siku na siku 7 kwa wiki.

(v) Kuongeza ushiriki wa wananchi kwa kuwawezesha kuwa wabia wakubwa katika biashara muhimu katika mnyororo wa thamani (value chain) katika uchumi wa bahari (Blue Economy).Kwa sasa, wawekezaji kutoka nje ya nchi wanapaswa kushirikisha Watanzania katika umiliki wa makampuni yote yatoayo huduma zinazodhibitiwa.

(vi) Kuimarisha udhibiti kwa kuwepo kwa Sheria mahsusi kwa ajili ya udhibiti wa sekta ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji nchini tofauti na hapo awali ambapo sheria moja ya udhibiti ilitumika kusimamia sekta mbili, yaani sekta ya usafiri majini na sekta ya usafiri nchi kavu.

(vii) Kuimarisha usalama wa huduma za usafiri kwa njia ya maji nchini ambapo miongozo mbalimbali inayotolewa na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization-IMO) itazingatiwa hivyo kuwa na huduma salama na rafiki kwa mazingira kutokana na kuimarika kwa udhibiti.

### 4.0 Hitimisho

Kwa ujumla, utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli Na. 14 ya Mwaka 2017 utaongeza ufanisi na kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji. Aidha, utawezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi kuhusu shehena zinazosafirishwa kwa njia ya maji na hivyo kuliwezesha taifa kuchukua hatua sahihi kwa kuzingatia taarifa sahihi. Utekelezaji wa Sheria hii, umewapa Watanzania wengi zaidi fursa ya kushiriki katika uchumi utokanao na urithi wa bahari na maji yaliyopo Tanzania na shughuli za sekta ya usafiri kwa njia ya maji nchini.

**IMETOLEWA NA: MKURUGENZI MKUU**

**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA -TASAC**

215351202

# RC mbogo madiwani kumkataa mkurugenzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewaagiza madiwani wa Manispaa ya Shinyanga, kutengua uamuzi wa kumkataa mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Geoffrey Mwangulumbi, kwa madai kwamba hawakufuata kanuni na taratibu.

Amesema walichokifanya madiwani hao ni ukiukaji wa kanuni na taratibu, kwa kuwa walipaswa kuitisha kikao maalumu na kumpelekea malalamiko ili ayafanyie kazi, lakini alishangaa kusikia tu kikao cha baraza kimevunjika madiwani wakimkataa mkurugenzi kutokuwa na imani naye.

Telack alibainisha hayo jana kwenye kikao cha kawaida cha baraza la madiwani la Manispaa ya Shinyanga, ambao waliamua kuendelea na baraza hilo baada ya kutengua uamuzi wao wa juzi wa kumkataa Mwangulumbi.

Alisema baraza hilo haliwezi kuendelea kuwapo endapo hawatatengua uamuzi wao wa kumkataa mkurugenzi ikiwa kanuni na taratibu zilikosewa kufuatwa.

Madiwani hao walitengua uamuzi wao kisha baraza kuendelea na kujadili ajenda mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya manispaa hiyo.

"Taarifa hizi za kumkataa mkurungenzi nilizipata toka majuzi nikaona ngoja niwapime upeo wenu madiwani kama mtafuata kanuni na taratibu. Nilishangaa tu mmechukua uamuzi mkavunja kikao cha baraza bila ya kufuata taratibu, hivyo naagiza uamuzi wenu muutengue kwanza ndipo mwendelee na kikao. Tofauti na hapo, baraza lenu ni batili,"alisema Telack.

"Ninachotaka kusema madiwani tuachane na malumbano yasiyo na maana kwa kuvunja tu vikao bila kufuata taratibu. Pale penye upungufu tuwasiliane ili twende pamoja. Nafahamu changamoto za manispaa hii. Ni kweli yale ambayo mnalalamikia juu ya maazimio yenu kutotekelezwa mko sahihi kabisa," aliongeza.

Mkuu huyo wa mkoa pia alisema tatizo ambalo linasababisha migogoro hiyo kuwapo ni kutoelewana kati ya watumishi wa halmashauri na mkurugenzi wao kwa sababu kila mtu ni mbabe, hivyo kusababisha miradi mingi kuwa na usimamizi mbovu na kutotekelezeka ndiyo maana maazimio mengi hayafanyiwi kazi.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Masovela, aliwataka watumishi wa manispaa hiyo, madiwani na mkurugenzi, kuzungumza lugha moja ili kuondoa makandokando yaliyopo na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, John Kisandu, alisema wametengua uamuzi wao wa kumkataa mkurugenzi huyo na kukiri kwamba hawakufuata kanuni na taratibu, hivyo wataendelea kufanya naye kazi na kumtaka maazimio yao awe anayafanyia kazi.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Msimamizi Mkuu wa Kituo Jumuishi cha kutunza watoto na vijana waathirika wa usafirishaji, Regina Mandia (wa pili kushoto), wakati wa maadhimisho ya siku ya kupinga biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mussa Zungu na Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Hamoud Jumaa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wanafunzi 190 kuonyesha ubunifu

INATOKA UK. 4

watazawadiwa fedha taslim na medali, huku wanasayansi chipukizi wanne wakipata udhamini wa masomo ya chuo kikuu unaotolewa na Shirika la Karimjee Jivanjee Foundation ili kuwawezesha kusoma masomo ya sayansi na teknolojia ngazi ya vyuo vikuu.

Alisema washindi wa jumla wa maonyesho hayo pia wataiwakilisha Tanzania kwenye maonyesho ya kimataifa ya Eskom Expo Young Scientists yatakayofanyika Oktoba mwaka huu jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

Mwazilishi Mwenza wa YST, DK.Gosbert Kamugisha, alisema kuna haja sasa kuona namna ya kufanya mabadiliko kwa masomo ya sayansi ili yawe ya vitendo.

Meneja wa Taasisi ya Karimjee Jivanjee Foundation ambao ni wadhamini wa maonyesho hayo ya wanasayansi chipukizi, Devota Rubama, alisema tayari wameshatoa udhamini kwa wanafunzi 27 walioshinda tuzo hizo.

Alisema lengo la kudhamini wanafunzi hao ni kuunga mkono jitihada za YST pamoja na serikali zinazolenga kukuza ujuzi na vipaji vya vijana wadogo kwa kuzingatia uchumi wa nchi kwa njia ya utafiti wa kisayansi na maendeleo ya teknolojia nchini.

## Mamia wamzika Agnes Kabigi

INATOKA UK. 5

marafiki, Jane Mihanji, alisema Kabigi alizaliwa Julai 13, 1967 mkoani Mbeya.

Alisem Kabigi alianza elimu ya msingi katika Shule ya Msingi kifungiro mwaka 1975 hadi 1981, alijiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kibosho mwaka 1982 hadi mwaka 1985 na mwaka 1986 hadi 1988 alihitimu kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Zanaki

Mwaka 1989 na mwaka 1991 alisomea stashahada ya habari na baada ya hapo alifanya kazi kwa muda mfupi na kujiunga na Chuo cha Diplomasia na kupata Stashahada ya Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia mwaka 1994.

Mwaka 2008 hadi 2010, alisoma na kupata Shahada ya Uzamili (Masters) ya masuala ya Mawasiliano ya Umma katika chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine.

Baadhi ya sehemu alikofanya kazi ni pamoja na katika magazeti ya Uhuru na Mzalendo mwaka 1991 hadi 1994 na mwaka 1994 hadi mwaka 2003 katika na kampuni ya IPP Media katika magazeti ya Nipashe akiwa mwandishi mwandamizi.

Juni 2018, aliajiriwa na shirika la Ariel Glaser Pediatric AIDS Healthcare Initiative (AGPAHI) akiwa Meneja Mawasiliano na Ushawishi alikofanya kazi mpaka kufariki dunia.

Mume wa marehemu, Julius Mwanjila (JB), alisema kwa mara ya kwanza kukutana na mkewe ilikuwa mwaka 2000 na hapo ndipo walianza urafiki hadi kufunga ndoa na kwamba alimpenda mkewe kuliko kitu chochote na alikuwa mahiri sana kumwongoza katika kila jambo hususani alipoonekana kutetereka.

"Watu wanasema Mungu amempenda zaidi mke wangu, lakini mimi nampenda zaidi. Ni ngumu sana kuhimili hali hii, naomba Mungu anisaidie," alisema huku akilia.

Baadhi ya taasisi ambazo zilitoa salamu za rambirambi ni pamoja na Jukwaa la Fursa, Zanaki, Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) na AGPAHI.

Mkurugenzi wa AGPAHI, Dk. Sekela Mwakyusa, aliiambia Nipashe kuwa Kabigi alifariki dunia akiwa amekaa kwenye kiti ndani ya gari la ofisi.

Alisema Kabigi na wenzake walikuwa Shinyanga kwa shughuli za kikazi ikiwa ni pamoja na kutembelea sehemu mbalimbali na wadau wa shirika hilo linalojishughulisha na masuala ya kudhibiti virusi vya ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Alisema Kabigi aliwasili Kahama Alhamisi ya wiki iliyopita na kwamba alikuwa akijisikia vibaya, ingawa hali haikuwa mbaya, hivyo hakwenda hospitali.

Alisema pamoja na hali hiyo aliendelea na kazi hadi Ijumaa asubuhi hakuwa na tatizo na aliondoka na wenzake kwenda kwenye kazi wakipitia hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya kuchukua nyaraka walizokuwa wanazihitaji.

# Mkuchika achangisha mil. 26/- ujenzi kanisa

**Na Steven William,** MUHEZA

ZAIDI ya Sh. milioni 26 zimepatikana katika hafla ya kuchangia ujenzi wa kanisa jipya la Anglikana la Mtakatifu Yakobo lililoko katika kijiji cha Ubembe, Muheza mkoani Tanga.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika, aliwaongoza waumini katika kuchangia ujenzi huo kwenye hafla iliyofanyika Jumapili iliyopita.

Mkuchika alitangaza hadharani mbele ya waumini kwamba Sh. milioni 26 zilipatikana kutokana na michango ya watu mbalimbali kwa lengo la ujenzi wa nyumba ya Mungu.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa kanisa hilo jipya, Katibu wa Ujenzi, Frank Ngulizi, alisema jumla ya Sh. milioni 126 zinahitajika ili kukamilisha kazi hiyo.

Ngulizi alisema katika harambee hiyo zilikuwa zinahitajika Sh. milioni 33 kwa ajilli ya kupaua na kwamba ujenzi wake unakwenda vizuri chini ya usimamizi wa Mchungaji Charles Mhanusi.

Alisema ujenzi huo wa kanisa ambalo litakuwa na uwezo wa kuingiza waumini 400, mpaka sasa ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 20 kwa kufanyika kazi ya kuzungusha boma lakini ujenzi unaendelea.

Kwa upande wa Waziri Mkuchika alisema lazima waumini hao kujitolea fedha katika kujenga nyumba ya Mungu kwa kuwa ni faida kwao katika kupata pepo nzuri watakapokufa.

Alisema kutoa ni moyo si utajiri kwa maana hiyo lazima wananchi na waumini wachangie katika ujenzi wa kanisa hilo ili likamilika haraka.

Naye Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, alisema katika suala la Mungu, lazima watu wachangie fungu lao katika ujenzi wa kanisa na kwamba na yeye si mgeni na amechangia sana kanisa hilo.

Alisema kuhusu ujenzi wa kanisa hilo, wataendelea kuchangia na ujenzi kwa kuwa ni nyumba za Mungu ambaye amewapa pumzi binadamu hapa duniani, hivyo ni lazima aheshimiwe.

**katika harambee hiyo zilikuwa zinahitajika Sh. milioni 33 kwa ajili ya kupaua na kwamba ujenzi wake unakwenda vizuri chini ya usimamizi wa Mchungaji Charles Mhanusi.**

# Waziri akunwa maandalizi sherehe Nanenane kitaifa

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, juzi aliwasili mkoani Simiyu kwa ajili ya kujionea maandalizi ya Maadhimisho ya 26 ya Sikukuu ya Wakulima, maarufu (Nanenane), ambayo kitaifa yatafanyika mkoani hapa.

Maonyesho hayo yanalengo la kuwatambua na kuwaenzi wadau wa sekta ya kilimo ambao ni wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaushirika, wasindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili kwa mchango wanaoutoa katika kuendeleza uchumi wa nchi.

Mwaka huu, maonyesho hayo yanafanyika mjini hapa katika Viwanja vya Maonyesho ya Kilimo Nyakabindi. Baada ya kuwasili, Hasunga aliupongeza uongozi wa mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara kwa kufanikisha kuingiza uwanjani huduma za msingi za maji na umeme.

Alisema jukumu hilo kwa serikali na wadau wa sekta binafsi ni kuendeleza viwanja hivyo vya Nyakabindi kwa kujenga mabanda ya maonyesho ya kudumu na kuboresha huduma muhimu za kijamii ili kuwe na maonyesho endelevu yenye sura ya kitaifa na kimataifa.

**Kwa wafanyabiashara itakuwa ni fursa nzuri ya kutangaza bidhaa zao hususani pembejeo na zana mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili.**

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuongeza na kuboresha viwanja vya maonyesho katika kanda mbalimbali nchini. Alisema kwa sasa kuna viwanja vinane vya maonyesho ya kilimo ambavyo ni Themi (Arusha) Kanda ya Kaskazini inayohusisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara; Mwalimu Nyerere (Morogoro) Kanda ya Mashariki ambayo mikoa yake ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga.

Viwanja vingine ni John Mwakangale (Mbeya) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Njombe, Katavi, Songwe na Rukwa; Nzuguni (Dodoma) katika Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma na Singida; na Nyakabindi (Bariadi) Kanda ya Ziwa Mashariki yenye mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara.

Pia vipo viwanja vya Nyamuhongolo (Mwanza) Kanda ya Ziwa Magharibi yenye mikoa ya Mwanza, Kagera na Geita; Ngongo (Lindi) Kanda ya Kusini inayojumuisha mikoa ya Mtwara na Lindi na Fatma Mwasa (Tabora) Kanda ya Magharibi yenye mikoa ya Tabora na Kigoma.

Waziri Hasunga alisema wakati wa sherehe hizo, wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaushirika na wadau wengine katika sekta za kilimo, watapata fursa nzuri zaidi ya kuona na kujifunza mbinu na teknolojia sahihi za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na bidhaa nyinginezo.

Pia alisema kwa wafanyabiashara itakuwa ni fursa nzuri ya kutangaza bidhaa zao hususani pembejeo na zana mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili.

Hasunga alisema kaulimbiu ya maonyesho hayo kwa mwaka huu ni "Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Ukuaji wa Uchumi wa Nchi".

Alisema kaulimbiu hiyo imechaguliwa baada ya kutafakari kwa undani uchumi wa viwanda unavyoweza kuchangia katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, pato la taifa na sambamba na kupambana na umaskini.



Mratibu wa mradi wa Mwanamke Amka kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Huheso Foundation, Wilberth Wanga, akizungumza na wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, mkoa wa Shinyanga jana, wakati wa uzinduzi wa mradi huo, ambao utahudumia kata tano zilizopo halmashauri hiyo. **PICHA: SHABAN NJIA**

# PM amtaka DED kusimamia ujenzi hospitali

**Na Said Hamdani,** RUANGWA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ruangwa mkoani Lindi, Andrew Chezue, kusimamia kwa karibu ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo ili ukamilike mapema.

Majaliwa alitoa agizo hilo juzi alipotembelea kukagua na kujionea maendeleo ya ujenzi huo. Ujenzi wa hospitali hiyo unatokana na Sh. bilioni 1.5 zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wake, huku halmashauri ikichangia eneo la ujenzi lenye ukubwa wa ekari 100.

Baada ya kukagua na kujionea ujenzi unavyoendelea, Waziri Mkuu alisema kuna haja ya kusimamia kazi hiyo kwa karibu zaidi ili kuhakikisha utekelezaji wake unakamilika mapema.

Aidha, Majaliwa aliwataka mafundi ambao utekelezaji wa kazi zao wako nyuma kuongeza kasi ikiwamo kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha zinakamilika mapema kama ilivyokusudiwa.

Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa, alisema muda uliowekwa na serikali kukamilisha miradi hiyo umekwisha, huku akiushauri uongozi wa halmashauri kupeleka maombi wa kuongezewa muda ili kukamilisha ujenzi huo.

"Muda uliopo ni mdogo hivyo kuna umuhimu kwa halmashauri mkapeleka serikalini ombi la kuongezewa muda kukamilisha kazi hii," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza hospitali zote za wilaya na vituo vya afya vinavyojengwa nchini, hadi Julai 30, mwaka huu (jana) viwe vimekamilika ujenzi wake.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Dk. Mahela Godfrey, alimwelezea Waziri Mkuu Mjaliwa kuwa kazi ya ujenzi wa hospitali hiyo, ulianza Januari 12, mwaka huu na unafanyika kwa kuzingatia ramani maalumu iliyotolewa na Tamisemi.

Alisema hadi sasa majengo matano yamepauliwa na yanaendelea na hatua ya umaliziaji, wakati mawili yako hatua ya upauaji na umaliziaji na kwamba fedha zilizokwishatumika ni Sh. 1,361,929,666.38 kati ya Sh. bilioni 1.5 zilizotolewa na Serikali Kuu.

# Wataka mgogoro umalizwe kudumisha amani, utulivu

**Na Rose Jacob,** SERENGETI

SERIKALI imeombwa kuutafutia ufumbuzi wa haraka mgogoro wa mipaka ya vijiji vya Merenga na Machochwe katika Wilaya ya Serengeti mkoani Mara uliodumu kwa zaidi ya miaka 30.

Imeelezwa kuwa kuendelea kwa mgogoro huo kunaweza kuchochea uvunjifu wa amani, yakiwamo mapigano ya koo za kabila la Walenchoka na Wakira kutokana na kugombea ardhi.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wakazi wa kijiji cha Merenga kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na uongozi wa serikali ya kijiji hicho ili kupata mustakabali wa mgogoro wa mipaka baina ya vijiji hivyo.

Baadhi ya kinamama wa kitongoji vya Mabatini, Merenga na sehemu ya Nyamihuru wanaoishi katika eneo lenye mgogoro wa mipaka kati ya vijiji vya Merenga na Machochwe, walidai kuhofia usalama wa maisha yao.

**Tunaiomba serikali iliangalie suala hili maana kijiji chetu kina hati mbili za usajili maana kilisajiliwa Septemba 15, 1993 kwa hati ya kuandikishwa kijiji namba 406.**

"Tunaiomba serikali itusaidie maana tunashindwa kufanya shughuli zozote za maendeleo na watu tunaishi kwa kujifichaficha kutokana na mgogoro huu wa mpaka. Kinamama wameshindwa hata kuchota maji wakihofia usalama wao maana wakienda hata kusaga katika kijiji cha Machochwe wamekuwa wakinyanyaswa kwa kurudishwa nyuma ya foleni hadi usiku unaingia kisha wanafukuzwa wanaondoka bila hata kusaga," walisema Marco Nyabili na Mary Magige.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Merenga, Mathias Kipuko, alisema taswira hasi ya mgogoro huo inatajwa kuchangiwa zaidi na baadhi ya maofisa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwa kutoa hati mbili za usajili kwenye kijiji kimoja na kuhamisha holela mipaka ya vijiji hivyo.

"Tunaiomba serikali iliangalie suala hili maana kijiji chetu kina hati mbili za usajili maana kilisajiliwa Septemba 15, 1993 kwa hati ya kuandikishwa kijiji namba 406, lakini cha kushangaza Septemba 15, 2005 ikatoka hati nyingine namba 342 jambo ambalo limekuwa likileta migogoro ambayo haina tija," alisema Kipuko.

Aidha, sakata la mgogoro huo wa mipaka ya vijiji limetua kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, ambaye amemwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Simiyu, Tumaini Gwakisa, kufika katika vijiji hivyo ili kutatua mgogoro huo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Merenga, Peter Chacha, aliwataka zaidi ya wakazi 6,000 wa kijiji hicho kuendelea na shughuli zao za maendeleo, ikiwamo ufugaji, kilimo na uchimbaji mdogo wa dhahabu wakati serikali ikiendelea kushughulikia mgogoro huo ulioanza tangu mwaka 1987.



Katapila likikusanya kifusi baada ya kubomoa baadhi ya vibanda vya wafanyabiashara katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi, ili kupisha upanuzi unaoendelea wa Barabara ya Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Askofu aonya wanaobeza wasomi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

ASKOFU wa Kanisa la Moravian Jimbo la Rukwa, Conrad Nguvumali, amekemea tabia ya baadhi ya wananchi ya kuwabeza wasomi ambao hawajapata ajira na kudai kuwa kitendo hicho kimekuwa kikiwaathiri kisaikolojia na kujiona kuwa hawana maana.

Kauli hiyo aliitoa juzi katika mahafali ya Chuo cha Theolojia Mlimani kilichoko mjini Sumbawanga. Katika mahafali hayo, wahitimu 42 watunukiwa vyeti baada ya kumaliza kozi mbalimbali zikiwamo za masomo ya kiroho na ujasiriamali.

Alisema kutokana na ugumu wa upatikanaji wa ajira, baadhi ya watu wamekuwa wakiwabeza wasomi na kuona kuwa walikwenda vyuoni kupoteza muda hali inayosababisha kuwaathiri kisaikolojia.

Askofu Nguvumali alisema dhana iliyojengeka katika jamii ni changamoto kubwa kwa kuwa wananchi wanaamini kuwa kila mtu anayekwenda chuoni lazima apate ajira kumbe inawezekana akasoma na kisha kujiajiri.

"Kuna mtindo wa kuwabeza wasomi waliohitimu vyuo na bado hawajapata ajira, sambamba na kufanikiwa maisha kuwa walikwenda vyuoni kupoteza muda. Dhana hii ni hatari na lazima kuikemea kwani inaweza kusababisha vijana wasione umuhimu wa elimu na matokeo yake tukakumbatia ujinga," alisema.

Alisema kwenda vyuoni kupata elimu ni kumpa mtu fursa ya kukabiliana na mazingira, hivyo ni vyema wahitimu wa vyuo wawe wanajikita katika mambo mengine ikiwamo ujasiriamali na kwamba watapata wigo mkubwa wa kujiajiri na kuajiri hata hao wanaowabeza.

Nguvumali alisema kuna tofauti kubwa ya mjasiriamali ambaye amesoma chuo na yule ambaye hana elimu, japo asiyekuwa na elimu anaweza kuwa na mtaji lakini atakuwa akipiga hatua polepole tofauti na msomi.

Mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya ujasiriamali katika chuo hicho, Peter Mayanja, alisema elimu waliyopata chuoni hapo kwa muda wa mwaka mmoja imewafungua na kujiona kuwa wanaweza kuzikabili changamoto zilizokuwa zikiwasumbua awali.

Alitoa wito kwa vijana wengine wa mikoa ya Rukwa na Katavi kujiendeleza kielimu ili kushindana katika ulimwengu huu wa utandawazi kwa kuwa bila elimu ni ngumu kufanikiwa hivi sasa.

# Ndugu wadaiwa chanzo cha matukio ya ukatili

**Na Yasmine Protace**

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia kwa watoto yanafanywa na baadhi ya wana ndugu, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Deodatha Simeon ambaye ni Ofisa wa Dawati la Jinsia kutoka Kituo cha Polisi cha Magomeni, Dar es Salaam, katika mkutano ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kuwashirikisha viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali.

Katika mkutano huo wa siku moja mada ilikuwa nafasi ya viongozi wa dini katika kupinga ukatili wa kingono.

Deodatha alisema katika matukio yanayoripotiwa, inaonyesha kuwa watoto wanatendewa vitendo vibaya na baadhi ya wanandugu.

"Baadhi ya wazazi wamekuwa busy (wana mambo mengi), masuala ya watoto hawayafuatilii na hali hiyo imekuwa ikichangia hata baadhi ya wanandugu kuwafanyia ukatili watoto," alisema.

Aliongeza kuwa wazazi wanapaswa kujifunza kuwaosha watoto wa kike kwa kuwakagua sehemu mbalimbali na kwamba hali hiyo itasaidia kuujua mwili wa mtoto uko katika hali gani.

Pia alitaka elimu kwa mtoto itolewe kuanzia miaka miwili na hali hiyo itamjenga na kumsaidia kusema chochote anachofanyiwa.

Alisema katika kupambana na matukio hayo, polisi imejipanga vizuri na inatoa huduma ya mkono.

Mkurugenzi wa Idara ya Haki, Amani na Uadilifu wa Uumbaji wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Camillus Kasala, alisema mwaka 2017 kanisa liliandaa sera na mwongozo dhidi ya ulinzi wa mtoto katika kupinga ukatili.

Alisema kwa sasa wanasimamia suala hilo kwa kupitia vyama vya kitume ambapo kanisa hilo limegawanyika katika majimbo 34.

Mwenyekiti wa Wanawake katika Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), Shamim Khan, alisema wamekuwa wakifanya matembezi na kutumia maigizo ambayo yanalenga kupinga ukatili kwa watoto na wanawake.

**Baadhi ya wazazi wamekuwa busy (wana mambo mengi), masuala ya watoto hawayafuatilii na hali hiyo imekuwa ikichangia hata baadhi ya wanandugu kuwafanyia ukatili watoto.**

# Muro amtaka DMO ziara za kushtukiza

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amemwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru wilayani humo, Dk. Maneno Focus, kufanya ziara za kushtukiza katika hospitali zilizoko wilayani humo, ili kubaini wauguzi wanaolala na wanaotegea zamu za usiku na kuwachukulia hatua.

Pia amemtaka mganga huyo kwa kushirikiana na Katibu wa Afya kuwapatia semina wauguzi katika hospitali zilizoko wilayani humo, kutumia lugha ya unyenyekevu kwa wagonjwa na kuwapatia faraja kama saikolojia ya utabibu inavyotaka.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya kuzindua kampeni maalum ya kitaifa ya kuzuia vifo vya mama na mtoto inayojulikana kama 'Jiongeze Tuwavushe Salama', Muro alisema tangu ameteuliwa katika nafasi hiyo ameshafanya ziara nyingi kwenye hospitali nyakati za usiku.

"Kuna siku nimetembelea pale hospitali ya Tengeru usiku nikajifanya ni mgonjwa nikakuta madaktari wamelala, mlinzi akaniambia nikakae eneo fulani nitatibiwa asubuhi, ndiyo nikampigia simu daktari mmoja ambaye alikuja na yeye akajionea mwenyewe," alisema.

Alisema ziara za mara kwa mara za kushtukiza zitawafanya wauguzi kuwa makini na kazi yao na watawahudumia wagonjwa kwa muda wote wa saa 24 kama inavyotakiwa na walivyoelekezwa.

Aidha, Muro alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru, kupeleka wauguzi katika zahanati mbili zilizoko katika vijiji vya Songoro na Maruvano, baada ya ukarabati na ujenzi wa majengo ya afya katika vijiji hivyo kukamilika.

Dk. Focus alisema ofisi yake imejipanga kuwahudumia vyema wananchi wa Meru na kwamba wafanyakazi wazembe watadhibitiwa katika uongozi wake. Alisema chini ya uongozi wake, wamejitahidi kuboresha huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Meru, kwa kuongeza vifaa tiba lakini pia vituo vya afya na zahanati zimeendelea kujengwa kwa kasi, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

"Katika hospitali, zahanati na vituo vya afya tumeboresha huduma zetu kwa hali ya juu na vifaa hususani vya mama na mtoto vinapatikana kwa zaidi ya asilimia 98. Tunataka mama akifika kujifungua kusitokee kabisa kifo cha mtoto au mama," alisema.

# Waziri Kalemani aagiza mkandarasi kuajiri vijana

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameiagiza Kampuni ya Nipo Group kutoa ajira kwa vijana 50 wa Kijiji cha Khusumay, Karatu, ili wasaidie kazi za uwekaji umeme kwenye vijiji 39 vya wilaya hiyo.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea wilaya hiyo na kuzindua mradi wa umeme vijijini awamu ya tatu unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (Rea) hafla iliyofanyika kiwilaya katika Shule ya Sekondari ya Baray Khusumay.

Dk. Kalemani alisema ameagiza utoaji wa ajira hiyo kwa sababu mkandarasi huyo amepewa kumaliza kazi ya uwekaji miundombinu ya umeme na kuwaunganishia wananchi nishati hiyo kwa muda wa miezi 24, lakini mpaka sasa hajafikia hata nusu ya kazi.

"Sasa naagiza ajiri vijana 50 wa eneo hili ili muda wako tuliowekeana mkataba umalize ni Juni, 2020 lakini nataka umalize kazi hii Desemba 30, mwaka huu, sasa hawa vijana watakusaidia na wakati huo watanufaika na ajira na Meneja wa REA Wilaya simamia hawa," alisema.

**Sasa naagiza ajiri vijana 50 wa eneo hili ili muda wako tuliowekeana mkataba umalize ni Juni, 2020 lakini nataka umalize kazi hii Desemba 30, mwaka huu.**

Dk. Kalemani aliahidi kurudi kijijini hapo kufuatilia kama kazi hiyo imeisha kwa wakati muafaka ili wananchi wapate umeme na kuzalisha mali kupitia viwanda vidogo vidogo.

Pia alimwagiza Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wa wilaya hiyo, Edward Mwakapuja, kufungua vituo kwenye vijiji husika ili wananchi wapate unafuu wa kuwafikia na kulipa Sh. 27,000 ili waunganishiwe umeme huo wa REA.

Sambamba na hilo, Waziri Kalemani aliwataka wafanyakazi wa Tanesco kuhakikisha wanafanya kazi za kuhudumia wananchi na kuepuka kuvaa suti kama wanakwenda kanisani.

"Nimepiga marufuku wafanyakazi Tanesco kuvaa suti labda kama mnaenda kanisani Jumapili, sababu hapa kazi tu. Suti na kazi wapi na wapi? Acheni kabisa pigeni kazi," alisema.

Aliwasihi pia wananchi hao kutunza miundombinu ya umeme waliyowekewa ili waendelee kunufaika nao na kupata maendeleo.

Dk. Kalemani aliwaagiza wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Baray Khusumay kuhakikisha wanafanya vizuri masomo yao na kufaulu vizuri kwa sababu umeme wameshapata.

Kuhusu suala la kukatika kwa umeme, aliagiza Tanesco kuhakikisha wanamaliza tatizo hilo haraka kwa sababu umeme upo wa kutosha hadi ziada. Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alishukuru serikali kwa kuwafikishia umeme kijiji hicho ambacho tangu Uhuru hakijawahi kupata umeme. Pia aliomba waziri kufuatilia changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara wilayani humo.

Akijibu suala la kukatika kwa umeme, Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herin Mhina, alisema sababu ya kukatika kwa umeme huo ni kutokana na utengenezaji wa zaidi ya nguzo 600 ambazo zimewekwa mpya.



Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justin Nyari, akifurahia kwa kumtunza msanii kwenye kikao cha wadau wa madini ya Tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Makandarasi barabara lami wapewa somo

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

MAKANDARASI wanaotengeneza barabara kwa kiwango cha lami katika Jiji la Arusha, wametakiwa kuzingatia maelekezo ya mikataba yao inayowataka kutoa kipaumbele cha ajira kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mradi.

Ofisa Tarafa wa Themi, Felician Mtahengerwa, alisema hayo wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya CCM Kata ya Levolosi ya kutembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Miradi waliotembelea ni pamoja na kukagua barabara zenye urefu mita 585, zinazojengwa katika kata hiyo na Kampuni ya Ravji ya Moshi mkoani Kilimanjaro, soko la Kilombero na ukarabati wa kituo cha Polisi cha Kilombero, alichobaini kuwa na changamoto kubwa ya kuvuja wakati wa mvua.

Mtahengewa aliitaka kampuni hiyo kuwapatia ajira vijana waliko katika eneo la miradi katika kata hiyo bila kujali itikadi zao za kisiasa. Pia aliitaka kampuni hiyo kukamilisha mradi huo kwa wakati na kwa ubora unaohitajika. Alisema kuna umuhimu wa wadau wa maendeleo kuona uwezekano wa kukarabati Kituo cha Polisi cha Kilombero kwa kujitolea samani za ofisi sambamba na ukarabati wa paa na kusaidia ulipaji wa deni la maji, kwa kuwa kituo hicho kinasaidia usalama katika eneo hilo.

"Unajua suala hili si la lazima ni hiari ya wadau wa maendeleo kuona umuhimu wake kwani kituo hiki kinasaidia sana katika kulinda mali zao na usalama katika eneo hili, hivyo waone umuhimu wa kuisaida serikali kujitolea," alisema.

Naye msimamizi wa kampuni hiyo, Peter Mahushi, alisema atahakikisha wanamaliza kazi katika muda uliopangwa na kwamba ifikapo Septemba 14, mwaka huu, watakabidhi miradi hiyo.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa vijana wa kata hiyo kwa kuanza na vijana watano na kuwataka viongozi kuwapelekea majina yao ili yaangaliwe uwezo wao na kuahidi changamoto zote kuzifanyia kazi ndani ya muda uliopangwa.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Levolosi, Tabu Simile, alisema CCM imeridhishwa na ujenzi wa miradi ya barabara kwa kuona thamani ya fedha inayotolewa ikitumika kama ilivyokusudiwa.

Alitaka changamoto ndogo walizokutana nazo wahusika wazitatue kama walivyoahidi ndani ya muda ili kwenda sambamba na kasi ya ujenzi wenye viwango vinavyokubalika.

Miradi hiyo ya ujenzi wa barabara za lami katika Jiji la Arusha, inatekelezwa kwa kiwango kikubwa na serikali chini ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), jambo ambalo linazidi kuung'arisha Mji wa Arusha.





# DC ahimiza ukulima wa kisasa migomba

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

MKUU wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, amewataka wakazi wa wilaya hiyo ambao kwa asilimia 90 ni wakulima, kujikita zaidi katika matumizi ya mbinu bora za kilimo cha migomba.

Pia amwataka kujielekeza kwenye mafunzo ya uboreshaji wa kilimo ambayo yanatolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Tengeru mkoani Arusha.

Hokororo alisema hayo juzi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakulima wa Migomba, alipokwenda katika Kata ya Mengeni kuzindua machapisho mbalimbali yanayohusu mradi wa uhamasishaji wa mbinu bora za kilimo cha migomba.

"Ndizi kwetu ni jambo la msingi sana. Kila mmoja wetu atapaswa kuweka nguvu zake zote kuhakikisha tunaendelea kuboresha kilimo chetu cha migomba kwa kutumia mbinu bora za kilimo na teknolojia tuliyoletewa na wenzetu wa Tari-Tengeru. Wakulima ni lazima tuhudhurie mafunzo katika mashamba darasa 50 yaliyoanzishwa na wataalamu wa kilimo kwa ajili ya kufundisha wakulima," aliagiza.

**Kila mmoja wetu atapaswa kuweka nguvu zake zote kuhakikisha tunaendelea kuboresha kilimo chetu cha migomba kwa kutumia mbinu bora za kilimo na teknolojia tuliyoletewa na wenzetu wa Tari-Tengeru.**

Alisema wakulima wa Wilaya ya Rombo, wana kila sababu ya kuimarisha kilimo cha migomba kwa kuwa ubora wa ndizi zitakazozalishwa ndiyo mabadiliko yanayotakiwa katika kufikia uzalishaji endelevu wenye mchango chanya katika ukuaji wa uchumi, usalama wa chakula na lishe bora.

"Na hili nalisukuma pia kwa watendaji wa vijiji. Kama kuna vijiji ambavyo vimetajwa kwenye huu mradi na namna hasa ya kuifanya hiyo migomba iwe bora, kuna haja ya kuhimiza wananchi wetu wazingatie matumizi ya teknolojia za kuboresha kilimo cha migomba zinazofundishwa na watafiti wa Tari-Tengeru," aliagiza.

Kwa sasa, vijiji 45 vya wilaya ya Rombo, vinalima ndizi kati ya vijiji 68 na eneo ambalo unatekelezwa mradi wa uhamasishaji wa mbinu bora za kilimo cha migomba ni kata za Mamsera, Challa, Mengwe, Mengeni, Mandan na Aleni. Mpaka sasa, mashamba darasa 50 yameanzishwa na wakulima 3,402 wamefikiwa na mradi huo.

"Kwa bahati mbaya sana taarifa zetu zote hapa inaonekana kwamba bado wakulima hawajawa na mwamko wa kutosha. Sasa mimi kwenye maeneo ya namna hii huwa najiuliza, hivi kwa sasa tungependa tupewe nini? Tumepata mradi unaofadhiliwa na Bill & Mellinda Gates, tumepata wadau ambao wanatufanyia utafiti kwenye eneo letu na tumeona haya mashirika yote manne yameamua kufanya kazi ili kuboresha uzalishaji wa kwenye Wilaya ya Rombo.

"Shida yetu kubwa, hawa wamekuja kwetu, tena wanatupatia ujuzi bure na maelezo bure, utaalamu bure, hatununui lakini wakulima hawajiongezi na kukubali kutoka kwenda kusikiliza utaalamu wanaopewa. Wote tunakubaliana kwamba ndizi ni zao la chakula, ndizi ni ajira na ndizi ni biashara, tubadilike na tuanze kuona mabadiliko ya zao hili katika wilaya yetu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa msimamizi wa mradi huo, Juma Kitundu, moja ya mambo yanayosisitizwa kwa wakulima hasa kuhudumia shina la mgomba ni kupunguza miche ya ziada, kuondoa matunguu, kuondoa ua dume na kuweka miega.

Mambo mengine ni kuchimba mitaro shambani ili kuzuia upotevu wa maji ya mvua kwa kutumia makinga maji, kuweka samadi, matandazo na kudhibiti visumbufu vya migomba kwa kusafisha miche kuzuia mdudu fukusi na minyoo ya ardhini.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (kulia), akikagua shamba la chumvi la kiwanda cha Uvinza, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kigoma juzi, kusikiliza changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi. Wa pili kulia anayetoa maelezo ni Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Mukash Mamlani na Meneja wa kiwanda hicho, Ben Mwaipopo. **PICHA: WM**

# Polepole ajitosa madai ya walimu

**Na Paul William,** MOSHI

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, amejipa kibarua cha kufuatilia madai yote ya walimu wa mkoa wa Kilimanjaro ikiwamo malimbikizo ya fedha za likizo ambayo bado wanaidai serikali.

Polepole aliahidi kushughulikia madai hayo juzi baada ya kuzindua Jukwaa la Walimu wazalendo mkoa wa Kilimanjaro.

"Nileteeni orodha ya majina ya walimu wa mkoa wa Kilimanjaro ambao wanaidai serikali ili niyafuatilie na walipwe stahiki zao," aliagiza.

Alisema serikali imekuwa ikiwapandisha madaraja walimu, lakini imekuwa haitoi malipo stahiki kwa madaraja hayo mapya kwa kipindi kirefu tangu walipopanda madaraja yao.

Mbali na ahadi hiyo, Polepole akiwa mkoani Kilimanjaro aliongoza uchangishaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa kituo cha Polisi Usangi kilichoko wilayani Mwanga, ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Umoja wa Vijana (UVCCM) Wilaya ya Siha na ujenzi wa choo cha wanafunzi katika Wilaya ya Rombo.

Katika hafla za uchangishaji wa fedha kwa ajili ya miradi hiyo ya ujenzi, Polepole amefanikisha kukusanya mifuko 315 ya saruji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Walimu Wazalendo Taifa, Asha Feruzi, alisema jukwaa hilo la walimu wazalendo ni sehemu ya watu wa kwanza kutengeneza kura za CCM.

"Tunataka walimu kuonyesha kwa vitendo jambo hili. Hatutaki tena lawama tulizopewa mwaka 2015 wakati wa uchaguzi mkuu wala hazitajirudia katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani. Tutahakikisha CCM inashinda kwa kishindo," alisema.

**Tunataka walimu kuonyesha kwa vitendo jambo hili. Hatutaki tena lawama tulizopewa mwaka 2015 wakati wa uchaguzi mkuu wala hazitajirudia katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani.**

# Manispaa Moshi yaja kivingine uwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MEYA wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, amesema halmashauri hiyo imeanza mchakato wa kuainisha fursa za uwekezaji wa miradi miwili ya kimkakati ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata takataka na kutengeneza mbolea pamoja na mradi wa machinjio ya kisasa itakayojengwa Kata ya Bondeni.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu miradi hiyo, Mboya alisema kiwanda cha kuchakata takataka na kuzalisha mbolea, kinaweza kuigharimu zaidi ya Sh. milioni 900.

Meya huyo alisema mchakato huo ukikamilika pamoja na ujenzi wake, mradi huo utaongeza uwezo wa halmashauri kuzoa taka kutoka tani 168 kwa siku hadi tani 230.

"Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni kutaka kuendelea kubakia kileleni na kutetea heshima yake ya kuwa kinara wa usafi wa mazingira kitaifa. Tulianza mchakato huo kwa kuagiza malori makubwa matatu China ambayo yana uwezo wa kuchukua tani 100," alisema Mboya.

Kuhusu ujenzi wa majengo ya uwekezaji kibiashara, Meya huyo alisema halmashauri hiyo ina mpango wa kujenga jengo la uwekezaji wa kibiashara katika eneo la stendi kuu ya mabasi.

Katika sekta ya masoko, Mboya alisema mpango uliopo kwa sasa ni kujenga soko la kisasa eneo la Shanty Town, kujenga soko la Mbuyuni kwa mfumo wa ghorofa na soko la kati kwa mfumo wa ghorofa.

Kwa sasa, alisema halmashauri hiyo imeanza kutekeleza mkakati wake wa ujenzi wa stendi ya kimataifa ya mabasi ya Ngangamfumuni ambayo itakuwa mradi mkubwa kuliko yote iliyopangwa kutekelezwa.

Stendi hiyo ya mabasi yaendayo mikoani, ambayo serikali imetoa Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kuanza ujenzi wake, inajengwa na kampuni ya ujenzi ya kimataifa ya CRJE (East Africa) Ltd kwa mkataba wa miezi 24.

Ukurasa 18



Washirika wa Marekani wa mtaka Jenerali Hafta]r, waipuuza UN

## TUJIKUMBUSHE:
YAKUBU GOWON



Ukurasa 19

## Kimataifa



## EAC isipuuzie mgogorohuu wa Rwanda, Uganda

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JULAI 31, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




## Mbunge aliyeng'ong'wa na Trump aipania Israel, haigusi Somalia

Ukurasa 20

### BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-7

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa Serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya saba ya kitabu hicho inayoanzia na Changamoto ya Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

**5.3 Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano**

Hii nayo imekuwa ni kero kubwa kwa upande wa Zanzibar. Tarehe 2 Desemba, 1994, Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha mabadiliko kumi

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. PICHA: MTANDAO

## Ripoti ya mauaji yazusha maandamano mapya Sudan

Ukurasa 17

# EAC isipuuzie mgogoro huu wa Rwanda, Uganda

**Na Mashaka Mgeta**



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto), akiwa na Rais Paul Kagame wa Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

KUKOSEKANA kwa ushirikiano kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kunaweza kuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu, mipango na mikakati ya kufikia lengo la kuundwa kwake.

Ingawa ni ukweli usiopingika kwamba katika jumuiya yenye nchi sita zilizo wanachama kama ilivyo EAC haiwezi kukwepa kutofautiana, lakini misingi na kanuni za usuluhishi wa migogoro inapojitokeza inapaswa kutekelezwa kwa haraka na ukali, ili iwe kwa maslahi ya jumuiya nzima.

Kuendelea kupuuzia migogoro iliyopo kwenye ukanda kama EAC, ni sawa na kukaribisha ienee kwenye mataifa mengine yakiwamo yenye uhusiano mzuri miongoni mwao na kati ya wananchi wake.

Kwa bahati mbaya, mgogoro wa kidiplomasia uliopo kati ya Rwanda na Uganda unazidi kukua, ukihusisha matukio mapya yanayoashiria kutoweka kwa uwezo wa kurejea hali ya maelewano kati yao.

Kila nchi imekuwa ukiishutumu nyingine kwa kuhusika na vitendo vya jinai vinavyokiuka sheria za kimataifa na hata ubinadamu.

Shutuma hizo zimekuwa zikitolewa kwa njia mbalimbali ikiwamo hotuba, matamko ya maandishi na uenezi wa propaganda hasa kupitia vyombo vya habari.

Jumanne ya wiki iliyopita, vikosi vya usalama vya Uganda vinadaiwa kuwakamata raia 40 wa Rwanda waliokuwa kwenye eneo la Kabuye, karibu na jiji la Kampala.

Kukamatwa kwa wanachama hao wa kanisa la ADEPR unadaiwa kuratibiwa na mawakala wa kikundi cha upinzani cha Rwanda National Congress (RNC) cha Kayumba Nyamwasa, gazeti la New Times limeripoti.

Mawakala hao wakatajwa kuongozwa na Frank Ruhinda na 'Mchungaji'Busigo. Wawili hao wanashukiwa kujihusisha na harakati za kuipinga serikali ya Rwanda inayoongozwa na Rais Paul Kagame, wakifadhiliwa na kuwezeshwa na serikali ya Uganda.

Waumini hao walio raia wa Rwanda, wanadaiwa kukamatwa na majeshi ya usalama ya serikali ya Uganda inayoongozwa na Rais Yoweri Museveni kwa tuhuma kwamba ni 'mashushushu' wa DMI.

Gazeti hilo likaandika kuwa taarifa zilizopatikana kutoka kwa watu wanaosadikiwa kuwa waumini wa kanisa hilo wasiotaka kujulikana kwa sababu za kiusalama, zinadai kuwa, siku chache zilizopita, Ruhinda na Busigo walifika mara kwa mara huko Kibuye wakiwa na mipango ya kuichafua serikali ya Rwanda.

Ikaelezwa kwamba kwa wenye uelewa kuhusu shughuli za RNC nchini Uganda, kikundi hicho kilikabiliwa na wakati mgumu kwenye eneo la mpaka na nchi ya DRC miezi michache iliyopita kwa kudhibitiwa na jeshi la nchi hiyo (FARDC) na sasa kinajijenga tena.

Lakini wakati wafuasi wa RNC walipojaribu kuingiza siasa zao kanisani, wakihusisha zaidi suala la 'mabadiliko nchini Rwanda'uongozi wa kanisa hilo uliwakatalia.

Vyanzo mbalimbali vikakaririwa vikidai kuwa Ruhinda na Busigo wamekuwa wakiwasumbua baadhi ya waamini wa kanisa hilo kushirikishana nao kuhusu mikakati yao ya kiintelijensia.

Inaelezwa kwamba waamini hao waliwaambia kwamba imetosha kwa Rwanda kuwa na vita na umwagaji damu, kwa maana mambo hayo yalishatokea na kuliathiri taifa hilo.

Pia wanadaiwa kujulishwa kwamba, "ni dhana potofu kwa mtu yeyote kupanga na kutekeleza vitendo vya umwagaji damu kupitia kwenye nyumba ya kumwabudu Mwenyezi Mungu."

Kwa kikwazo hicho, gazeti hilo likaeleza kwamba vyanzo mbalimbali vililiarifu kwamba wawili hao, walikasirika kiasi cha kuwatishia viongozi wa kanisa hilo kwamba watakabiliwa na mambo mabaya.

Waangalizi wa shughuli za RNC nchini Uganda wanakaririwa na gazeti hilo wakiainisha ushahidi wa mazingira unaokifunganisha kikundi hicho na taasisi za usalama na kitengo cha intelijensia cha jeshi la nchi hiyo.

Rwanda imekuwa ikilalamika kuwapo raia wa nchi hiyo wanaoteswa kwenye mahabusu ya kambi ya kijeshi iliyopo Mbuya ambapo ni Makao Makuu ya jeshi la Uganda.

Inaelezwa kwamba, baada ya kushindwa kutimiza matakwa yao kwenye kanisa la ADEPR, wanaotajwa kuwa mawakala wa RNC 'wakawachomea utambi' wafuasi wa kanisa hilo waliokuwapo Kibuye.

Wafuasi hao wanadaiwa kuzingirwa na wana usalama wa Uganda majira ya mchana wakati wakiwa kwenye ibada.

Gazeti hilo likaeleza kwamba mashuhuda waliona magari matatu ya kiraia kama yanayotumiwa kwa usafiri wa umma nchini Uganda na mengine matatu ya polisi maarufu kama "panda gari" yakifika mahali walipokuwa waamini hao wa ADEPR huko Kibuye.

Mwanaume aliyekuwa amevalia nguo za kiraia pamoja na mwingine mwenye sare za polisi wa nchi hiyo walitoka nje ya magari hayo na kuweka 'uzio' kwenye eneo la kuingilia mahali hapo.

Inaripotiwa kuwa wakati umati ukishuhudia tukio hilo, askari wa usalama waliingia kanisani hadi kufika kwenye gorofa ya kwanza na kuwatoa nje.

Waamini hao wanadaiwa kutii agizo la maofisa wa usalama wa Uganda na kushuka hadi eneo la chini ya jengo walimokuwamo na kuingizwa ndani ya magari mawili yaliyowasili kwenye eneo hilo.

Kwa mujibu wa gazeti hilo, kwenye kundi la waamini hao walikuwamo wanaume, wanawake na watoto na baada ya kila mmoja kuingia kwenye gari, wakapelekwa eneo lisilojulikana.

Baada ya hapo, mitandao ya kijamii ikiwamo blogu ya CommandPost na magazeti kama Daily Monitor, yaliandika kuwa kitengo cha intelijensia cha jeshi la nchi hiyo na polisi waliwakamata wanaintelijensia wa Rwanda.

Shutuma hizo zinadaiwa kumuibua Mchungaji John Karangwa aliye mwanasheria wa ADEPR jijini Kigali, Rwanda kuhoji mantiki ya kuwatangaza waamini hao kuwa ni mashushushu.

Mchungaji Karangwa akakaririwa na vyombo vya habari vya Rwanda akisema, " Ni wazi kwamba taasisi za usalama zilizwalenga wafuasi wa ADEPR tu kwa sababu walikuwa na majina ya Kinyarwanda. Lakini nataka kuwaambia kwamba wapo Waganda ambao ni wafuasi wa kanisa hilo. Lengo letu ni kuwainjilisha watu wote wa dunia."

Rwanda imekuwa na muendelezo wa kuishutumu Uganda kwa kuwatesa raia wake wanaoingia nchini humo, lakini pia kuvisaidia vikundi vya uasi vyenye lengo la kuuangusha utawala wa Rais Kagame. Uganda imeyakanusha madai hayo mara kwa mara.

Lakini kwa upande wake, Uganda nayo imekuwa ikiishutumu Rwanda kwa kupanga njama za kuuangusha utawala wa Rais Museveni kupitia mashushushu wanaoingia nchini humo kwa shughuli mbalimbali za kijamii.

Rwanda kadhalika imekanusha madai hayo na hivyo kuwa sehemu ya kuzidi kuenea kwa mgogoro wa kidiplomasia kati ya mataifa hayo.

Serikali ya Kagame inaamini kuwa RNC inahusika na mashambulio ya mabonu nchini Rwanda yakiwamo yaliyowaua watu watu 17 na kuwajeruhi wengine wanaokadiriwa kufikia 400.

Mmoja wa Wanyarwanda anayedaiwa kuteswa na vikosi vya ulinzi vya Uganda ni Roger Donne Kayibanda, ambaye kupitia mitandao ya kijamii alidaiwa kwenda nchini humo Januari mwaka huu kushiriki hafla ya harusi ya kaka yake, lakini akajikuta mikononi mwa wana usalama kwenye kitongoji cha Kisaasi karibu na Kampala.

Inaelezwa na gazeti hilo kuwa, akiwa anastarehe na rafiki zake, watu watano walimzunguka na kumchukua.

Wakati Kayibanda alipojaribu kuwakatalia, anadaiwa kuchukuliwa kwa nguvu na kuingizwa ndani ya gari lililokuwa na vioo vyenye vizuizi vya kuona ndani.

Ni wazi kwamba mwendelezo wa mgogoro huu wa kidiplomasia hauna tija kwa EAC.

Ipo haja kwa jumuiya hiyo kutafakari ushiriki wake katika kuusuluhisha kabla haujazigawa nchi wanachama na hivyo kuwepo hatari ya kuenea kwenye mataifa mengine zaidi.

***Makala haya yameandikwa kutoka vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.***

Na Fransisko Mpangala

# Mitandao ya kijamii ijenge utangamano, si chungu katika jamii

MWISHONI mwa mwaka jana simu yangu ya smartphone ilizima ghafla na kushindwa kuwaka tena.

Kwa kuwa ilitokea ghafla sana, ilinichukua miezi miwili kujipanga upya ili kununua smartphone nyingine.

Kitendo cha kukosa smartphone kwa miezi miwili kilikuwa pigo kubwa sana kwangu kwani, matumizi ya simu ya kawaida (tochi) ambayo hayana huduma ya intaneti yalininyima fursa ya kupata habari na mijadala mingi ya kisiasa kupitia mitandao ya kijamii kama nilivyozoea.

Hakika nimekuja kuithamini sana mitandao ya kijamii, hasa kipindi kile cha miezi miwili niliyoshindwa kuipata huduma yake (wanasema ukose kitu ndio ujue umuhimu wake).

Kushindwa kuitumia mitandao hii kulinifanya kuitazama mitandao ya kijamii kwa namna ya kipekee na lazima nikiri kuwa msukumo wa kuandika makala hii unatokana na shauku ya kuelezea umuhimu wa mitandao ya kijamii uliongezeka maradufu kipindi niliposhindwa kuipata huduma yake.

Mitandao ya kijamii inatafsiriwa kama nyenzo ya kuunganisha watu kwa kuwaleta pamoja na kujenga urafiki miongoni mwao ndani na nje ya nchi.

Pia inaunganisha watu wenye shauku ya aina moja, kwa maana mtumiaji anapaswa kujitambua mapema, na kujiweka katika kundi analodhani linamfaa au lina manufaa zaidi kwake.

Binafsi ninapenda kufuatilia mambo ya siasa, kwa maana hii niliigeuza mitandao ya kijamii kama chombo cha habari kwa kupafanya pahala pa kujifunza, kuhabarika na kijiwe cha kujadili mambo ya siasa.

Ingawa zipo faida nyingi za mitandao ya kijamii, itakuwa ni ajabu sana nikijisahaulisha kuwa hakuna changamoto zilizoletwa na mitandao ya kijamii.

Hivyo makala hii italenga kuchambua faida na hasara zilizoletwa na mitandao hiyo ya kijamii kwa upande wa siasa na wanasiasa kwa ujumla.

**TAMU ZA MITANDAO YA KIJAMII**

Mitandao ya kijamii inatoa fursa ya kupata habari nyingi za kisiasa ndani ya muda mfupi.

Katika moja ya makala ya mwandishi Christian Bwaya inayohusiana na mambo ya teknolojia anasema:

"Mitandao hii hasa ya kijamii ni kama 'maporomoko' ya habari mpya kila sekunde yanaitwa 'streaming', 'TL' na majina mengine.

Kadri unavyofuatilia habari moja, ndivyo unaletewa 'mafuriko' ya zingine mpya.

Hukutani na ishara kuwa sasa umekaribia kufikia mwisho, kapumzike. Matokeo yake unaweza kujikuta muda wote unaunganisha habari moja kwenda nyingine.

Ingawa mwandishi huyu alikuwa anajaribu kuzungumzia changamoto za kutumia mitandao hii (nitayajadili mwishoni) lakini kwa upande mwingine, maneno hayo yanaelezea faida kubwa iliyoletwa na mitandao ya kijamii kwa wadau wa siasa.




Jengo la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika barabara ya Sam Nujoma jijini Dar es Salaam. TCRA ina jukumu pia la kuratibu matumizi ya mitandao. **PICHA: MTANDAO**

Mtumiaji ana uhakika wa kupata habari nyingi za kisiasa kadri muda na nafasi yake itakavyomruhusu.

Mtumiaji halazimiki kusubiri au kutegemea taarifa ya habari kwa kuwa ana uhakika wa kupata habari 'mithili ya mafuriko' muda wowote anaojisikia kiganjani.

Mitandao ya kijamii kwa upande mwingine imezidisha fursa kwa wadau wa siasa kutoa maoni yao kuhusiana na habari, mijadala au makala mbalimbali kwa njia ya ujumbe mfupi 'comments'.

Kwa maana hii ushirikishwaji wa watu kutoa mawazo yao kuhusiana na mambo ya kisiasa umeongezeka maradufu. Pia inatoa fursa kwa mtoa habari, mjadala au makala kujua maoni ya watu kuhusiana na taarifa husika.

Faida nyingine inayotokana na mitandao ya kijamii ni kuibuka kwa kundi la watu wanaojiita 'wanaharakati'.

Kwa kujua na kutambua nguvu ya mitandao ya kijamii katika kufikisha ujumbe, 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' hufanya kila wawezalo kuitumia ipasavyo kufikisha sauti zao zisikike na hatimaye kuleta tofauti inayokusudiwa kwa nia njema.

Hii imesaidia kufikisha kero mbalimbali kwa Serikali au viongozi wao ili kusaidia kuzipatia ufumbuzi.

Kwa maana hii, mtu akishindwa kufikisha kilio chake kupitia vyombo vya habari, bado anaweza kuwatumia 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' kufikisha kero zake kwa viongozi na wanasiasa kwa ajili ya ufumbuzi.

Isitoshe mitandao ya kijamii imewarahisishia wananchi kuona kazi mbalimbali zifanywazo na viongozi wao.

Kupitia ukurasa wa instagram wa mbunge wa Segerea Bonnah Kaluwa, napata fursa ya kuona kazi mbalimbali zinazofanywa na mbunge huyo katika jimbo lake.

Anaitumia pia kutoa taarifa mbalimbali kama ratiba ya mikutano kati yake na wananchi wa jimbo lake. Kwa maana hii mitandao ya kijamii imewasaidia wanasiasa kufikisha taarifa zao kwa urahisi na kuwaonyesha wapigakura kazi mbalimbali za kimaendeleo wazifanyazo kwenye maeneo yao.

Mitandao ya kijamii pia inatoa fursa kwa wananchi na wadau wa siasa kuona vikao na kampeni za kisiasa 'mubashara'.

Hii imewarahisishia wanasiasa kutangaza sera na kufikisha jumbe zao kwa urahisi. Nakumbuka mwaka 2016 nilifuatilia kwa karibu kampeni za Rais Donald Trump wa Marekani kupitia facebook 'mubashara'.

Hata hivyo, hakuna zuri lisilokosa kasoro. Zipo changamoto zilizoletwa na mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa na wanasiasa.

**CHUNGU ZA MITANDAO YA KIJAMII**

Moja ya changamoto kubwa inayoikabili mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa (na kwa ujumla wake) ni kuwepo kwa habari nyingi 'feki' na za kizushi.

Kwa kuwa mitandao ya kijamii haina uchujwaji wa habari (filtration) kama ilivyo kwa vyombo vya habari, mchanganyiko wa habari za ukweli, uwongo au zilizozidishwa chumvi ni nyingi sana.

Shida inazidi kuwa kubwa kwa wapokeaji wa habari hizo ambao wanaupokea uwongo uliotolewa kwa nia mbaya kama ulivyo.

Hii inatokana na watu wengi kuwa wavivu kuchambua kwa undani au kufuatilia ukweli wa taarifa mbalimbali.

Wapo watu kwenye mitandao ya kijamii ambao kwa nyakati nyingine huitumia vibaya kuwadhalilisha viongozi wenye heshima na hadhi kubwa kwenye jamii. Ingawa yawezekana baadhi ya tuhuma zinazoanzia kwenye mitandao ya kijamii zikawa na ukweli, lakini lugha inayotumika kuwasilisha ikawa si nzuri (matusi).

Wapo wenye chuki binafsi ambao huzusha kwa makusudi habari zilizojaa chuki kwa viongozi mbalimbali kwa lengo la kuwadhalilisha au kuwashushia hadhi yao.

Mara nyingi watu wa aina hii hung'ang'ania ishu zisizo na msingi, lakini zenye madhara kwa hadhi na heshima ya mwanasiasa husika katika jamii.

Hakika hili si jambo zuri kwani viongozi na wanasiasa hawa ilichukua muda mrefu kuitengeneza hadhi na heshima waliyonayo, hivyo kutokea mtu au kikundi cha watu kuja kumchafua kirahisi kwa sababu binafsi si jambo zuri.

Kwa sisi wadau wa kufuatilia mambo ya siasa huwa tunakutana na 'watumiaji wasumbufu' kwenye mitandao hii.

Hawa ni wasumbufu kwa maana ya watu wanaovuka mipaka katika kupishana hoja kistaarabu hadi kufikia kashfa, matusi na udhalilishaji.

**USHAURI.**

Kutokana na mitandao ya kijamii kutengenezwa kwa mfumo wa kumvutia mtumiaji, wadau wanapaswa kuchukua tahadhari na kujidhibiti ili kuepuka kunogewa na kujikuta wanaitumia kila saa.

Wanapaswa kujizuia kugusagusa simu zao kuepuka 'mafuriko ya habari' za kisiasa zinazotoka kila saa, ambazo yawezekana nyingine mtumiaji hazihitaji.

Hii itasaidia wadau kuzidisha uzingativu wa shughuli wanazofanya kwenye maeneo yao ya kazi.

Lazima wadau wakumbuke kuwa mitandao ya kijamii ina mchanganyiko wa habari nyingi za ukweli na uwongo na hivyo watumiaji wanapaswa kuwa makini na ikiwezekana kufuatilia habari iliyotolewa kwa kina ili kujua ukweli wa taarifa iliyotolewa.

Vipo vyanzo makini kwenye mitandao ya kijamii ambavyo vina hadhi (status) ya kutoa habari za ukweli, hivyo nashauri zitumike hizo.

Kwa upande wa kumdhibiti mtumiaji msumbufu njia pekee ya kukabiliana naye ni 'kumblock' kwa sababu jaribio lolote la kumuelimisha hata liwe la kistaarabu kiasi gani litaishia kuzua balaa zaidi.

***Kwa maoni zaidi napatikana kwa barua pepe fransiscompangala08@gmail.com***

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-7

Inatoka Uk. 13

na moja ya Katiba ya Nchi. Miongoni mwa mabadiliko yaliyofanywa ni badiliko lililomuondoa Rais wa Zanzibar asiwe moja kwa moja ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kama ilivyokuwa hapo awali. Badiliko hili limekuwa likipingwa wakati wote na upande wa Zanzibar.

Maelezo yake ni kwamba, badiliko hilo lilifanyika kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa kwanza chini ya mfumo mpya wa Vyama vingi vya siasa, kwa lengo la kuwezesha Rais wa Jamhuri ya Muungano, pamoja na Makamu wake, wote wawili wawe wametoka katika Chama cha siasa kimoja, ili kuepusha uwezekano wa kuwa na Serikali ya Muungano ambayo ni ya mseto wa vyama vya siasa viwili tofauti.

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya kuzingatia kwamba, katika ushindani wa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar baina ya vyama vya CCM na CUF, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa chama cha CUF kupata ushindi; wakati kwa upande wa uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa CCM kupata ushindi. Maana yake ni kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano angetoka CCM, wakati Rais wa Zanzibar angetoka CUF. Hali hiyo ingeifanya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwa na Serikali ya mseto wa vyama viwili.

Ilionekana kuwa hilo lingekuwa ni tatizo. Kwa sababu kwa kawaida, Serikali ya mseto huundwa baada ya mazungumzo na makubaliano baina ya vyama husika vitakavyounda Serikali hiyo, na siyo kwa kulazimishwa na Katiba. Kwa mfano, Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyoundwa Zanzibar baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ilitokana na mazungumzo na makubaliano baina ya CCM na CUF.

Kwa hiyo, ili kuwezesha Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wa Rais wote wawili watoke katika chama kimoja cha siasa, ndipo ulipotengenezwa utaratibu mpya wa Makamu wa Rais kuwa ni mgombea mwenza wa mgombea Urais, kwani wote watakuwa wameteuliwa na Chama chao kimoja. Endapo mgombea Urais atateuliwa kutoka Tanzania Bara, mgombea mwenza atateuliwa kutoka Zanzibar; na endapo mgombea Urais atateuliwa kutoka Zanzibar, mgombea mwenza atateuliwa kutoka Tanzania Bara.

Lakini, pamoja na uzuri wa sababu hiyo, badiliko hilo limeendelea kulalamikiwa na upande wa Zanzibar hadi sasa.



Sehemu ya gwaride lililoshiriki katika mojawapo ya sherehe za Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

> Tatizo kubwa linaloonekana wazi ni hofu ya Zanzibar kumezwa. Hofu hiyo imezaa unyeti pekee katika mtazamo wa baadhi ya Wazanzibari kuhusu Muungano…Hofu ya Zanzibar kumezwa imekuwapo tangu Muungano huu ulipoundwa…

**SURA YA 6**
**MCHAKATO WA MADAI YA SERIKALI TATU**

6.1 Madai Serikali Tatu

Baada ya kufifia kwa matumaini ya kupata muundo wa Muungano wa Serikali moja; juhudi kubwa sasa zilihamia kwenye kudai muundo wa Serikali tatu.

Muundo huo wa Serikali tatu ndio uliopendekezwa na Tume ya Warioba katika Rasimu yake ya Katiba mpya iliyowasilishwa kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Lakini, yafaa ieleweke kwamba, madai ya Serikali tatu maana yake ni madai ya kurejesha Serikali ya Tanganyika iliyokuwapo kabla ya Muungano. Madai hayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara, lakini, pia yamekuwa yakikataliwa na Serikali, katika kipindi chote cha awamu zote nne za Uongozi wa nchi yetu, kama ifuatavyo:

- Madai ya mara ya kwanza yalitolewa mwaka 1984 na Rais wa Zanzibar Aboud Jumbe, wakati wa Awamu ya Kwanza ya Uongozi wa Rais Nyerere.
- Madai ya mara ya pili yalitolewa mwaka 1991 na Tume ya Jaji Mkuu Nyalali, wakati wa Awamu ya Pili ya Uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi.
- Madai ya mara ya tatu yalitolewa mwaka 1993 kupitia Azimio la Bunge la Muungano, wakati wa Awamu ya Uongozi wa Rais Ali Hassan Mwinyi.
- Madai ya mara ya nne yalitolewa mwaka 1999 na Tume ya Jaji Kisanga, wakati wa Awamu ya Uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa.
- Madai ya mara ya tano yalitolewa na Tume ya Jaji mstaafu Warioba wakati wa Awamu ya Uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Hapa chini ninaeleza sababu zilizotumika katika kupendekeza muundo wa Muungano wa serikali ya tatu; na sababu za kukataliwa kwa madai hayo.

6.2 Sababu za kupendekeza Muundo wa Serikali Tatu

Sababu kubwa inayojitokeza katika maelezo ya wale wote waliopendekeza kuwapo kwa muundo wa Serikali tatu katika nyakati hizo mbalimbali, ilikuwa ni kwamba, muundo wa Serikali tatu ndio ungekuwa jawabu la kuondoa malalamiko mengi yaliyokuwapo katika muundo wa serikali mbili.

Tume ya Nyalali ndiyo ilikuwa ya kwanza kuwasilisha hoja hii, kwa maneno yafuatayo:

"Tatizo kubwa linaloonekana wazi ni hofu ya Zanzibar kumezwa. Hofu hiyo imezaa unyeti pekee katika mtazamo wa baadhi ya Wazanzibari kuhusu Muungano…Hofu ya Zanzibar kumezwa imekuwapo tangu Muungano huu ulipoundwa, na ndiyo iliyowafanya waasisi wa Muungano wakubaliane kwamba, Zanzibar itabaki na serikali yake, ikiwa na mamlaka kamili ndani ya Zanzibar juu ya mambo yote yasiyokuwa ya Muungano…Lakini, muundo huo hadi leo hii, miaka 27 baadaye, bado haujaweza kuondosha hofu hiyo…Wapo watu wanaosema kwamba, malalamiko na matatizo yaliyopo katika Muungano yanasababishwa na mambo madogomadogo ambayo yanaweza kurekebishwa bila kubadilisha mfumo mzima wa Muungano…Tunaamini kwamba, tatizo lenyewe limejengeka ndani ya muundo wa serikali mbili .Ndiyo sababu tunapendekeza mabadiliko ya kwenda kwenye serikali tatu."

Tume zote zilizofuata, yaani, Tume ya Kisanga (1999) na Tume ya Warioba (2013) zimekuwa zikitumia hoja hiyohiyo kama sababu yao kubwa ya kupendekeza muundo wa serikali tatu.

**6.3 Sababu za kukataliwa kwa madai yaliyotangulia**

Kuna sababu tatu kubwa na muhimu ambazo zimekuwa zikizuia madai ya muundo wa muungano wa serikali tatu yasikubaliwe. Sababu hizo ni:

**6.3.1 Kukataa kukiukwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Muungano (Articles of Union)**

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ni Muungano wa hiari, uliofikiwa baada ya mazungumzo na maafikiano baina ya Rais Nyerere wa Jamhuri ya Tanganyika kwa niaba ya watu wa Tanganyika na Rais Karume wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kwa niaba ya watu wa Zanzibar. Baada ya hapo, vilevile kwa hiari, uliridhiwa na vyombo vya kutunga sheria vya nchi hizi mbili kwa niaba ya wananchi wote wa nchi zao. Hakuna upande mmoja uliolazimisha upande mwingine kuingia katika Muungano huo.

Kama tulivyokwishakuona, muundo wa Muungano uliwekwa na Mkataba wa Makubaliano ya Muungano (Articles of Union) na ambao ndio pia, uliridhiwa na vyombo vya kutunga sheria vya nchi hizi, zilizoungana, ni muundo wa serikali mbili, yaani, Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar

Hiyo ndiyo sababu kubwa ya kukataliwa kwa madai yote hayo. Sababu nyingine ni hizi zifuatazo:


**6.3.2 Kwamba, madai hayo hayakuwa yakitoka kwa wananchi walio wengi.**

Ushahidi wake ni kama ifuatavyo:

(i)Madai ya Rais Aboud Jumbe wa Zanzibar, 1984

Tukianza na madai yaliyoibuliwa mwaka 1984 na Rais Jumbe wa Zanzibar, ni dhahiri kabisa kwamba, madai hayo hayakutokana na Wazanzibar walio wengi, kwa sababu hakuna ushahidi unaoonesha kwamba, wananchi wa Zanzibar waliulizwa watoe maoni yao juu ya suala hilo. Badala yake Rais Jumbe alifanya maandalizi yake kimyakimya tu, kwa kumtumia Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar wakati huo, kuandaa rasimu ya mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa madhumuni hayo.

Maandalizi hayo ya siri yalipojulikana, na ushahidi wa rasimu ya mabadiliko hayo ya Katiba kutolewa katika kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM cha mwezi Februari, 1984; Kiongozi huyo alilazimika kujiuzulu nyadhifa zake zote. Hoja ya Rais Aboud Jumbe ilikuwa ni kutaka kuwapo kwa Serikali ya Tanganyika kuonekane wazi katika Muungano huu, ili Serikali ya Tanganyika isiendelee kuonekana "imevaa koti la Muungano."



Viongozi wa Kijeshi na wa Kiraia nchini Sudan ambao wamekubaliana namna ya kuongoza taifa hilo kwa kugawana katika kipindi cha miezi 36.**PICHA: MTANDAO**

# Ripoti ya mauaji yazusha maandamano mapya Sudan

KAMATI iliyoundwa kufanya uchunguzi wa mauaji Sudan, imesema jumla ya watu 87 waliuawa na wengine 168 walijeruhiwa wakati vikosi vya usalama viliposhambulia maandamano ya amani katika Jiji la Khartoum hapo Juni 3.

Ukandamizaji huo ulitokea wakati maofisa wa ngazi ya juu walipokiuka amri iliyotolewa na Baraza la Mpito la Kijeshi (TMC), anasema mkuu wa kamati hiyo ya uchunguzi iliyoundwa na TMC, Fath al-Rahman Saeed.

Kwenye ripoti yake, Saeed anasema majenerali wanaongoza nchi hawakutoa amri ya kutawanya maandamano ya Juni 3 na kuwatuhumu askari wa Kikosi cha Kupambana na Fujo (RSF) kwa mauaji hayo.

Anaongeza kuwa maofisa wanane wa RSF walikaidi amri ya kutawanya maandamano ya amani siku hiyo ya Juni 3 Jijini Khartoum.

Ingawa hakutoa maelezo ya kina jinsi uchunguzi utakavyoendelea dhidi ya maofisa wanaotuhumiwa.

Aidha, Saeed anasema vikosi vya usalama vilipewa maagizo ya kutawanya watu eneo la karibu na walikopiga kambi waandamanaji linaloitwa Colombia, lakini si kuvamia na kushambulia kambi hiyo kwa sababu ilikuwa ni alama ya vuguvugu lililochangia jeshi kumuondoa kiongozi wa muda mrefu Omar al-Bashir.

Baraza la majenerali linaloiongoza nchi limekuwa likisisitiza kwamba, halikutoa amri ya kutawanya umati wa waandamanaji lakini lilitoa agizo ya operesheni ikiwemo ya RSF na vikosi vingine ya kusafisha eneo la Colombia, ambalo wanasema lina shughuli za dawa za kulevya na ghasia.

"Waliondoa vizuizi, wakafyatua gesi ya kutoa machozi na kufyatua risasi kiholela, hivyo kusababisha mauaji ya waandamanaji na wengine kujeruhiwa na kuchomwa kwa matenti," anasema.

UPINZANI WAKATAA UCHUNGUZI

Muungano wa upinzani wa uhuru na mabadiliko (FFC), hata hivyo umeikataa ripoti ya kamati ukisema watu zaidi ya 100 waliuawa na kutaka uchunguzi huru.

Siku hiyo ya Juni 3, askari waliokuwa wamevalia sare za kijeshi walivamia eneo ambalo waandamanaji waliketi hapo kwa muda mrefu, nje ya makao makuu ya jeshi na kuanza kuwafyatulia risasi na kuwapiga waandamanaji.

Nalo Shirikisho la Wanataaluma wa Sudan (SPA), limekataa uchunguzi huo likisema:

"Uliagizwa na baraza la kijeshi lenyewe, na hii inatoa doa uadilifu wake kwasababu jeshi linatuhumiwa katika kesi hiyo."

Kwa upande wao, waandamanaji waliojawa na ghadhabu waliandamana Jumamosi iliyopita wakiikataa idadi iliyotolewa kama anavyosema mwandamanaji mmoja Amam al-Tahir:

"Uchunguzi huu hauna maana kwasababu tunafahamu kilichotokea dhidi ya waandamanaji."

Awali, waandamanaji na makundi ya haki za binadamu yalikituhumu kikosi cha RSF kwa ukandamizaji uliofanywa, lakini madai hayo yalikanushwa na mkuu wa kikosi hicho Jenerali Mohamed hamdan Daglo.

Lakini uchunguzi wa pamoja uliofanywa na waendesha mashtaka na baraza la kijeshi umedhihirisha kuwa kikosi hicho sambamba na vikosi vinginevyo vilishiriki mauaji ya Juni 3.

Umati wa waandamanaji ulipiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi kuanzia Aprili 6, wakilitaka jeshi kuungana nao kumuondoa Al-Bashir.

Bashir aliondolewa Aprili 11, lakini waandamanaji waliendelea kupiga kambi wakilishinikiza baraza la kijeshi lililochukua madaraka kukabidhi madaraka kwa raia.

Mauaji hayo ya Juni 3 yalisababisha kuvunjika kwa mazungumzo baina ya jeshi na viongozi wa kiraia, lakini wiki kadhaa baadaye mazungumzo hayo yaliendelea chini ya upatanishi wa Umoja wa Afrika (AU) na wanadiplomasia wa Ethiopia.

Pande zote mbili zimekubaliana kugawana madaraka kwa kipindi cha mpito cha miezi 39. DW

UCHAMBUZI

# Washirika wa Marekani wamtaka Jenerali Haftar, waipuuza UN

• Ni katika mgogoro wa Libya

Na Nimi Mweta

NCHI zenye nguvu Mashariki ya Kati ambazo pia ni washirika wakubwa wa Marekani zinaonekana wazi kupendelea kufaulu kwa Jenerali Khalifa Haftar, kiongozi wa kundi la uasi lenye uelekeo wa kuiondoa madarakani serikali inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa jijini Tripoli.

Taarifa za wiki chache zilizopita zinasema kuwa jenerali huyo sasa anashikilia zaidi ya theluthi mbili ya eneo lote la Libya, lakini inaelekea hana subira ya kuteka maeneo mapana yaliyobaki kabla ya kuanza kuuzingira mji mkuu.

Ni kanuni ya kawaida inayotumika katika 'vita ya muda mrefu' kubadili kabisa mfumo wa utawala ndani ya nchi kwa harakati ya kutwaa silaha.

Ukiangalia kinachoandikwa katika mitandao, tayari unapata picha Jenerali Haftar ni nani hasa, kwani alikuwa sehemu ya jeshi (makamanda) wa kiongozi wa zamani wa Libya, Kanali Muammar Gaddafi.

Wakati wa uasi ulioanzia jiji la Benghazi Mashariki ya nchi hiyo akawa pamoja na waasi, na baadhi ya wanaomchukia katika mitandao wanasema yeye ndiye alimwua Gaddafi, ambayo ina maana alikuwa kamanda wa vikosi vilivyomsaka Gaddafi.

Hata hivyo, si yeye au kamanda mwingine wa huko aliyemmaliza Gaddafi ila ndege za kivita za Ufaransa.

Kilichoelezwa wakati huo kuwa kilitokea ni kuwa Kanali Gaddafi, hasa kwa kupitia mwanae Saif al-Islam, alikuwa amepeleka mkondo wa vifaru kwenda kumaliza uasi jijini Benghazi, na ilihofiwa kuwa kama mkondo huo ungewasili kungekuwa na mauaji ya kutisha.

Kwa hali hiyo, wakati bado mkutano wa umoja wa kujihami wa nchi za Magharibi (NATO) bado ukiendelea London nchini Uingereza, Ufaransa ikatuma ndege zake za kivita (Rafale) kwenda kuangamiza mkondo wa vifaru ili usifike karibu na Benghazi.

Ikawa sasa ni watu wa Gaddafi kukamatwa na nchi kuparaganyika, baada ya Gaddafi mwenyewe kuuawa katika handaki alipojificha msafara uliposhambuliwa angani akiwa anajitahidi kufika mpaka wa Niger, Kusini ya nchi hiyo, kwa mujibu wa nyakati hizo.

Kuanzia hapo hadi kufikia hapa ni historia ndefu, lakini la msingi ni kuwa makundi ambayo yalifaidika na mabadiliko nchini Libya yaliendana na mazingira ya kisiasa eneo la Mashariki ya Kati wakati huo.

Haikuwa jambo la kushangaza kuwa makundi ya kisiasa yaliyojiinua katika kipindi hicho yakawa ya wale ambao katika ukanda huo wanaitwa ni wanademokrasia, yaani wanapenda sana kutumia nyenzo ya demokrasia kufikia malengo ya kiharakati ambayo katu hawajawahi kuyakana.

Ndiyo mwelekeo wa Rais Recep Tayyip Erdogan wa Uturuki na aliyekuwa rais nchini Misri, hayati Mohammed Mursi, akatawala mwaka mmoja, akapinduliwa.

Invyoelekea ni kuwa serikali iliyoko madarakani nchini Libya ilikuwa ikijiambatanisha na matumaini hayo ya demokrasia ya kimapinduzi kwa mfano ilivyo Iran, Misri wakati wa uchaguzi wa 2011 au nchini Tunisia ambako chama chenye mwelekeo wa kiharakati kiko madarakani.

Ila hakuna uharibifu mkubwa, kama ilivyo Uturuki, kwani jamii hizo zina mahusiano ya muda mrefu na nchi za Magharibi. Na licha ya uanaharakati kisiasa, jamii hizo hazina udhati wa kidini.

Kwa maana hiyo kulikuwa na 'kukuna vichwa' kati ya nchi zinazopakana na Libya jawabu liwe nini, wakati nchi za Ulaya na mashirika ya Umoja wa Mataifa kimsingi hazina ugomvi na siasa za kiharakati mradi zisivuke mipaka.

Bunge la Misri wakati wa Mursi lilivuka mpaka na kuanzisha tena maandamano, baada ya kupitisha sheria kuwa binti wa miaka 12 anaweza kuolewa kwa ruhusa ya baba yake – yaani aamue kama hakuna tatizo lolote.

Maandamano yaliposhona jeshi likapata nafasi kuingilia kati, kwani halitaki kamwe siasa za kiharakati, n.k.

Kutokana na uwepo wa makundi tofauti ya kijeshi nchini Libya yasiyokuwa na utawala rasmi wa kitaifa, na uwezekano wa kuingiza silaha kiasi jemadari yeyote anachotaka, na kupewa fedha na nchi zisizotaka kuona wanaharakati wako madarakani, haikuwa vigumu kwa Jenerali Haftar kujiimarisha.

Kulikuwa na muda wa kutosha kwani utawala wa Libya haujawahi kutengemaa, ni kama ilivyo Somalia, tofauti ikiwa ni kwa upande wa rasilimali, kuwa Libya ni tajiri wa mafuta na kuna fedha nyingi zinazoingia au kuizunguka nchi hiyo.

Haiwezi kukaa imeparaganyika bila mwelekeo kama Somalia au kwa upande mwingine Afghanistan; na ndiyo anapoingia Haftar.

Wapinzani wa Jenerali Haftar hawana shaka yoyote katika mitandao huyu ni mtu gani au anasimamia nini hasa, kwani hakuna kingine ila lugha ya wanaharakati ambao kimsingi ni dirisha la kiharakati la mapambano yenye msingi wa kitamaduni.

Ni kupinga jamii za Mashariki ya Kati kufuata mwenendo wa kijamii wa nchi za Magharibi, hata kama inabidi kutumia nguvu za ziada kuhakikisha kuwa jamii hizo zinabakia katika uelekeo wake wa jadi.

Kwa njia hiyo Jenerali Haftar akawa chaguo la tawala za kiimla zinazotaka mabadliko, kuondoa mbali harakati.

Ukiangalia katika kurasa tofauti unakuta masikitiko makubwa ya wachangiaji ambao kwa ujumla wao ni wanaharakati wa jadi hiyo na chuki hiyo ya nchi za Magharibi, tofauti na nchi za Kusini ya jangwa la Sahara ambazo zimeathiriwa kwa undani na utamaduni wa Magharibi.



Jenerali Khalifa Haftar.
**PICHA: MTANDAO**

> Wakati wa uasi ulioanzia jiji la Benghazi Mashariki ya nchi hiyo akawa pamoja na waasi, na baadhi ya wanaomchukia katika mitandao wanasema yeye ndiye alimwua Gaddafi, ambayo ina maana alikuwa kamanda wa vikosi vilivyomsaka Gaddafi.

Harakati katika eneo hili ni kupigania uhuru wa mtu binafsi na demokrasia, siyo kutetea jadi iliyoingiliwa na nchi za Magharibi.

Kwa maana hiyo wanaharakati walio na makao nchi za nje, siyo Libya kwenyewe wanamkaanga Haftar kila kukicha ni kibaraka wa nchi za Magharibi, kifaa cha CIA.

Moja ya mashambulio makubwa ambayo Jenerali Haftar amefanya hivi karibuni ilikuwa ni kupiga kambi ya kuhifadhi wakimbizi waliookolewa baharini na wasiojulikana wapelekwe wapi.

Baadhi ya taarifa zenye uhusiano na kundi la Jenerali Haftar zilisema kulikuwa na depot (ghala) ya silaha zinazotumiwa na jeshi la serikali rasmi ya Libya, hivyo ikaonekana kuwa kwa vile kambi hiyo ilikuwa karibu na depot ilipigwa kimakosa.

Bado suala hilo halijamalizika kwani hakuna mazingira Libya ya kufanya uchunguzi halisi na kujua dhamira halisi ya kupiga mabomu.

Ukiangalia kwa jinsi vita inavyokwenda nchini Libya hakuna shaka kuwa kwa mwenendo uliopo ni Jenerali Haftar anayeelekea kushinda, kwani nje ya shauku ya kuteka Tripoli kwa haraka, kimsingi ameshika nchi karibu yote.

Kutokana na kuungwa mkono na washirika wa karibu wa Marekani barani Ulaya na Mashariki ya Kati, hata wasio washirika wa karibu kama Ufaransa, siyo rahisi kuona ni kwa njia gani serikali ya Tripoli inajikusanya, ianzishe mwamko mpya nchini Libya na kurudisha nyuma majeshi ya Jenerali Haftar hadi yaishilie. Hawana pumzi hiyo.

Utawala wa Tripoli ulikuwa ni tokeo la harakati ya kumwondoa Gaddafi ambayo ilikamilika kwa hatua ya vikosi vya Ufaransa kumsambaratisha Gaddafi, na hapakuwa na mkutano halisi wa kikatiba wa kupambanua hali ya baadaye ya nchi hiyo kwani vita haijawahi kusimama tangu aanguke Gaddafi.

Kwa maana hiyo ni suala hilo ambalo sasa linamalizwa kwa mbinu zile zile za awali, kuwa serikali iliyopo Tripoli ni kama vile ina baraka za wafuasi wa Gaddafi, wanaharakati wanaojipambanua kwa kutokuwa tayari kutoa mafuta kwa bei poa kwa nchi za Magharibi wakati bei inajipanga yenyewe kupitia mivutano ya wingi na uhaba katika soko la dunia, tena kwa aina za mafuta, si bei moja kwa mafuta ghafi yote. Ni kukosa tu la kuongea dhidi ya Jenerali Haftar.

UCHAMBUZI

# TUJIKUMBUSHE YAKUBU GOWON

Na Raphael Kibiriti

ALIKUWA kiongozi wa tatu wa taifa la Nigeria katika serikali ya Shirikisho iliyoongozwa na Jeshi la Nigeria, kipindi cha kati ya mwaka 1966-1975. Jenerali Yakubu Gowon alizaliwa Oktoba 19, 1934.

Aliingia madarakani, baada ya kufanya mapinduzi ya kijeshi dhidi ya Serikali iliyokuwa ikiongozwa na Johnson Aguiyi-Ironsi.

Wakati wa utawala wake, serikali ya ilifanikiwa kusitisha vita vya wenyewe kwa wenyewe katika eneo la Biafra, ambavyo vilianza mwaka 1967 hadi mwaka 1970.

**MAISHA YAKE**

Gowon ni wa kabila la Ngas (Angas) la Lur, lililoko katika kijiji kidogo chini ya Serikali ya mitaa ya Kanke katika Jimbo la 'Plateau'.

Wazazi wake, walihamia Wusasa, mji katika eneo la Zaria, wakiwa watumishi wa Kanisa la Mtume 'Church Missionary Society' (CMS), wakati Gowon mdogo.

Baba yake alijawa na faraja, baada ya kugundua kuwa siku aliyomuoa mkewe ndiyo siku ambayo aliyekuwa Malkia mtarajiwa Elizabeth wa Uingereza aliolewa na Mfalme mtarajiwa King George VI.

Gowon ni mzaliwa wa sita kati ya watoto 11 na alipata malezi ya awali Zaria, ambako ndiko alipata elimu yake ya msingi.

Akiwa shuleni, Gowon alipenda michezo, na alikuwa mwanariadha mzuri, pia golikipa wa kutegemewa wa timu ya mpira wa miguu ya shule yao.

Aidha, alikuwa mahiri wa kurusha mkuki na mkimbiaji wa kutegemewa wa mbio ndefu.

Aliwahi kuvunja rekodi ya kukimbia umbali wa maili moja, mwaka wa kwanza wa masomo yake ya chuo kikuu.

Aidha, alikuwa kiongozi wa mchezo wa ngumi.

**KUINGIA KATIKA SIASA**

Alijiunga na Jeshi la Nigeria mwaka 1954 na ilipofika Oktoba 19, 1955, alipata kamisheni ndani ya Jeshi hilo katika cheo cha Luteni Usu. Vilevile siku hiyo ilikuwa ni sherehe yake ya kutimiza miaka 21 ya kuzaliwa kwake.

Alifanya mafunzo ya kijeshi katika Chuo cha Unadhimu cha kijeshi cha Sandhurst, nchini Uingereza, kati ya 1955 na 1956.

Aidha, mwaka 1962, aliendelea na mafunzo katika Chuo cha Camberley nchini humo kabla ya kwenda katika chuo cha Joint Staff, mwaka 1965.

Gowon alishiriki katika operesheni ya Walinzi wa Amani wa Umoja wa Mataifa nchini Congo (sasa DRC), katika awamu zote mbili kuanzia mwaka 1960 hadi mwaka 1961, na nyingine mwaka 1963.

**MADARAKA**

Mwaka 1966, alikuwa Mkuu wa Kikosi, akiwa na cheo cha Luteni Kanali.

Hadi wakati huo, Gowon hakujihusisha kwa hali yoyote na masuala ya siasa hadi pale mambo yalipoanza kwenda mrama nchini humo hali iliyomlazimu ajiingize katika majukumu ya uongozi.

Akiwa mtu asiyefungamana na upande wa makabila ya Hausa au Fulani, hakuweka mbele pia suala



Jenerali Yakubu Gowon. **PICHA: MTANDAO**

la uzawa wala la itikadi ya kidini.

Na ndiyo maana ikawa rahisi kwake kuchaguliwa kuwa kiongozi wa taifa ambalo wakati huo lilikuwa kwenye mgawanyiko na mvutano mkubwa wa u-dini na u-kabila.

Januari 1966, aliteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la nchi hiyo, akiwa na umri mdogo wa miaka 32.

Hiyo ilijitokeza kutokana na mapinduzi ya kijeshi yaliyofanikishwa na wanajeshi wa vyeo vya chini, wengi wao wakiwa wa kabila la Igbo chini ya uongozi wa Meja Chukwuma Kaduna Nzeogwu, ambaye ndiye hasa aliyefanikisha kuiangusha serikali ya kiraia.

Wakati wa harakati za mapinduzi hayo, viongozi wengi wenye asili ya Kaskazini na Magharibi waliuawa, wakiwemo Sir Abubakar Tafawa Balewa, Waziri Mkuu Sir Ahmadu Bello, Sardauna wa Sokoto, aliyekuwa Waziri Mkuu wa eneo la Kaskazini, pamoja na Samuel Akintola, Waziri Mkuu wa Jimbo la Magharibi.

Wengine ni Luteni Kanali Arthur Unegbe na viongozi wengine wengi.

Sababu kubwa zilizosababisha mapinduzi hayo ni kukosekana kwa mwakilishi kutoka Kaskazini kwenye uongozi wa kitaifa, kitu ambacho kilikuwa ni doa kwani kwa mara ya mwisho kwa kiongozi kuongoza kutoka eneo hilo, ilikuwa mwaka 1919.

Aidha, sababu nyingine ilikuwa ni kushindwa kwa Meja Jenerali Johnson Aguiyi-Ironsi (ambaye alikuwa mkuu wa nchi wakati wa mapinduzi ya Januari 1966 na Gowon akiwa Mnadhimu Mkuu wake), kutanzua madai na malalamiko ya wananchi wa Kaskazini.

Ikumbukwe kuwa mapinduzi hayo yaliungwa mkono na wananchi wa Jimbo la Mashariki, pamoja na waliokuwa wa mlengo wa kushoto.

Baadaye ikaja amri namba 34 ya Ironsi, ambayo ilitoa mapendekezo ya kufuta utaratibu wa serikali ya Shirikisho kwa ajili ya kupata serikali moja.

Hatua hiyo ilikuwa ikipiganiwa na wananchi wengi, hasa wale wa Kusini mwa nchi hiyo, wengi kutoka kabila la Igbo, ambalo ndilo lenye nguvu zaidi huko.

Hali hiyo inawezekana kabisa ilitafsiriwa vibaya na watu wa Kusini, (na hasa wa-Ibo) katika kuchukua madaraka ya nchi kwenye ngazi zote za uongozi.

Wananchi wa Kaskazini walikuwa wakiburuzwa na maamuzi ya watu wa Magharibi na Mashariki katika nyanja za elimu, na hilo lilitokea kwa sababu wao walijikita zaidi kwenye itikadi za kidini ambazo awali zilisusia elimu iliyokuwa ikitolewa na nchi za Magharibi.

Wakati huo huo, wananchi wengi wa Mashariki walikuwa tayari wameajiriwa katika sekta mbalimbali ndani ya serikali ya Shirikisho.

Ilipofika Julai 29, 1966, wakati Ironsi akiwa katika nyumba ya serikali huko Ibadan, majeshi kutoka Kaskazini ambayo yalikuwa yakiongozwa na Meja Theophilus Danjuma, pamoja na Kapteni Martin Adamu, waliivamia nyumba aliyokuwa akiishi na mwenyeji wake Luteni Kanali Adekunle Fajuyi.

Katika uvamizi huo waliwavua nguo na kuwapiga na mwishowe wakawaua kwa risasi.

Majeshi mengine toka Kaskazini, chini ya Luteni Kanali Murtala Mohammed, kiongozi halisi aliyepanga mapinduzi na baadaye kuchukua madaraka ya kuongoza nchi toka kwa Yakubu Gowon, yaliuteka uwanja wa ndege wa Ikeja, jijini Lagos.

Wengi wa maofisa kutoka kabila la Igbo na wachache wa kutoka Mashariki waliuawa wakati wa mapinduzi hayo.

> “ Sababu kubwa zilizosababisha mapinduzi hayo ni kukosekana kwa mwakilishi kutoka Kaskazini kwenye uongozi wa kitaifa, kitu ambacho kilikuwa ni doa kwani kwa mara ya mwisho kwa kiongozi kuongoza kutoka eneo hilo, ilikuwa mwaka 1919.

Na Anil Kija

# Mbunge aliyeng'ong'wa na Trump aipania Israel, haigusi Somalia



Mbunge kutoka chama cha Democrat kutoka Jimbo la Minnesota nchini Marekani aliye mpinzani wa Rais Donald Trump, Ihlan Abdullah Omar (katikati) akiwa pamoja na Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi. **PICHA: MTANDAO**

MJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wa jimbo la Minnesota, Ihlan Abdullah Omar mwenye asili ya Somalia amepata sifa duniani kote kwa majibizano na Rais Donald Tump kwanza kuhusu utendaji kazi wa rais huyo wa Marekani, halafu kuhusika na masuala kadhaa ya nchi za nje.

Baada ya Rais Trump kumsuta kuwa 'ana bahati kuwa hapo alipo' kwani alizaliwa Mogadishu mwezi Oktoba mwaka 1982, na kumtaka arudi kwao, Ihlan Omar ameelekeza macho yake kwingine. Hana kazi na Somalia ambayo bado ana uraia wake wa kuzaliwa; anajielekeza Israel.

Wakati nchi kama Kenya na hata Tanzania zinazoelewa kwa karibu hatari na madhara ya ugaidi unaotokea Somalia, kuwa endapo yuko mbunge Marekani mwenye asili ya nchi hiyo anaweza kutoa mchango adhimu kutatua suala hilo, matarajio hayo yameyeyuka.

Kutatua suala la Somalia siyo jambo linaloleta sifa kwa mbunge mwenye asili ya Afrika nchini Marekani ila kuongezea katika sauti lukuki za kutaka haki kwa watu wa Palestina, na kuongeza chuki dhidi ya Israel na Wayahudi kwa jumla. Ihlan Omar ameamua kutupa nyavu zake huko, kwani kuna tija endelevu.

Mbunge huyo amependekeza azimio la Bunge linaloweza kupitishwa kuwa sheria likipata kura za kutosha, kusisitiza vikwazo dhidi ya Israel, kutotembelewa na kukwepa bidhaa au huduma zake, na pia kuondolewa kwa mitaji kutoka Marekani (na kwingineko duniani) nchini Israel kutokana na kuikalia kwa mabavu ardhi ya Palestina.

Azimio au muswada huo wa sheria pia una wapendekezaji wenza, ambao ni Rashida Tlaib (mchakazwaji mwingine katika 'tweet' za Trump) na mbunge mwenzao, John Lewis.

Muswada huo umejikita katika rekebisho la kwanza la Katiba ya Marekani; linawawezesha raia wa Marekani kutetea haki za binadamu ndani na nje.

Wachunguzi wa habari wanasema kuwa licha ya kuwa muswada huo hauhitaji kampeni ya BDS (kususia, kuondoa mitaji na kuweka vikwazo dhidi ya Israel) kwa jina, unaonekana ni jibu kwa muswada mwingine uliopendekezwa kupinga kampeni hiyo dhidi ya Israel.

Ni kazi ambayo kwa kiasi kikubwa inaendeshwa na watu wenye asili ya Kiyahudi nchini Marekani.

Hivyo wabunge wanne wanawake vijana, watatu wakiwa wamezaliwa Marekani lakini wana asili ya nje, pamoja na Ihlan, wanaunganisha ajenda tata za utendaji wa Trump kwa upande mmoja, halafu Israel.

Wabunge hao vijana walivuka mpaka kwa kutoa mwito kuwa Rais Trump ashtakiwe katika Bunge la Marekani (yaani kwa azimio la pamoja la mabaraza yote mawili, Wawakilishi na Senate kuwa anafaa kufikishwa mahakamani, hali itakayomlazimisha ajiuzulu). Ni suala ambalo limezuka miezi ya karibuni kutokana na uchunguzi wa mwendesha mashtaka maalum Robert Mueller iliyohoji udhati wa Rais Trump kuona uchunguzi wa kuingiliwa uchaguzi mkuu 2016 unaendeshwa vyema kufikia tamati sahihi.

Wabunge wakahisi anaweza kushtakiwa kwa suala hilo, lakini wabunge hao wanawake vijana wanakwenda mbali, wanaona utawala wake ni balaa, uozo mtupu, rushwa na uzembe usio kifani. Trump alikasirika, akasema 'wanakotoka kumeoza.'

Hivi sasa wabunge hao wanaonekana kuwa vinara wa kampeni ya wazi ya kujenga chuki dhidi ya Israel, na pendekezo lao linaonekana kutaka kuziba mdomo watetezi wa Israel dhidi ya wakinzani wake, kufanya kampeni ya BDS iwe ni sehemu ya Katiba ya Marekani, isipingwe.

Hata wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa chama cha Democratic hawatazamii kuwa muswada huo wa kina Ihlan utaenda mbali katika ngazi ya kamati, na wajumbe wa Democratic ndio wenye viti zaidi Baraza la Wawakilishi.

Mbunge Brad Sherman (Democratic, California) alisema hana wasiwasi na kampeni ya BDS katika ngazi ya uchumi, ila kuvuruga sura ya Israel.

Mbunge Lee Zeldin (Republican, New York) ambaye alizungumza bungeni mara baada ya Ihlan Omar kuwasilisha pendekezo lake, alisema harakati ya BDS haijajitenganisha kwa uwazi na kundi la Hamas, akikumbusha kuwa kundi hilo linatumia wanawake na watoto kama ngao.

"Wabunge wakahisi anaweza kushtakiwa kwa suala hilo, lakini wabunge hao wanawake vijana wanakwenda mbali, wanaona utawala wake ni balaa, uozo mtupu, rushwa na uzembe usio kifani. Trump alikasirika, akasema 'wanakotoka kumeoza.'

Alieleza kwa udani hatari kwa Israel inayotokana na makundi ya kigaidi kama Hezbollah nchini Lebanon, Hamas katika ukanda wa Gaza na mengineyo. Akasisitiza mshikamano zaidi na Israel.

Alikataa hoja kuwa tatizo lote Mashariki ya Kati ni kukalia Ukingo wa Magharibi kwa mabavu, akikumbusha kuwa mwaka 2008 Israel ilikuwa tayari kuachia asilimia 93 ya eneo hilo kwa Palestina.

Israel inaliita Judea na Samaria na baadhi wanapinga kuwa linakaliwa kwa mabavu, na tayari sheria inakamilishwa kuunganisha eneo kubwa la Ukingo wa Magharibi na Israel kama eneo halisi la nchi hiyo, kuondoa mjadala kuwa walowezi wa Kiyahudi waondolewe huko.

Wapalestina miaka yote wametaka eneo lote hilo pamoja na Yerusalemu Mashariki kama mji wao mkuu, jambo ambalo halikubaliki kwa Israel, kuwa wakishafika hapo, watainyonga Israel.

Wachunguzi wa habari walisema kuwa hatua ya wabunge hao wanaharakati ilitokana na kuwasilishwa miswada na maazimio matano na Kamati ya Mambo ya Nje ya Baraza la Wawakilishi kuunga mkono Israel.

Mapendekezo matatu yalikuwa ni kutafuta azimio la Bunge na mawili ni miswada ya sheria ya kuweka adhabu kwa wanaounga mkono Hamas na kuboresha misaada ya ulinzi na usalama kwa Israel. Azimio la 246 la Baraza, lililopendekezwa na Bradley Schneider (Democratic, Illinois) linapinga harakati ya BDS, likiainisha vitendo vinavyolenga "kampuni za Marekani zinazofanya biashara halali chini ya sheria ya Marekani, na juhudi zote za kuondoa uhalali wa kuwepo kwa Dola ya Israel."

Pendekezo linasisitiza pia mazungumzo kama njia ya kutatua mzozo wa Palestina wakati Mamlaka ya Palestina haiongei na utawala wa Trump.

Liko pendekezo jingine linaloendana kiasi fulani na hatua za kina Ihlan Omar, la mbunge Alan Lowenthal (Democratic, California) linalosema kuwa ni kuundwa kwa nchi mbili tofauti katika eneo hilo ndiyo kutawezesha Israel kudumu na kuwa salama kama taifa la Wayahudi, kwa kuzingatia madai halali ya Wapalestina ya kuwa na nchi yao wenyewe.

Azimio linapinga hali ya sasa ya sera ya Marekani katika eneo hilo, kuwa Marekani imetoa pendekezo (kupitia kwa mshauri wa Rais Trump, mkwe Jared Kushner katika mkutano wa Bahrain mwezi uliopita) ambalo halina dhamira ya kuundwa kwa nchi mbili kama lengo lake.

Lilicharura pia hali ya kuunga mkono au kudengulia hatua za kumega maeneo (Ukingo wa Magharibi) kinyume cha muafaka wa kimataifa kuhusu utatuzi wa suala la Palestina.

Azimio hilo linasema kuwa kwa mwelekeo huo, hapatakuwa na uwezekano wa kufikia suluhu ya suala hilo kwa amani milele.



# Daktari ashangaa kifafa kuhusishwa na ushirikina

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, Dk. Khamis Ally, ameishauri jamii kuachana na tabia ya kuhusisha ugonjwa wa kifafa na imani za kishirikina na badala yake wafike kwenye vituo vya afya ili kupata matibabu.

Dk. Ally alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wanawake wa mkoa wa Mbeya ambao walitembelea hospitali hiyo kwa lengo la kuzungumza na kinamama wajawazito na waliojifungua.

**Chama kinatambua mchango wao na kitaendelea kutoa ushirikiano na kuwasihi kuendelea kuwahudumia wagonjwa kwa moyo wa upendo.**

Alisema dhana ya kuhusisha ugonjwa wa kifafa na imani za kishirikiana, imechangia kwa kiasi kikubwa watu kupoteza maisha na wengine kupelekwa hospitalini wakiwa na hali mbaya.

"Kifafa ni ugonjwa ambao unasababishwa na vitu mbalimbali ikiwamo ulevi wa kupindukia, matumizi ya dawa za kulevya na mtoto kuminywa kichwa wakati mama anajifungua, hivyo hautokani na imani za kishirikina," alisema.

Naye Muuguzi Mkuu wa Hospitali hiyo, Stella Mhina, aliwashauri wananchi hususani vijana kuacha tabia ya unywaji wa pombe kupita kiasi kwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayosababisha ugonjwa wa kifafa.

Alisema baadhi ya wagonjwa wanaotibiwa kifafa hospitalini hapo, chanzo kikubwa ni ulevi kutokana na mtu kulewa hadi ubongo kuvurugika na kupata ugonjwa huo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, alipongeza mafanikio yaliyopatikana katika hospitali hiyo ikiwamo ukarabati wa majengo kwenye wodi mbalimbali za wagonjwa.

Alisema chama kinatambua mchango wao na kitaendelea kutoa ushirikiano na kuwasihi kuendelea kuwahudumia wagonjwa kwa moyo wa upendo.



Vijana wakazi wa Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam, wakitoka kutafuta kuni kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia majumbani jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafundwa sheria za usalama barabarani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAISLAMU jijini Mbeya, wamekumbushwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kujiepusha na ajali za mara kwa mara ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya Watanzania wengi.

Hayo yalisemwa jana na Sheikh wa Msikiti wa Baraa Ibn Aazb ulioko Kata ya Isanga jijini hapa, Dourmohamed Issa, wakati wa Sala ya Ijumaa iliyofanyika mwishoni mwa wiki.

Sheikh Issa alisema licha ya kuhubiria waumini kufuata Maandiko Matakatifu, suala la kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani ni muhimu kwa ajili ya kuokoa maisha yao.

Alisema Waislamu wanatakiwa kuwa kielelezo cha kutii sheria bila shuruti kwa kuhakikisha wanakidhi vigezo vya matumizi ya vyombo ya moto barabarani.

"Lazima tuwahubirie waumini wetu masuala ya kuzingatia sheria za usalama barabarani ili wasipate vilema au kupoteza maisha hatuna budi kuunga mkono jitihada za serikali katika vita dhidi ya ajali za barabarani," alisema Sheikh Issah.

Aliongeza kuwa madereva wanatakiwa kuzingatia sheria kwa kuhakikisha wanatumia vyombo vya moto wakiwa na leseni badala ya kuendesha holela.

Alisema madereva kuwa na elimu ya kuendesha vyombo vya moto kabla ya kutumia huku akiwashauri watembea kwa miguu kuheshimu alama zilizowekwa barabarani.

"Madereva wasio na leseni waende vyuoni wakasome ili waongeze ujuzi na kupata cheti cha kuhitimu hii itasaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza barabarani," alisema Sheikh Issa.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwataka madereva wote hususani wanaotumia magari ya abiria kuacha tabia ya kupakia abiria wanaozidi idadi ya viti.

Alisema tabia ya madereva kuzidisha abiria kwenye magari inaweza kuleta madhara makubwa pindi inapotokea hitilafu kwenye chombo cha usafiri na kusisitiza kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kuwatoza faini wale watakaokaidi utaratibu huo.

# Wafurahia maandalizi ya Nanenane

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

BAADHI ya wafanyabiashara katika Jiji la Mbeya, wamepongeza hatua za maandalizi ya sherehe za Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo yanatarajiwa kuanza kesho na kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanafanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Allyrich Mulungu ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Allyrich Sanaa Group inayojihusisha na uchapishaji na usambazaji wa mabango, matangazo na kalenda, alisema sherehe za mwaka huu zimefana kulinganisha na miaka ya nyuma.

Mulungu alisema serikali imejitahidi kuboresha miundombinu ya barabara, maji na umeme hali ambayo imeshawishi kuvutia wafanyabiashara wengi kushiriki maonyesho ya mwaka huu.

"Tumeyafurahia maonyesho ya mwaka huu kwa sababu serikali imeboresha miundombinu muhimu kwa ajili ya kufanya biashara zetu ambayo kipindi cha nyuma ilikuwa kikwazo kwetu. Naamini wakulima na wananchi wengine watafurahia na kujifunza vingi kutoka kwetu," alisema Mulungu.

Aliwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye maonyesho hayo ili kujifunza masuala mbalimbali ya utengenezaji bidhaa na kuwahakikishia kupewa elimu ya ujasiriamali bure.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema maonyesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, yamefungua wigo mpana kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kutangaza na kuuza bidhaa zao.

Alisema wakuu wote wa mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini watashiriki na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mdeme, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa maonyesho hayo.

**Tumeyafurahia maonyesho ya mwaka huu kwa sababu serikali imeboresha miundombinu muhimu kwa ajili ya kufanya biashara zetu ambayo kipindi cha nyuma ilikuwa kikwazo kwetu. Naamini wakulima na wananchi wengine watafurahia na kujifunza vingi kutoka kwetu.**





# Watamba kuleta mapinduzi kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya kimataifa ya mapinduzi ya kijani barani Afrika (Agra) imeingia makubaliano na Serikali ya Tanzania ili kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo husUsan kwenye mazao ya kimkakati kwa ajili ya viwanda.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana baada ya mkutano ulioshirikisha mawaziri watatu wa Tanzania na ujumbe wa taasisi hiyo ukiongozwa na Rais wake, Dk. Agnes Kalibata.

Timu ya Tanzania iliongozwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa na Manaibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Omar Mgumba.

Akizungumza baada ya kuingia makubaliano hayo, Waziri Bashungwa alisema utekelezaji wake umegawanywa kwa vipindi vya muda mfupi na mrefu na utaanza kwa kuimarisha na kuzalisha kilimo kwenye mazao manne.

**Wameafikiana na taasisi hiyo kuangalia namna ya kusukuma mbele ASDP ll na pia kuwezesha mazao hayo kutumika katika viwanda vilivyopo nchini.**

"Kwa kipindi cha muda mfupi, tumekubaliana kuanza na mazao manne ikiwamo alizeti, mahindi, mpunga na maharage ya soya ambayo kwa msimu mmoja tunaweza kupata mavuno ambayo yatakwenda kwenye viwanda,"alisema.

Alibainisha kuwa mkakati wa serikali ni kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula nje ya nchi ambapo zao la alizeti ndiyo lina fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa viwanda nchini.

Waziri huyo alisema wameafikiana na taasisi hiyo kuangalia namna ya kusukuma mbele ASDP ll na pia kuwezesha mazao hayo kutumika katika viwanda vilivyopo nchini.


Dk. Kalibata kwa upande wake, aliipongeza serikali kwa kuweka utaratibu mzuri kati ya wakulima, serikali na sekta binafsi. Alisema wanalenga kuwezesha mabadiliko katika kilimo na kuwakomboa wakulima kwa kuongeza tija na kuipeleka Tanzania katika uchumi wa viwanda.

Alisema taasisi hiyo imetoa ruzuku ya Dola za Marekani 600,000 kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa ASDP ll kwa kusaidia serikali katika masuala ya kiufundi yanayohusu programu mbalimbali za kilimo.

Naibu Waziri Bashe alisema mazao ya chakula ndiyo biashara kubwa duniani kuliko jambo jingine lolote.

"Tumejadiliana namna ambavyo sekta binafsi itaingia kwenye uzalishaji na wao Agra kusaidia wanaozalisha mbegu ili kuweza kufikia malengo hayo, sisi kama Wizara ya Kilimo tunafanya pamoja na Wizara ya Viwanda ili kuondokana na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakumba wakulima,"alisema.

Aliongeza kuwa kumekuwa na changamoto ya masoko na wameijadili na kuangalia namna ambavyo fedha zinazotolewa na wafadhili kwenye sekta ya kilimo kuwa na uratibu wa pamoja na kufahamika malengo yake ili kupata matokeo yanayotarajiwa.



Mwenyekiti wa Kampuni ya Sekta ya Ulinzi Binafsi (TSIA) Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, akizungumza na baadhi ya askari wa kutoka sekta hiyo walipokutana kufanya mazoezi ya pamoja na kujengeana mbinu shirikishi za kiulinzi, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Kongwa waomba chakula bei nafuu

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

WAKAZI wa Kongwa wameiomba Serikali kuwapatia msaada wa chakula cha bei nafuu kutokana na mavuno ya mwaka huu kutokuwa mazuri, hivyo kukabiliwa na upungufu wa chakula.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wilayani humo iliyokuwa na lengo la kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi, wakazi hao walisema wanakabiliwa na hali ngumu kutokana na ukame.

Mkazi wa Kijiji cha Makawa, Amon Lukwa, alisema wana hali ngumu kwa kuwa mvua haikunyesha vya kutosha na mavuno yao si mazuri.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, tatizo tulilonalo ni ukame, kuna upungufu mkubwa wa chakula, tumelima lakini mavuno hakuna, serikali inatusaidiaje ili angalau tupate chakula cha kununua kwa bei rahisi," aliomba.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Omary Mkulo, alisema tayari wameshapokea maelekezo kutoka serikalini ya kufanya tathimini ya hali ya chakula.

"Maelekezo hayo tumeshayapokea tunaendelea na tathimini kujua kuna upungufu wa kiasi gani na katika maeneo yapi na mara tukikamilisha tutawasilisha serikalini ili tupate chakula cha bei nafuu," Dk. Mkulo alisema.

Kwa upande wake, Dk. Mahenge aliwataka wananchi kuwa na subira wakati halmashauri inaendelea kufanya tathimini na kuhimiza tathimini hiyo kufanyika kwa haraka.

"Ndugu zangu, mmesikia tathimini inafanywa ili kujua upungufu upo kwa kiasi gani, kwenye kijiji gani na kina nani wanahitaji huo msaada, hivyo tusubiri tathimini itakamilika mapema," Dk. Mahenge alisema.

Aliwataka wananchi kubadilika kwa kulima mazao yanayostahimili ukame ili tatizo kama hilo lisiweze kutokea tena.

"Ni lazima tukubali kubadilika kulingana na hali ya hewa inavyokwenda, yapo mazao ikinyesha mvua kidogo yanaweza kustawi, tubadilike, tusikubali kushindwa hata siku moja,"alisema.

# Kampuni za ulinzi zataka mkakati kumaliza uhalifu

**Ibrahim Joseph,** DODOMA

KAMPUNI binafsi za ulinzi nchini (TSIA) zimeshauriwa kuweka utamaduni wa kubadilishana mbinu za ulinzi kwa askari wao ili kukabiliana na uhalifu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kampuni hizo Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, wakati askari wa kampuni hizo wakifanya mazoezi ya pamoja na kushirikishana mbinu zaidi za kiulinzi jijini Dodoma.

Kayombo alisema kuna haja kampuni hizo kubadilishana mbinu za kiulinzi kwa askari wake na kuwapo na mafunzo ya mara kwa mara.

"Siku hizi kuna aina nyingi za kiuhalifu na wizi, hivyo askari wetu wanatakiwa kujengewa mbinu za mafunzo na mbinu mpya za kupambana na aina za matukio kama hayo yanayoweza kujitokeza kwenye maeneo yetu ya kazi," alishauri.

Alisema mafunzo hayo na mazoezi hufanyika kila mwisho wa mwezi na hushirikisha kampuni za ulinzi zaidi ya 20.

Mwenyekiti huyo alisema katika mafunzo hayo ya mwezi huu, jumla ya askari 381 walishiriki na walianza mazoezi hayo ya pamoja majira ya saa moja asubuhi wakipita kwenye baadhi ya mitaa ya Jiji la Dodoma.

Alibainisha kuwa mazoezi hayo yanalenga kuwajengea ukakamavu askari wao ili kupambana na matukio ya kiuhalifu pindi yanapojitokeza kwenye maeneo yao ya kazi.

Alisema sekta hiyo ipo chini ya Jeshi la Polisi na wamekuwa wakipata ushirikiano mkubwa katika kupewa mafunzo ya kikazi pamoja na silaha.

Meneja wa Kampuni ya Ulinzi ya SGA, Issa Samadu, alisema utaratibu huo unasaidia kudumisha umoja wao ambao umekuwa na faida kubwa ya kushirikishana mbinu ya kusimamia kampuni pamoja na askari wengi kujuana.

Samadu alisema kutokana na umoja huo, wamekuwa wakipeana taarifa za namna ya kuwaajiri askari wapya ili kuepuka kuchukua wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu.

"Hapa Dodoma tumekuwa na utaratibu wa tupeana taarifa au kuuliza kwa kampuni nyingine kabla ya kumwajiri askari mpya," alisema.



# RC Ayoub apongeza wanafunzi kujitolea

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema ujumbe wa wanafunzi kutoka nje ya nchi na kujitolea katika shughuli za kijamii, unaunga mkono juhudi za serikali za kuondoa changamoto za sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu.

Ayoub alisema hayo juzi wakati wa sherehe ya kuwaaga wanafunzi wa shule ya Charles Darwin ya Uingereza waliokuja kujitolea katika ujenzi wa ukuta na ufundishaji wa masomo mbalimbali katika shule za Fuoni na Kijitoupele.

Alisema serikali ya mkoa wa Mjini Magharibi inathamini juhudi zinazochukuliwa na wanafunzi hao katika kujitolea kwenye shughuli za kielimu, hatua ambayo itaongeza ufanisi wa upatikanaji wa elimu na kupunguza baadhi ya matatizo yaliyomo katika shule mbalimbali za mkoa huo.

"Sisi viongozi wa serikali ya mkoa huu tunapenda kuwahakikishia kuwa tunathamini juhudi zilizochukuliwa na ujumbe huu kusaidia maeneo mbalimbali ya mkoa wetu hasa katika ufundishaji wa vijana wetu, hatua ambayo inatawaongezea ujuzi," alisema Ayoub.

Pia Ayoub (pichani chini) aliwakumbusha wananchi wa mkoa huo kuendeleza utamaduni wa kushiriki na kujitolea katika shughuli mbalimbali za kijamii ili kuongeza kasi ya maendeleo katika maeneo yao na kuimarisha ustawi wa jamii.

"Ninatoa wito na kuwakumbusha wananchi wenzangu tuendelee kujitolea katika kazi za kijamii. Hili ni jukumu letu kwani maendeleo ya nchi hii tutayaleta sisi wenyewe. Tumeona wenzetu hawa wametoka nchini kwao wanatuonyesha mfano katika kufanya shughuli za kimaendeleo kwa kujitolea," alisema.

Katika hatua nyingine, Ayoub aliipongeza Taasisi ya African Adventures kwa kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za wageni hao kujitolea kwenye ujenzi wa taifa na ufundishaji wa wanafunzi kwa baadhi ya masomo.

Naye Mkurugenzi wa African Adventures, Samson Zubeir, alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na wageni hao ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi wake.



# Waziri afurahia mafanikio uchunguzi wa saratani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amesema uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kwa Zanzibar umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kugundua maradhi mbalimbali ya kinamama na kupatiwa tiba.

Hamad alisema hayo jana wakati akiwatunuku vyeti timu ya madaktari kutoka Jimbo la Jiangsu, China pamoja na madaktari na wauguzi wa Zanzibar ambao wamemaliza mradi wa awamu ya pili ya kutoa huduma za upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi.

**Naipongeza kwa dhati kabisa Wizara ya Afya kwa kufanya juhudi za makusudi za kuleta madaktari bingwa kutoka China kuja nchini na kutoa huduma za matibabu kwa wanawake.**

Alisema wananchi wengi wakiwamo wa kutoka vijijini, wamejitokeza kupata huduma hiyo ambayo ilikuwa ikifanywa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, mjini hapa.

Kwa mujibu wa Hamad, wanawake 5,181 walichunguzwa maradhi hayo, 72 kati yao waligundulika kuwa katika saratani hatua ya awali, huku 15 wakiwa katika hatua ya juu na wanahitaji matibabu.

"Wagonjwa 15 ambao wamegundulika wanayo saratani katika hatua ya matibabu, watapelekwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam kwa matibabu zaidi," alisema.

Akizungumza katika sherehe za kuwaaga madaktari hao, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, aliwataka wananchi kuzitumia fursa za kupima afya ambazo zinatolewa bure.

Mgeni alisema hatua hizo zinazotokana na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupima afya za wananchi wake ikiwa ni mikakati ya kutoa matibabu bure kwa wananchi wake.

"Naipongeza kwa dhati kabisa Wizara ya Afya kwa kufanya juhudi za makusudi za kuleta madaktari bingwa kutoka China kuja nchini na kutoa huduma za matibabu kwa wanawake," alisema.

Mratibu wa Madaktari kutoka China, Jasmine Qi Xiaomin, alisema uchunguzi wa afya za wananchi mapema zinasaidia kujua hali ya maradhi na kupata tiba sahihi kwa wakati.

Aidha, aliipongeza Wizara ya Afya kwa ushirikiano mzuri katika kipindi chote walichokuwapo nchini na kusaidia kutoa matibabu ya wananchi mbalimbali wakiwamo wanawake katika saratani ya shingo ya uzazi.

"Ushirikiano wetu tuliopata umetusaidia kwa kiasi kikubwa kufanya kazi zetu kwa mafanikio makubwa ya kutoa huduma za uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Maradhi yasiyo ya Kuambukiza, Omar Mwalimu, alisema Tanzania inaongoza katika saratani ya shingo ya kizazi katika ukanda wa Afrika Mashariki. Alisema watu 35,000 hupata saratani ya shingo ya kizazi kila mwaka lakini ni asilimia 20 tu ndio wanaofika hospitalini kupata matibabu.



Diwani wa Kata ya Ndembezi (CCM), Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, akizungumza kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Manispaa ya Shinyanga juzi, huku akivaa joho kwa madai ya kutokuwa na imani na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Geofley Mwangulumbi, kutokana na kutotekeleza maadhimio ya madiwani hao na hasa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Apigia chapuo utalii Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa utalii wametakiwa kuandaa miundombinu bora katika kuutangaza utalii katika kisiwa cha Pemba ili uimarike na kukua kwa kasi zaidi kisiwani humo.

Mkurugenzi wa Masoko Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Miraji Ukuti, alisema hayo juzi katika mkutano uliowashirikisha wadau wa utalii katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake ikiwa ni miongoni mwa shamra shamra za Bonanza la Tatu la Utalii kisiwani Pemba.

Alisema utalii ni sekta mama ambayo inasababisha kukuza na kuunyanyua uchumi wa Zanzibar kwa asilimia 27 na kuzalisha ajira kwa wananchi wake.

Aidha, alisema serikali inatoa miongozo katika sekta binafsi inayoweza kutengeneza mazingira mazuri katika kukitangaza kisiwa cha Pemba juu ya dhana nzima ya utalii kwa wote.

Naye Ofisa Takwimu kutoka Kamisheni ya Utalii kisiwani Pemba, Hamad Khamis Rashid, alisema kutoa takwimu sahihi ndiko kunakoweza kupima mafanikio ya kazi ya msingi ya kuutangaza utalii ikiwamo uhakiki, uchambuzi, ulinganishwaji na usambazaji wa taarifa zinapohitajika kwa muda na wakati uliopangwa.

Nao maofisa mapato kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), waliwataka wadau wa utalii kulipia kodi zinazohusiana na sekta hiyo kwa kuwa mapato hayo hutumika katika huduma za kijamii kama vile afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na kuweka kumbukumbu sahihi za uingiaji wa wageni.

Mdau wa utalii kutoka Mozet Tours, Omar Ali Khamis, aliitaka Kamisheni ya Utalii kuwaandaa watu maalumu wa kupokea wageni watakaoelezea uhalisia wa kianzio cha utalii, kuwaandalia mazingira mazuri ya kuvifikia vianzio ikiwamo usafiri sambamba na kupunguzwa wingi wa kodi. Alisema kufanya hivyo kutawezesha kufikiwa malengo ya utalii kwa wote.

# Waomba suluhu mgogoro wakulima, wafugaji

**Na Gideon Mwakanosya**, SONGEA

WAKULIMA wa Kijiji cha Hanga Ngadinda katika Halmashauri ya Madaba mkoani Ruvuma, wamelalamikia kuwapo mgogoro kati yao na wafugaji ambao uongozi wa serikali umedaiwa kukaa kimya na kushindwa kuwasaidia kumaliza mgogoro huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kijijini hapo, wakulima hao walisema kwa muda mrefu wamekuwa na changamoto kubwa kutokana na wafugaji kuwaachia ng'ombe kwenye mashamba na kusababisha mazao yao kuharibiwa.

Samuel Moyo, mkazi wa kitongoji cha Hanga Ngadinda alisema Julai 7, mwaka huu, majira ya saa 8:00 usiku, kundi kubwa la ng'ombe lilikutwa katikati ya shamba lake na kuwasiliana na majirani ambao waliwakamata na kuwapeleka kwenye ofisi ya kijiji.

Hata hivyo, alisema baadaye amri ilitoka wilayani kuwa ng'ombe hao waachiwe ambao walikuwa zaidi ya 60, mali ya mfugaji Saguda Mayanda.

**Mfugaji huyo alikataa kwamba hawezi kulipa kwa madai kuwa tayari ameshawasiliana na uongozi wa wilaya na ana mpango wa kwenda mahakamani kupinga tozo hizo.**

Alisema baadaye uongozi wa serikali ya kijiji, ulimtaka Mayanda alipe fidia ya gharama ya mazao yaliyoharibiwa, lakini hakulipa na ng'ombe waliamuliwa kurudishwa kwa mfugaji huyo.

Melkion Mnenuka, mkazi wa kitongoji cha Stand, naye alisema Julai 19, mwaka huu, majira ya usiku, zaidi ya ng'ombe 200 waliingia shambani mwake na kuharibu mazao.

Alisema wakati ng'ombe hao wanaingia kwenye shamba, yeye mwenyewe alikuwa katikati ya shamba akiwa analinda, hivyo alifanikiwa kuwakamata baada ya kuwasiliana na majirani pamoja na ofisa mtendaji wa kijiji ambaye baada ya muda si mrefu alifika eneo la tukio na kuwakuta ng'ombe 215. Alisema walipowahoji waliokuwa wakichunga ng'ombe hao, walidai kuwa ni ng'ombe wa Saguda Mayanda.

Mnenuka alisema mtendaji wa serikali wa kijiji hicho aliwasiliana na polisi ambao walifika kwenye eneo la tukio na kuwakamata watuhumiwa wawili na kuwafunga pingu.

Hata hivyo, alisema mmoja kati yao alikimbia akiwa na pingu mkononi na baadaye ng'ombe hao waliamuriwa kupelekwa ofisi ya serikali ya kijiji ambako mmiliki wa ng'ombe alitakiwa kulipa Sh. 10,000 kwa kila ng'ombe mmoja kama ushuru wa serikali ya kijiji na halmashauri Sh. 5,000.

Alisema mfugaji huyo alikataa kwamba hawezi kulipa kwa madai kuwa tayari ameshawasiliana na uongozi wa wilaya na ana mpango wa kwenda mahakamani kupinga tozo hizo.

Kelvin Mapunda, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mchweka, alisema kutokana na kuwapo matukio mengi ya idadi kubwa ya mifugo kukutwa kwenye mashamba ya watu, anaiomba serikali kuchukua hatua za haraka ili kuondokana na mgogoro uliopo kwenye kijiji hicho kati ya wakulima na wafugaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba, Shafii Mpenda, alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu suala hilo, alithibitisha kuwapo kwa tatizo hilo lakini alisema kuna changamoto zimeanza kufanyiwa kazi tofauti na wanavyolalamika wananchi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa eneo la Nachingwea mkoani Lindi juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hashim Mgandilwa. **PICHA: OWM**

# Polisi waua mtuhumiwa wa ujambazi

**Na Timothy Itembe**, TARIME

JESHI la Polisi katika mkoa wa kipolisi wa Tarime na Rorya, wamemuua mtu anayedaiwa kuwa jambazi, Joshua Nyamanche, anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 45 na 55, mkazi wa kijiji cha Korotambe, Tarime mkoani Mara.

Kamanda wa Polisi wa Tarime na Rorya, Henry Mwaibambe, aliwaambia waandishi wa habari ofisini kwake jana kuwa tukio hilo lilitokea Julai 28, majira ya saa 9.20 mchana katika barabara ya Nkerege wakati askari wakiwa katika msako.

"Julai 28 majira ya saa 09:20 katika maeneo ya Mtana, barabara ya Nkerege, askari polisi wa vyeo mbalimbali wakiwa kwenye doria, walipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuwa kuna majambazi wapatao watatu wamepanga kuvamia kituo kimoja cha mafuta mjini Tarime.

"Polisi hao walifanikiwa kuwaona walipo na baada ya majambazi hao kugundua kuwa wanafuatiliwa, walianza kurusha risasi kwa askari polisi hao ndipo askari walianza kujibu mashambulizi na kufanikiwa kumpiga risasi jambazi moja mgongoni aitwaye Joshua Nyamache," alisema Mwaibambe.

Kamanda Mwaibambe aliongeza kuwa katika tukio hilo, majambazi wengine wawili walitoroka na Jeshi la Polisi linaendelea kuwatafuta huku likiwataka wasamamria wema kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kukomesha uhalifu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Tarime/Rorya, Mrakibu Mwandamizi (SSP) George Katambazi, alisema kuwa jambazi huyo alikutwa akiwa na bastola ambayo imefutwa namba ikiwa na risasi tatu kwenye magazine, huku katika eneo la tukio kuliokotwa maganda mawili ya risasi za bastola.

Katambazi aliongeza kuwa jambazi huyo alifariki dunia muda mfupi akiwa njiani akipelekwa katika hospitali ya wilaya kwa ajili ya matibabu.

# Mamilioni yatengwa kumaliza utapiamlo

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Sh. milioni 342.4 kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuwahudumia watoto 65,315 wenye umri chini ya miaka mitano wenye ugonjwa wa utapiamlo mkali.

Mratibu wa Lishe kutoka Halmashauri ya Ushetu, Hadija Nasibu, alibainisha hayo jana wakati wa utiaji saini katika mikataba ya kupambana na utapiamlo na watendaji wa kata na vijiji kutoka kata 20 zilizoko katika halmashauri hiyo.

Alisema halmashauri imekuwa ikitenga bajeti ya lishe kuvuka lengo la Sh. 500 kwa kila mtoto aliye chini ya umri wa miaka mitano na kuongeza kuwa kwa mwaka wa fedha uliopita, zilitengwa Sh. milioni 276.8 na Sh. 1,000 zilitolewa kwa kila mtoto.

Nasibu alisema asilimia 28 ya watoto chini ya umri wa miaka mitano mkoani Shinyanga wamedumaa na kuongeza kuwa kiwango cha utapiamlo mkali kwa Halmashauri ya Ushetu ni asilimia 0.076 na hali hii inaonyesha utapiamlo katika halmashauri hiyo ni mkubwa kulinganisha na halmashauri zingine.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka 2015/16 halmashauri ilitenga Sh. milioni 57.2 kwa watoto 73,056 na kila mtoto alipata shilingi 784, huku mwaka 206/17 walitenga Sh. milioni 70.8 kwa watoto 73,056 na kila mtoto alipata Sh. 970.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2017/18, walitenga Sh. milioni 140.05 kwa ajili ya watoto 73,056 na kila mtoto alipata Sh. 2,040 huku mwaka 2018/19 zilitengwa Sh. milioni 276.8 kwa watoto 64,550 na kila mtoto alipata Sh. 4,280.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Nicodemus Senguo, alisema asilimia kubwa ya wananchi wa Ushetu wamekuwa wakilima chakula kingi lakini lishe iko chini kulinganisha na wingi wa chakula kilichopo.

ITV
IJUE SHERIA: SAA 12:30 JIONI
JE, UNAFAHAMU SHERIA YA MIRATHI, SHERIA ILIUNDWA KWA MALENGO GANI, WAHUSIKA WAKUU NI KINA NANI NA MAMLAKA GANI INA UWEZO WA KUSIKILIZA MASHAURI YAHUSUYO MIRATHI.

## HABARI KIMATAIFA

# Wafungwa 57 wafariki dunia kwenye ghasia gerezani

**SAO PAULO, Brazil**

HALI ya wasiwasi inaendelea kutanda katika jela ya Altamira, Kaskazini mwa Brazil, baada ya wafungwa 57 kuuawa Jumatatu wiki hii katika makabiliano kati ya makundi hasimu.

Hali hiyo imeendelea kujitokeza katika eneo hilo la kimkakati ambako makundi hasimu ya wahalifu yanaendelea kupigana kuhusu biashara ya dawa za kulevya.

Mamlaka ya magereza imeeleza kuwa kati ya wafungwa hao, 16 wamepatikana wakiwa wamekatwa vichwa.

Uhasama huo, ambao ulianza majira ya saa 7:00 asubuhi saa za Brazil katika jela la Altamira iliyopo Jimbo la Para, katikati mwa msitu wa Amazon, ulimalizika mapema mchana.

**"Inawezekana kwamba wafungwa wengi wamefariki dunia kwa kukosa hewa," alisema msemaji wa mamlaka ya magereza.**

"Askari magereza wawili walitekwa, lakini waliachiliwa haraka kwa sababu lengo ilikuwa ulipizaji kisasi kati ya makundi hasimu na sio ghasia za kupinga mazingira ya kizuizini," alisema Gavana wa Para, Jarbas Vasconcelos.

Wafungwa kutoka kundi la wahalifu waliingia katika sehemu walikokuwa wanafungwa wafungwa wa kundi lingine hasimu kabla ya kuwachoma moto.

"Inawezekana kwamba wafungwa wengi wamefariki dunia kwa kukosa hewa," alisema msemaji wa mamlaka ya magereza.

Video iliyorushwa kwenye mitandao ya kijamii ilionyesha vichwa sita vya wafungwa vimewekwa karibu na ukuta.

Wizara ya Sheria nchini Brazil imesema kuwa mchakato wa kuwahamisha wafungwa waliohusika na ghasia hizo kwenda jela mbalimbali umeanza.

Ilieleza kuwa hali hiyo haitojirudi tena katika magereza, kwani usalama wa kutosha utaimarishwa.

**RFI**

# UN yataka uchunguzi mauaji ya wanafunzi

**KHARTOUM, Sudan**

UMOJA wa Mataifa (UN) umetaka kufanyike uchunguzi wa mauaji ya wanafunzi watano yaliyotokea wakati wa maandamano ya raia nchini Sudan ya kushinikiza serikali ya kiraia kabla ya mazungumzo kuhusu serikali ya mpito nchini humo.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, (UNICEF) limetoa wito kwa mamlaka kuchunguza na kuwatia hatiani watuhumiwa waliohusika na ukatili huo dhidi ya watoto na kuongeza kuwa hakuna mtoto atakayezikwa akiwa na sare za shule.

Wanafunzi waliouawa walikuwa wa umri wa miaka kati ya 15-17.

Wakati UNICEF ikitoa wito huo, kiongozi wa baraza la kijeshi nchini Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan amelaani mashambulizi dhidi ya wanafunzi hao na kuyaita ni uhalifu usiokubalika, hii ikiwa ni kulingana na kituo cha televisheni cha serikali. Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alinukuliwa na kituo hicho wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Sudan akisema kile kilichotokea Al-Obeid ni cha kusikitisha.

Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alisema: "Kuwaua raia walioandamana kwa amani ni uhalifu usiokubalika na wahalifu wanatakiwa kuwajibishwa mara moja".

Waandamanaji wanavituhumu vikosi vya jeshi vinavyoongozwa na Jenerali mwenye mamlaka makubwa nchini humo, Mohamed Hamdan Dagalo kwa mauaji hayo ya vijana watano, wakati wa maandamano hayo katika mji wa Al-Obeid.

Jana katika Mji Mkuu wa Khartoum, mamia ya raia waliandamana kwenye mitaa ya al-Riyadh na Burri kufuatia mauaji ya waandamanaji, pamoja na wanafunzi hao.

Mmoja wa waandamanaji, Hassan Osman, aliliambia Shirika la Habari la AFP kwamba: "Mahitaji yetu ni serikali ya kiraia kwa sababu itatoa haki kwa mashahidi hawa waliouawa. Kila siku watu wanauawa, tunataka chombo huru ama cha kimataifa kuchunguza, kwa sababu hatuamini mfumo wa mahakama. Kila siku watu wanakufa, kama huko al-Obei.

Wanafunzi hao waliuawa wakati viongozi wa kiraia wakijiandaa kufanya mazungumzo na majenerali wa baraza la kijeshi ya kukamilisha mchakato wa kuanzishwa kwa serikali ya kiraia, wiki mbili baada ya kutiliana saini makubaliano ya kugawana madaraka mwanzoni mwa mwezi.

Serikali ilitangaza amri ya kutotembea nyakati za usiku katika miji minne iliyopo Jimbo la Kordofan Kaskazini kufuatia vifo hivyo, wakati makundi ya waandamanaji yakiitisha maandamano ya nchi nzima dhidi ya mauaji hayo. Shule zote za eneo hilo pia zimeamriwa kusitisha masomo.

***DW***



Wananchi wa Sudan wakifanya fujo barabarani kwa kuchoma moto mataili ya magari kuashiria kuchukizwa na kitendo cha wanajeshi wa nchi hiyo kuwaua wanafunzi. **PICHA: REUTERS**

# Kabila, Tshisekedi wakubaliana muundo wa serikali

**KINSHASA, Congo**

HATIMAYE Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi na mtangulizi wake, Joseph Kabila wamekubaliana kuhusu muundo wa serikali ya mseto ambayo itakuwa na mawaziri na manaibu waziri 65.

Wajumbe kutoka pande mbili hizo wametia saini mkataba rasmi wa madaraka, ambao wamesema kutakuwako na kamati ya ufuatiliaji wa mkataba huo. Serikali imetarajiwa kutangazwa mnamo wiki mbili zijazo.

Mkataba huo umefanyika majira ya saa 6:00 usiku kuamkia jana baada ya siku kadhaa za mazungumzo ambayo hayakuwa mepesi.

Mwakilishi wa Chama cha FCC, Nehemie Mwinyala, alisema Rais Tshisekedi na Kabila walionyesha uzalendo ili kufikia sio tu mageuzi ya amani kwenye uongozi wa taifa bali pia makubaliano kwa ajili ya serikali ya muungano baina ya vuguvugu la FCC na lile la CASH baada ya kufanyika kwa mazungumzo marefu.

Mkataba huo wa kuwapo na serikali ya mseto unaelezea kwamba Baraza la Mawaziri litakuwa na mawaziri 65.

Katika mgawanyo huo, FCC inayoongozwa na Kabila itachukuwa mawaziri 42 na CASH ya Rais Tshisekedi wizara 23.

Hata hivyo, mkataba huo haukufafanua ni wizara gani kila upande utachukua.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Rais Tshisekedi atamteua Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Bajeti na Uchumi na Gavana wa Benki Kuu, huku Joseph Kabila akipewa wadhifa wa kumteua Waziri Mkuu, Wizara ya Ulinzi, Sheria, Fedha na Akiba.

Jean-Marc Kabund A Kabund, kiongozi wa muda wa chama cha UDPS na aliyemwakilisha Rais Tshisekedi kwenye mazungumzo hayo alisema kwamba lengo la serikali hiyo ya mseto ni pamoja na kuendesha mageuzi ya sekta ya sheria na uchumi.

Alisema mkataba huo unazingatia mikakati itakayomwongoza Waziri Mkuu katika kuunda baraza lake la mawaziri ambalo litaidhinishwa na Rais.

Ni miezi sita sasa tangu kuapishwa kwa Rais Tshisekedi lakini hakujakuweko na serikali mpya.

Waziri Mkuu Sylvestre Ilunga aliyeteuliwa Mei 20 alishindwa kuunda serikali.

Alitakiwa kusubiri hadi kuwapo na makubaliano ya ugavi wa madaraka ili kuteua baraza lake la mawaziri.

Katiba ya Congo inaelezea kwamba chama chenye wingi wa viti bungeni ndicho kinamteua Waziri Mkuu.

Vuguvugu la FCC la Rais mstaafu Joseph Kabila ndilo limeshikilia wingi wa viti bungeni na pia kwenye baraza la seneti.

Jumamosi iliyopita, aliyekuwa Waziri wa Sheria, Alexis Thambwe Mwamba ndiye aliyechaguliwa kuwa Spika wa Bunge.

Viongozi wa upinzani wa vuguvugu la Lamuka wanatarajiwa kukutana mjini Lubumbashi ili kutoa msimamo wao kuhusu hali ya kisiasa nchini humo. Mkutano huo utakaoongozwa na Moise Katumbi, umehudhuriwa pia na Martin Fayulu na Adolphe Muzito.

Lakini, Jeanpierre Bemba hatoweza kuhudhuria kikao hicho kwa kile alichokieleza ni ndege yake kuwa na hitilafu huku akiwakilishwa na Eve Bazaiba Katibu Mkuu wa chama chake cha MLC.

***DW***

# Mahakama yaridhia mali Mbeya Club kuchukuliwa

**Na Salome Kitomari**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, imeridhia ombi la Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (Rita) kumiliki wa mali za iliyokuwa Mbeya Club kama Mdhamini wa Umma (Public Trustee) kwa niaba ya serikali.

Mbeya Club ni taasisi iliyokuwa inamiliki maeneo mbalimbali yakiwamo ya michezo katika Mkoa wa Mbeya.

Rita kama mdhamini wa umma ilifungua shauri Mahakama Kuu kuomba kuzisimamia mali za iliyokuwa Mbeya Club kutokana na uhai wa bodi ya wadhamini wake kuisha kisheria hivyo kukosa mamlaka ya kuendelea kusimamia mali za taasisi hiyo.

Mahakama imeridhia ombi hilo kupitia hukumu iliyotolewa na Jaji Dustan Ndunguru ya Juni 26, mwaka huu.

Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu ambaye ndiye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Emmy Hudson, alisema taasisi hiyo kwa muda mrefu imekuwa haina bodi ya wadhamini, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kusimamia mali za taasisi.

Alisema taasisi hiyo kwa kipindi kirefu imeshindwa kuipa uhai bodi kwa kutokufanya marejesho ya kila mwaka kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura ya 318 Toleo la 2002.

Kwa mujibu wa Hudson, Rita ilitangaza kusudio la kuzifuta Bodi ya Wadhamini ya Mbeya Club na kuipa muda ya kurekebisha upungufu uliyoko kwa wakati, lakini ilishindwa kutimiza matakwa hayo kwa wakati, hivyo kulazimika kuifuta bodi hiyo kupitia tangazo la serikali Na.1104 la 5 Agosti, 2016.

Rita ilifungua shauri la kuomba kuzisimamia mali zote ya taasisi hizo kwa mujibu wa Sheria ya Mdhamini wa Umma Sura ya 31 kifungu cha saba na hukumu kutolewa na Jaji Ndunguru.

"Rita ndiyo taasisi yenye dhamana ya kusajili na kusimamia utendaji kazi wa bodi za wadhamini wa taasisi na tunazisihi taasisi zote zinazomiliki mali kusimamia mali kwa uadilifu na ufanisi," alisema.

**"Rita ndiyo taasisi yenye dhamana ya kusajili na kusimamia utendaji kazi wa bodi za wadhamini wa taasisi na tunazisihi taasisi zote zinazomiliki mali kusimamia mali kwa uadilifu na ufanisi," alisema.**

# MOI kutoa huduma X-Ray kwa mtandao

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imejipanga kuanza kutoa huduma za mionzi kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kusoma picha za X-Ray.

Kupitia huduma hiyo, mashine za kisasa zitafungwa katika taasisi hiyo kwa ajili ya kupokea picha zitakazotumwa kutoka katika hospitali mbalimbali nchini na madaktari bingwa wa mionzi watazisoma na kurudisha majibu kwa muda mfupi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alibainisha hayo juzi wakati akikagua chumba hicho maalum cha kusomea picha za X-Ray katika taasisi hiyo.

Alisema kuwapo kwa chumba hicho na mashine za kisasa kutawezesha mgonjwa kupata majibu ya tatizo alilo nalo ndani ya muda mfupi na kuanza kupatiwa matibabu.

"Serikali imejikita kununua mashine za kigitali za X-Ray zitakazofungwa katika mtandao kwa ajili ya kusoma picha zitakazopigwa katika hospitali yoyote nchini, zitatumwa, zitasomwa na majibu kurudishwa ndani ya muda mfupi," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema huduma hiyo itaokoa gharama za kuajiri idadi kubwa ya madaktari bingwa wa mionzi, lakini wataondokana na mifumo ya zamani ya kusafisha picha na kurudisha majibu kwa daktari.

"Badala ya kuweka picha katika chumba cheusi katika mfumo ambao unatumika sasa, madaktari wetu wataanza kutumia kompyuta kusoma picha hizo zitakazotumwa kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Respicious Boniface, alisema wana madaktari bingwa wa mionzi ambao wana uwezo wa kutoa huduma hizo kwa ufanisi na wapo tayari kwa ajili ya kufanya kazi kwa saa 24.

Naye daktari wa mionzi, Mechris Mango, alisema kitengo hicho kinaweza kusoma picha 300 za X-Ray kwa siku na kurudisha majibu kwa mgonjwa kwa muda mfupi.

"Kitengo chetu tunapokea picha za X-Ray ambazo tunatumia teknolojia ya kompyuta kuzisoma na kurudisha majibu muda mfupi, urahisi wake ni kama kupokea ujumbe mfupi wa maneno na kurudisha majibu kwa uharaka huo huo," alisema Dk. Mango.

Alisema picha zitakazotumwa ni zile ambazo madaktari wameshindwa kuzisoma kwa urahisi, hivyo kutakiwa kutumia utaalamu zaidi kusoma kutoka katika kitengo hicho kuziandikia ripoti ya majibu ya tatizo lililobainika.




Maofisa mauzo wa Zantel wakitoa elimu kuhusu promosheni ya kampuni hiyo ya mawasiliano kisiwani Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima 80,000 kunufaika mradi wa PASS na AFDB

**Na Zuwena Shame**

ZAIDI ya wakulima wadogo 80,000 wanatarajiwa kunufaika na mikopo kupitia mradi uliozinduliwa na Taasisi ya Kilimo(PASS) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika(AfDB).

Mradi huo mpya unakusudia kuwawezesha kifedha wakulima wadogo pamoja na sekta nzima ya kilimo kupitia mikopo ya miradi ya dhamana na malipo ya bima.

Katika mkataba uliotiwa saini na pande hizo mbili zinazoshirikiana kuendesha mradi huo, PASS itakuwa na jukumu la kuangalia namna ya utekelezaji wa mradi huo nchini na katika nchi nyingine za kiafrika ikiwamo Ghana, Uganda na Zimbabwe.

Meneja wa AFDB nchini, Alex Mubiru, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha kilimo na kuwa na uhakika wa mazao kwa wakulima wadogo nchini.

"Huu ni ukuaji mkubwa kwetu sisi PASS na pia tunashukuru kwa kupewa nafasi kuongoza mradi huu, tutafanya kazi pamoja na kushirikiana kwenye matokeo mazuri na nchi nyingine," Mubiru alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo wenye thamani ya Dola Marekani 980,000, unakadiriwa kuwa wa miaka miwili na nusu.

Alisema PASS itakuwa inafanya kazi na taasisi mbalimbali ikiwamo kampuni za bima na taasisi za mikopo ili kuwezesha uchukuaji kilimo na kupunguza upotevu wa mazao na kupunguza matatizo yanayosababishwa na mnyororo wa hali ya hewa.

Wadau wengine wakubwa katika mradi huo ni Benki ya Dunia (WB), Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Japan.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA

### CHETI KIMEPOTEA



**MEDYLINE MATHIAS KAZULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0800.0039.2016** kilichotolewa na LOYOLA HIGH SCHOOL mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/158710/2019.**

115350802


### KUPOTEA KWA CHETI



**Kulwa Mahila Ntambi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1334/0015** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa katika Shule ya sekondari Mhongolo Progressive. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/KIG/RB/15778/2019**

115351302


### CHETI KIMEPOTEA



**ABDALLAH MAGANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0367-055** kilichotolewa na KILOSA SEKONDARI mwaka 1989. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/JNI/RB/170169/2019.**

115350702

### VYETI VIMEPOTEA



**JUSTINE PHILEMON RUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1840/0168 kilichotolewa na **KIMASEKI SEKONDARI** mwaka 2009. Cheti cha Chuo namba **TIA/SGD/DA/2011/2012/251** kilichotolewa na T**ANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY – SINGIDA CAMPUS** mwaka 2013.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi (kidato cha nne: MBI/RB/904/2019. Cheti cha Chuo: MBI/IR/803/2019.**

115347302

**JAMUHURU WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 50/2019**

Ombi la **YUSUPH RAMADHANI MBUGE** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu R**AMADHANI YUSUPH RAMANI**

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 01/08/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa.

Tarehe 23/07/2017

115350302

### KUPOTEA KWA CHETI



Mashukura Habibu anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu kilichotolewa mwaka 2015 na chuo cha Ualimu Patandi mchenye namba ya mthihani E.0526/0020 cheti chenye namba GC150000020.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: UD/RB/1607/2019**

115352202

### KUPOTEA KWA CHETI



**Jacob Florian Chawala** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.138/0079** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari Mpwapwa.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo choctote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: UD/RB/614/09**

115352302

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FINNIE AMEN URASSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 293 BBU NISSAN X-TRAIL.** Chassis namba NT30041482. Engine namba QR20115469A.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/173407/2019.**

115352002

**Summons to show cause why execution of Decree should not issue (O 21 r 37)**
**TANZANIA**
**IN THE RESIDENT/DISTRICT MAGISTRATES COURT OF AT MOSHI**
**FRANCIS PAUL KANGONGOLE ) PLAINTIFF**
**VERSUS**
**DEMETRIUS STEPHEN MGALAMI) DEFENDANT**

TO :
DEMETRIUS STEPHEN MGALAMI
WHEREAS: FRANCIS PAUL KANGONGOLE
Has have made application to this Court for execution of the decree in the above Case, you are hereby required to appear before this Court on the 15 day of August 2019 at o clock in ……..noon to show Cause why execution of the said decree should not issue.

GEVEN under my hand and the seal of the Court this 18 day of July 2019

215352502

**JAMHURI UA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya BUKOBA MJINI**
**Wilaya BUKOBA**
**MIRATHI NAMBA. 37 YA 2012**
**AMIDA IDD ALLY……………………MDAI**
**Anamdai**
**MWANNE IDD ALLY……………………. MDAIWA**
**Kwa K/K**

Kwa kuwa Mdai/ Wadai* ameleta /wameleta madai* yake/yao kwamba. Eleza hapa habari za madai:-

**MIRATHI**
Kwa hiyo* unaitajika/mnaitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMA TATU tarehe 26/8/2019 saa 2:30 asubuhi kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria / hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa kuwa* umeshindwa/mmeshindwa.

Kuitwa shaurini kumetolewa kwa maombi ya **AMIDA IDD ALLY**
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo terehe 24/7/2019

115352702

### KUPOTEA KWA CHETI



**Raif A. Abdallah** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1060/0187** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya **St. Mary's Sekondari.**

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa Control Namba: 991089019543**

115350602

### Eneo la biashara (Yard Plot) mita za Mraba 2,723 linauzwa.

Eneo (yard) Lina hati miliki, Kuna maji na umeme pia.

Eneo lipo Msamvu Morogoro, kandokando ya barabara ya Iringa, karibu na BM Garage

Eneo linafaa kwa matumizi ya kiwanda, maegesho ya malori, Hoteli, Hostel, maofisi, maghala n.k,

Kwa mawasiliano:
godlisten.minja@greenresources.no
+255 714 432 979

215338701

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI NA. 163/2018 NA 293 OF 2018**
**ESTER MARTIN ASSENGA……………………………MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**BEATRICE DONATH SHUWA ALIS & WENZAKE**
**WATATU………………………MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: BEATRICE DONATH CHUWA ALIS**
**BEATRICE MARTIN ASENGA**
**CDJ CLASSIC GROUP LIMITED**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi.Shauri limepangwa kutajwa tarehe 20/08/2019 saa mbili na nusu(2:30)asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti P MKWANDI, hivyo unatakiwa kufika mahakamani nyie au mawakili wenu.

ANGALIA: Kama hutohudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo 25 mwezi Julai, 2019.

P. MAKWANDI
MWENYEKITI

215352602

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# ZENIT YAMWANIA MALCOM

**MOSCOW, Urusi**

RAIS wa Zenit St Petersburg, Alexander Medvedev, amethibitisha kwamba wapo kwenye mazungumzo na Barcelona juu ya mpango wa kumsajili, Malcom.

Klabu hiyo ya Urusi imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, lakini Medvedev amebainisha kwamba, ada wanayoitaka Barcelona ya pauni 36 imekuwa kikwazo cha makubaliano.

Medvedev ameiambia televisheni Fontanka: "Mazungumzo kuhusu Malcom na Barcelona yapo kwenye hatua nzuri na tunapitia kwenye awamu muhimu ya maamuzi.

Akizungumza bei wanaoitaka Barcelona, Medvedev amesema kwamba, pauni milioni 36 ni nyingi zaidi kwako na haina uhalisia."

Zenit sio klabu pekee inayomwania Malcom kipindi hiki cha majira ya joto, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zimekuwa zikihusishwa nae, ambazo ni Everton, Arsenal na Tottenham.

Malcom anataka kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara jambo ambalo pale Barcelona inaonekana kuwa ngumu kwake tangu atue kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Msimu uliopita Malcom alicheza mechi 15 pekee kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na alifunga bao moja pekee.

Licha ya mkataba wake pale Nou Camp kuendelea hadi mwaka 2023, Malcom anaweza kuondoka Barcelona moja kwa moja kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

## KHEDIRA KUPUNGUZIWA MSHAHARA ATUE ARSENAL



**LONDON, England**

SAMI Khedira yupo tayari kupunguziwa mshahara wake ili ajiunge na klabu ya Arsenal kipindi hiki cha majira ya joto.

Kiungo huyo wa Juventus kwa sasa anaingiza mfukoni pauni milioni 5.5 kwa mwaka ikiwa na maana kila wiki analipwa pauni 106,000.

Kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport, washikabunduki hao wanataka kumpa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya euro milioni 3.7 kwa mwaka na atakuwa akichukua pauni 70,000 kwa wiki.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 yupo katika msimu wake wa mwisho katika mkataba wake pale Turin na anaona atakuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza katika dimba la Allianz.

Kikosi hicho cha kocha, Maurizio Sarri tayari kimemsajili Aaron Ramsey kutoka Arsenal na Adrien Rabiot kitu ambacho kinaonyesha kuwa safu ya kiungo ya kibibi kizee hicho ina wachezaji wengi, kwa kuwa Miralem Pjanic, Blaise Matuidi, Rodrigo Bentancur na Emre Can tayari wapo pale Juventus.

Khedira alionekana kwenye uwanja wa Emirates Jumapili wakati Arsenal ilipocheza mechi ya kirafiki dhidi ya Lyon.

Akizungumza baada ya mchezo huo, kocha wa Arsenal, Unai Emery alisema: "Ni mchezaji mzuri, lakini leo ndio kwanza nimemsikia akitajwa."

Kitu kingine kinachoweza kumfaya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kutua kwa miamba hao wa London Kaskazini kwa sababu ni rafiki wa karibuni mno na Mesut Ozil.

## GODIN ATAJA SABABU KUITOSA MAN UNITED

**MADRID, Hispania**

GWIJI wa Atletico Madrid, Diego Godin, amebainisha kwanini alikataa fedha kubwa na kuipiga chini ofa ya kujiunga na Manchester United msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa Uruguay aliamua kuondoka Madrid na kutua Milan mwishoni mwa msimu wakati mkataba ulipomalizika na Atletico, lakini alikuwa na nafasi ya kutua pale Old Trafford mwaka mmoja uliopita.

Badala yake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 akaamua kuendelea na mwaka mwingine pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano, na kukataa nafasi ya kuungana na kocha, Jose Mourinho.

"Ndio mwaka mmoja uliopita kulikuwa na ofa kutoka Juventus, Manchester United na mwanzoni kutoka Man City," alisema Godin akiliambia Gazzetta dello Sport.

"Lakini wakati ule nilikuwa bado nina mkataba na Atletico, sikufikiria kuhusu kuondoka. Wakati huu mambo yalikuwa tofauti, nilikuwa nakaribia mwisho wa mkataba wangu."

Godin amejiunga na Inter Milan kwa uhamisho huru mwanzoni mwa kipindi hiki cha majira ya joto, na kumaliza kipindi chake cha miaka tisa ya kucheza pale Atletico.

Kwa beki huyo wa kati mkongwe mambo yalikuwa tofauti wakati alipofuatwa na Inter Milan.

"Naweza kusema hakuna klabu iliyoweza kunishawishi kama ilivyofanya Inter," aliongeza kusema.

"Walikuja kwangu na walikuwa na ushawishi mkubwa zaidi kuliko klabu nyingine zilivyofanya. Walinionyesha mipango yao na matarajio yao yalivyo makubwa.

"Na nilipenda wazo la kuwa sehemu ya wachezaji ambao wanaweza kuisaidia Inter na nikaamua kujiunga nao."



# JUVENTUS
## WAMPASHA DYBALA KUUZWA

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imemwambia Paulo Dybala kwamba wanajiandaa kusikiliza ofa zitakazotolewa kwa ajili yake kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kuongezeka kwa sintofahamu kuhusu wapi atafiti kwenye timu hiyo chini ya kocha, Maurizio Sarri.

Dybala alikuwa na changamoto msimu uliopita kucheza sambamba na Cristiano Ronaldo na timu za Tottenham Hotspur na Manchester United zinaaminika kwamba zinasaka saini ya mchezaji huyo.

Kwa mujibu wa Goal.com Juventus inataka kumtumia Dybala kupata fedha za kununulia wachezaji wengine, ingawa mchezaji mwenyewe amebainisha mpango wake wa kutotaka kuondoka klabuni hapo.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Dybala mwenyewe anapanga kukutana na Sarri baada ya kutoka likizo na anataka kuzungumza naye kuhusu namna gani atafiti kwenye timu hiyo chini ya kocha huyo raia wa Italia msimu ujao.

Juventus wameripotiwa kwamba wamepokea ofa ya kumuuza Dybala lakini haijafikia kiwango wanachokitaka cha euro milioni 100.

Juvetus pia wanapanga kuangalia namna nyingine ya kuachana na Dybala hata kama hawatakuwa na ofa wanazozitaka.

Juventus wanapanga kumuuza mchezaji huyo ili waweze kumsajili nyota wa United, Romelu Lukaku, ambaye anaonekana kutakiwa kwa udi na uvumba na miamba hao wa soka la Italia.

Thamani ya Lukaku inatajwa kuwa ni euro milioni 82 na wao wanataka kwanza Dybala auzwe ili waweze kupata fedha za kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

# PSG YAMSAJILI RASMI GUEYE

**PARIS, Ufaransa**

**PARIS Saint-Germain imetangaza kukamilisha usajili wa kiungo, Idrissa Gueye kutoka Everton kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 32, ambazo zinaweza kuongezeka kupitia bonasi.**

**Kwa mujibu wa ESPN FC, mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alifanyiwa vipimo vya afya yake Jumatatu nchini Ufaransa kabla ya kusaini mkataba wa miaka minne na timu yake hiyo mpya inayotumia uwanja wa Parc des Princes.**

**PSG ilishindwa kumsajili Gueye mwenye umri wa miaka 29 Januari mwaka huu, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Aston Villa sasa atarudi tena kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwa mara ya kwanza tangu alipoondoka Lille kwenda pale Villa Park mwaka 2015.**

**"Najisikia fahari kusaini Paris Saint-Germain," alisema Gueye.**

**"Baada ya kuitumikia Senegal kwenye michuano ya AFCON, nilitaka kupata changamoto mpya na sasa nimejiunga na Paris Saint-Germain, moja ya timu iliyojiimarisha na kujiwekeza zaidi barani Ulaya.**

**"Napenda kuwashukuru wakurugenzi, kocha pamoja na benchi lake la ufundi kwa imani waliyoonyesha kwangu.**

**"Nitafanya kila niwezalo kuthibitisha imani yao kwangu na kuhakikisha natumia vizuri kipaji changu kwa kuisaidia timu hii. Baada ya miaka minne ya kucheza kwenye Ligi Kuu ya Engand, mitatu akicheza pale Everton, Gueye amejiunga na PSG kwa maombi ya kocha, Thomas Tuchel baada ya Mkurugenzi wa michezo wa zamani, Antero Henrique kushindwa kumsajili Januari.**

**Baada ya kuwa na tatizo kwenye nafasi ya kiungo kwa muda mrefu, PSG sasa watakuwa wameiimarisha nafasi hiyo, kwani sasa itakuwa chini ya Gueye, Paredes, Marco Verratti na Ander Herrera.**

# MARCOS ROJO ATAKA KUONDOKA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MARCOS Rojo anafikiria uwezekano wa kuondoka hapo Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto, wakati klabu hiyo ya Old Trafford ikiwa kwenye harakati za kumsajili Harry Maguire.

Beki huyo wa kati raia wa Argentine anaamini kwamba nafasi yake ya kucheza msimu ujao itakuwa finyu licha ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya nchini Australia na Mashariki ya mbali. United wanakaribia kukamilisha usajili wa beki wa Leicester City na timu ya taifa ya England, Maguire, ambaye alikosa kufanya mazoezi Jumatatu kwa sababu ya kuwa mgonjwa.

Ujio wake kwa namna yoyote utaifanya nafasi ya Rojo kucheza ni ndogo ambapo pia anakabiliwa na ushindani wa kuwania namba kutoka kwa Victor Lindelof, Chris Smalling, Phil Jones, Eric Bailly na Axel Tuanzebe.

Kwa mujibu wa ESPN FC, Rojo amekuwa anawaniwa na klabu za nchini Italia, Ufaransa na Hispania kama atachagua kuondoka United baada ya miaka mitano.

Rojo mwenye umri wa miaka 29, alisaini kujiunga na United kutoka Sporting Lisbon kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 16 wakati Louis van Gaal alipochaguliwa kuwa kocha kipindi cha majira ya joto mwaka 2014.


Muargentina huyo amecheza jumla ya mechi 113 kwa klabu hiyo, akishinda taji la FA na lile la EFL.

Lakini kutokana na kusumbuliwa na majeruhi nafasi yake ya kucheza imekumbwa na ushindani na hivyo Rojo alicheza mechi 14 tu za ligi kuu tangu mwanzoni mwa msimu wa 2017-18.

Kocha, Ole Gunnar Solskjaer alibainisha kwamba beki huyo ameichukua nafasi yake baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia katika dakika 45 za mwanzo wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Tottenham Hotspur mjini Shanghai wiki iliyopita.

Rojo pia alijumuishwa kwenye kikosi cha wachezaji 26 wa United ambacho kimesafiri mjini Oslo kwa mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya mji wa nyumbani kwake, Solskjaer, Kristiansund jana Jumanne.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ATANGAZA KURUDI TENA MADRID

Nilijuta nilipoondoka, ninazikosa zote Manchester na Madrid, lakini watoto wangu na mchumba wangu walizaliwa hapa, hivyo...

**MADRID, Hispania**

Cristiano Ronaldo amesema "anatumai kurudi Madrid mapema" kauli hiyo akiitoa baada ya nyota huyo wa Juventus kutunukiwa tuzo ya Marca Leyenda.

Ronaldo alipewa heshima hiyo jijini Madrid, ambapo mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] aliitwaa kutokana na "mafanikio yake katika soka la kulipwa na kiwango alichokipata duniani kote."

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34 kwa sasa, amefurahia mafanikio yake ya kushangaza wakati akiwa na Madrid kabla ya kujiunga na Juve msimu wa 2018-19, ambapo alikuwa mfungaji wa wakati wote kwenye klabu hiyo ya Hispania akicheka na nyavu mara 450 katika mechi 438 alizoichezea.

Ronaldo pia alitwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne na ubingwa wa La Liga mara mbili hayo yakiwa ni miongoni mwa mafanikio yake hapo Santiago Bernabeu.

Baada ya kupokea tuzo hiyo ya Marca Leyenda, mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United, Ronaldo aliwaambia waandishi wa habari katika hafla hiyo: "Nilijuta nilipoondoka Real Madrid.

"Ninazikosa zote [Manchester na Madrid] lakini kwa sababu hali ya maisha nimeishi miaka mingi zaidi Madrid, watoto wangu na mchumba wangu walizaliwa hapa, hivyo ninaikosa Madrid zaidi.

"Tuzo hii itakuwapo kila sehemu nzuri kwenye jumba langu la kumbukumbu. Madrid ni ya kipekee, nimesafiri sana lakini kuna miji michache kama Madrid.

"Zaidi ya tuzo hii inatokana na kila nilichokifanya Madrid. Ni taji la Hispania na inaniacha nikiwa na heshima sana. Shukrani kwa wote walioniwezesha kupata mafanikio haya. Ni fahari kwangu. Na ninatumai nitarudi Madrid mapema."

Ronaldo alifanya kipindi cha mpito kutoka Madrid kwenda Juve, kwa kuisaidia miamba hiyo ya Italia kutwaa taji la Serie A kwa mara ya nane mfululizo msimu wa 2018-19.

Nguli huyo alifunga mabao 28 katika mashindano yote msimu uliopita, 21 kati ya hayo akitupia katika ligi.

## KWA UFUPI

**PEPE KUPIMWA AFYA ARSENAL**

Nicolas Pepe anajiandaa kupimwa afya tayari kujiunga na Arsenal baada ya dili la pauni milioni 72 kukubaliwa na Lille. ***(Sky Sports)***

**MAGUIRE AISHUKIA LEICESTER**

BEKI wa Leicester City, Harry Maguire, 26, amepoteza uvumilivu na klabu hiyo na sasa beki huyo wa kati wa England amewataka 'Mbweha' hao kuongeza msukomo wa kumwezesha kutua Manchester United. ***(Sun)***

**UNITED YAIGOMEA LEICESTER**

MANCHESTER United ipo tayari kulipwa pauni milioni 70 ili kumpata Harry Maguire, 26, na si pauni milioni 90 kama ambavyo Leicester City inataka. ***(Mirror)***

**VERRATTI ATAKA NEYMAR AUZWE**

MCHEZAJI mwenza wa Neymar hapo Paris St-Germain, Marco Verratti, amesema klabu hiyo lazima imuuze Mbrazil huyo kama hana furaha na miamba hiyo ya Parc des Princes, licha ya kocha Thomas Tuchel kutamani kumbakisha. ***(Express)***

**RODRIGUEZ KUBAKISHWA MADRID**

Real Madrid imemwambia kiungo mshambuliaji Mcolombia James Rodriguez, 28, atabaki hapo Bernabeu. ***(AS - in Spanish)***

**ARSENAL 'YAKAZA' KWA PEPE**

DAU la pauni milioni 72 ambazo Arsenal inataka kulipa kwa Lille ili kuipata saini ya winga Nicolas Pepe, litajumuisha 'Gunners' hao kutanguliza kwanza pauni milioni 20 na kisha pauni milioni 52 zitafuata kwa kulipwa kwa awamu kwa kipindi cha miaka mitano. ***(Mail)***

**JUVE YAKIRI OFA KWA DYBALA**

Juventus imethibitisha uwapo wa ofa kwa mshambuliaji Muargentina Paulo Dybala, 25, huku kukiwa na kuvutiwa kwa huduma yake kutoka kwa Manchester United na Tottenham. ***(Mirror)***

**ROJO ATOA MSIMAMO UNITED**

BEKI Muargentina Marcos Rojo, 29, atazingatia kuondoka Manchester United kama ataamini uwapo wa nafasi katika kikosi cha kwanza utakuwa finyu msimu ujao. ***(ESPN)***

**MILINKOVIC-SAVIC AWEKWA SOKONI**

RAIS wa Lazio, Claudio Lotito amesema amewekа wazi wazo la kumuuza kiungo Mserbia Sergej Milinkovic-Savic, 24,- anayewindwa na Manchester United endapo patakuwapo na ofa sahihi. (Mail)

**MUSTAFI ATAKIWA MONACO**

Arsenal imepokea maombi kutoka Monaco ya kuhitajika kwa huduma ya beki wao kati, Mjerumani Shkodran Mustafi, 27. ***(L'Equipe, via Mirror)***

**MARIANO AFUATWA MADRID**

Real Madrid imepokea ofa kutoka kwa Roma na Monaco kwa mshambuliaji wao rai wa Jamhuri ya Dominican, Mariano, 25. ***(AS - in Spanish)***

**BRUCE AWAITA MASHABIKI**

KOCHA Newcastle, Steve Bruce haamini mashabiki wa klabu hiyo watajsusia mechi ya kwanza ya msimu dhidi ya Arsenal. ***(Talksport)***

**PALACE YAMGEUKIA CLARK**

Crystal Palace inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni tano kwa beki wa kati wa Newcastle United na Jamhuri ya Ireland, Ciaran Clark, 29. ***(Sun)***

**EVERTON KWA LEMINA, TOMORI**

Everton watazingazitia kumfuata kiungo wa Southampton na Gabon, Mario Lemina, 25, na beki wa Chelsea na England U-21, Fikayo Tomori, 21. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

# AZAM, POLISI TANZANIA KUTOANA JASHO CHAMAZI

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA wa Kombe la FA, Azam FC, wanatarajia kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Polisi Tanzania pamoja na Namungo FC ya mkoani Lindi, ndio timu zilizopanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche, alisema mchezo huo utakaoanza majira ya saa 1:00 usiku, utawapa sura halisi ya kuelekea kwenye mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika, ambao umepangwa kuanza na Ethiopia 1 kutoka Ethiopia.

Cheche alisema pia utasaidia kuwaimarisha wachezaji wao kuelekea mchezo wa kufungua msimu mpya ambapo watakutana na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ili kuwania Ngao ya Jamii.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na mazoezi na anaamini watafanya vema kampeni ya kuwania ubingwa wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na Ligi Kuu Bara.

"Alhamisi (kesho) tutacheza mchezo wa mwisho wa kirafiki kabla ya kuanza mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ni mchezo ambao utatupa picha halisi ya huko tuendapo," alisema Cheche.

Aliongeza kuwa wamepandisha wachezaji vijana wengi msimu huu na uamuzi huo unalenga kuongeza ushindani katika kikosi chao.

"Tumeamua kucheza na Polisi Tanzania baada ya kuridhishwa na viwango vya wachezaji waliopo katika timu hiyo, ni timu yenye ushindani ndio maana tukapendekeza tucheze nao, tunaamini itakuwa ni mechi nzuri, itakayotusaidia kujitathimini kiufundi," Cheche alisema.

Alisema kila mchezaji amejiandaa kufanya vema na malengo yao ni kufika mbali kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

**TUZO**



Mrisho Ngassa akikabidhiwa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro juzi, baada ya kuiongoza timu yake kuibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Mawenzi Market, kabla ya jana tena kikosi hicho cha mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam kuichapa Friends Rangers ya Daraja la Kwanza mabao 2-0 katika Uwanja wa Chuo cha Biblia, Bigwa, ikiwa ni muendelezo wa ushindi katika michezo yake ya kujiandaa na msimu mpya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mazoezi KMC yaongeza ubora

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO yanakwenda vema! Hiyo ni kauli ya uongozi wa KMC FC ya jijini Dar es Salaam ambayo inajiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali ya Rwanda, ambayo itachezwa Agosti 10, mwaka huu jijini Kigali.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Msemaji wa KMC FC, Anwar Binde, alisema wachezaji wa timu hiyo ambao hivi karibuni walishiriki mashindano ya Kombe la Kagame, wamezidi kuimarika na wanaamini watafanya vema michuano hiyo.

Binde alisema ushindani waliokutana nao kwenye mashindano ya Kombe la Kagame, umewasaidia kuwapa uzoefu wachezaji wake na sasa wana kikosi kinachotoa matumaini ya kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

"Wanafanya mazoezi mazuri, wanaonyesha ushindani, kikosi kina hamasa na kwa kifupi kuelekea kwenye michuano ya kimataifa, vijana wanaonyesha utofauti kila iitwapo leo, dozi ya asubuhi na jioni wanayoipata pale Uwanja wa Bora inawajenga vema, matumaini yetu makubwa ni kufanya vema katika mechi zinazotukabili," alisema Binde.

Mbali na KMC, timu nyingine inayoiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika ni Azam FC wakati Simba na Yanga zenyewe zitachuana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa.

## Mlandege yaja kivingine Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Mlandege, Abdulhamid Rashid, amesema ana matumaini makubwa ya timu yake kufanya vizuri katika msimu ujao wa Ligi Kuu Zanzibar tofauti na ilivyokuwa katika msimu uliopita.

Mlandege ilimaliza katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar msimu uliomalizika ambao ilishirikisha timu 19.

Rashid aliliambia gazeti hili jana kuwa, tayari kikosi chake kilishaanza mazoezi na kila mchezaji anaonekana yuko tayari kupambana kuwania ubingwa wa ligi hiyo baada ya kufahamu kilichowakosesha taji hilo msimu uliopita. "Tunajifua sawa sawa kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar ambao utaanza kutimua vumbi Agosti 25, mwaka huu, tunajua kila timu imejiimarisha, lakini kwa upande wetu tumejipanga kutorudia makosa," Rashid alisema.

Kocha huyo alisema ili kuwa na kikosi imara, amesajili wachezaji wapya saba na kati ya hao, watatu wanatoka Tanzania Bara.

"Timu ipo vizuri, tuna wiki moja tangu tuanze mazoezi, matumaini yangu msimu huu tutafanya vizuri zaidi, na ikiwezekana tumalize hata nafasi ya juu, kuhusu wachezaji wapya, nimesajili nyota saba na bado ninaendelea kuangalia wengine watakaonifaa, niwasajili," kocha huyo alisema na kuongeza kuwa wachezaji wake wana morali na wanaonyesha ushindani katika kuwania namba kwenye kikosi cha kwanza.

## Namungo yapata pigo ufunguzi Bara

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Namungo ambayo imepanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, itamkosa kiungo wake, Danny Joram, katika mechi za awali za ligi hiyo kutokana na kuumia mguu katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Aigle Noir, imeelezwa.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza kuwa, Joram atakaa nje ya uwanja kwa muda wa wiki nne, na baada ya hapo ataanza mazoezi mepesi ili kuungana na wenzake katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itakuwa imeshaanza.


"Mchezaji wetu Danny Joram Gustavo amefungwa plasta ngumu itakayomweka nje ya uwanja kwa muda wa wiki nne, uchunguzi wa kina wa matibabu umeonyesha alipata maumivu kwenye mfupa mdogo wa mguu, tunamwombea apone, arejee kuitumikia Namungo," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Thierry Hitimana, ameshaungana na kikosi hicho baada ya kumaliza likizo aliyopewa.

Katika kuhakikisha inafanya vema na kukabiliana na ushindani, Namungo imesajili wachezaji mbalimbali wenye uzoefu ndani na nje ya nchi akiwamo nyota Bigirimana Blaise akitokea Mbao FC.

# Michezo

Jumatano Julai 31, 2019
Nipashe



Khedira kupunguziwa mshahara atue Arsenal HABARI UK 28



Rais wa Real Madrid, Florentino Perez (kushoto), akimpongeza mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo, Cristiano Ronaldo, kwa kumkumbatia mara baada ya kutunukiwa tuzo ya Marca Leyenda juzi na kueleza matarajio yake ya kurejea Madrid. **HABARI UK. 30**

# AUSSEMS AREJEA NA SIMBA MOTO

## ●●●Waishika Orlando Pirates kwao, asema sasa wameiva kuivaa UD Songo huku akifafanua kuwa...

**NA Somoe Ng'itu**

BAADA ya jana kuhitimisha kambi yao Afrika Kusini ya kujiandaa na msimu mpya kwa kutoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Orlando Pirates, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema "tumeiva" na kwamba wako tayari kuanza kampeni ya kuwania taji la mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayotarajiwa kuanza mapema mwezi ujao.

Katika mchezo huo mkali ambao ulitawaliwa na ufundi wa hali ya juu, Simba ilikuwa ya kwanza kupata bao la kuongoza dakika ya 33 kupitia kwa kiungo Mzambia Clatous Chama huku shukrani zikimwendea pia mshambuliaji raia mweza wa Zambia, Augustine Mulenga aliyeisawazishia Orlando Pirates dakika tano kabla ya timu hizo kuelekea mapumziko.

Matokeo hayo yameifanya Simba kuhitimisha kambi yake Afrika Kusini bila kupoteza mchezo wowote kati ya minne iliyocheza ikiwa nchini humo ambapo ilianza kwa kuichapa Orbret TVET 4-0 kisha ikaikandamiza Platinum Stars 4-1 kabla ya kuanza kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Township Rollers ya Botswana na kisha Orlando Pirates.

Simba, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao msimu uliopita walifanikiwa kufika hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imepangwa kuanza ugenini dhidi ya UD Songo ya Msumbuji katika hatua ya awali ya michuano hiyo msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema kuwa kikosi chake kimeimarika na anaamini kitaanza vema katika mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Aussems alisema mechi za kirafiki ambazo timu yake imecheza, zimempa "picha halisi" ya viwango vya wachezaji wake kuelekea msimu mpya wa Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itafanyika kuanzia Agosti 23, mwaka huu.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa ushindani na morali ya wachezaji wako iko juu na hali hiyo inamfanya aamini kila mmoja yuko tayari kutekeleza majukumu yake katika kiwango cha juu.

"Nimeridhika na mazoezi ambayo tumefanya, tumepata vipindi vya mazoezi 19, kila mchezaji aliyesajiliwa ameshiriki na amepata muda wa kufanya mazoezi na kuonyesha sasa wako tayari kupambana, tunajua msimu utakuwa mgumu na wenye ushindani, hatuna wasiwasi na hilo, kwa sababu tuko tayari," alisema Aussems.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili kuwa, kikosi cha timu hiyo kitarejea leo baada ya kumaliza kambi yao iliyokuwa kwenye mji wa Rustenburg, Afrika Kusini.

"Kikosi kitarejea kesho (leo) usiku kutoka Afrika Kusini, hii ni baada ya kumaliza programu yake ya maandalizi ya msimu mpya, tunaamini matunda ya kambi hii yataonekana kwenye mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tumejipanga," alisema Magori.

Mara baada ya kurejea, kikosi hicho kitaanza kufanya shughuli mbalimbali za kuelekea Wiki ya Simba (Simba Day) ambayo itahitimishwa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Power Dynamo, utakaochezwa Agosti 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kisha kuifuata UD Songo tayari kwa mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa.

# Zahera amwaga 'sumu' Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU akiiongoza kwa mara ya kwanza katika maandalizi ya msimu mpya na kuiwezesha timu yake kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mawenzi Market kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro juzi, kabla ya jana tena kuichapa Friends Rangers ya Daraja la Kwanza mabao 2-0 safari hii wakicheza Uwanja wa Chuo cha Biblia, Bigwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera amesema kazi ya kukiweka sawa kikosi chake kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu, ndiyo imeanza rasmi.

Zahera alijiunga na timu hiyo juzi baada ya kurejea kutoka mapumzikoni Ufaransa.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Morogoro kwa niaba ya kocha huyo Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh alisema, Zahera amesema hana wasiwasi na timu yake.

"Kocha leo ameanza kazi rasmi baada ya kurudi na amesema mikakati yake ni kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa na msimu ujao," alisema Hafidh.

Alisema Zahera amefurahishwa na kiwango kinachoonyeshwa na kila mchezaji, na kueleza kuwa endapo wakiendelea hivyo ana matumaini makubwa ya kufika mbali.

Hafidh alisema kocha huyo ameahidi kufunga mahesabu ya usajili kwa kushusha nyota mmoja.

"Malengo makubwa ya kwenye usajili kwa kisasi kikubwa yamekamilika, kwa sasa kuna nafasi moja tu ya mchezaji kwa nafasi ya ushambuliaji kisha baada ya hapo tunafunga hesabu jumla," alisema.

Dirisha la usajili kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara pamoja na Ligi Daraja la kwanza linatarajiwa kufungwa rasmi leo Julai 31 majira ya saa sita usiku.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >